# Nipashe

Jumanne Februari 19, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579845

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Fatma Karume amwagiwa sifa na wadau kila kona

UKURASA 3


Nipashe

TESA

TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI

UTAFITI POMBE NAVYOATHIRI DNA NA KUONGEZA HAMU YA KUNYWA ZAIDI

Wazazi walivyo chanzo cha mimba za utotoni Bariadi

KCMC yaleta nuru wagonjwa wa saratani Kanda ya Kaskazini

UKURASA 13

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**WAZIRI AIPA MAAGIZO MANANE TUME MADINI**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ametoa maagizo manane kwa Tume ya Madini nchini, huku akionyesha...

UKURASA WA 3

**TPSF YASHTAKI MA-RC, MA-DC KISA WAWEKEZAJI**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imetoa mapendekezo tisa kwa serikali likiwamo la kuitaka...

UKURASA WA 4

**DPP AOMBA RUFANI YA MBOWE ITUPWE**

MKURUGENZI wa Mashtaka nchini (DPP), ambaye ni mlalamikaji katika rufani ya kupinga uamuzi wa...


## Polepole awaita Chadema wakorofi



UKURASA 3



# Nape ajutia kauli ‘bao la mkono’

• **Asema** ilimletea matatizo na kuwekwa kitimoto, inamsumbua na atazikwa nayo...

*Endelea ukurasa 2*

## Bwana harusi afa akitoka kuoa mke



UK. 2


**MICHEZO** **KAGERE AANZA KUAGA SIMBA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Waziri aipa maagizo 8 Tume Madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ametoa maagizo manane kwa Tume ya Madini nchini, huku akionyesha namna serikali ilivyopata hasara ya mabilioni ya shilingi kutokana na wamiliki wa leseni kutolipa malipo stahiki ya serikali.

Maagizo hayo aliyatoa jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuwaendeleza na kuwasaidia wachimbaji wadogo, kuimarisha utoaji na usimamizi wa leseni za madini nchini.

Alisema kuanzia Januari 2019, wizara ilifanya uhakiki wa leseni zote za uchimbaji madini ambazo zimetolewa na kubaini leseni nyingi zimekiuka matakwa ya kisheria.

Alieleza kuwa kuna watu wamehodhi na kushindwa kuendeleza maeneo ya utafiti waliyopewa kinyume cha kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake, hivyo kusababisha wachimbaji wengine hasa wadogo kukosa maeneo ya kuchimba.

"Pia kushindwa kulipa malipo stahiki ya serikali ikiwa ni pamoja na ada ya mwaka kinyume na kifungu cha 92(1) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017," alisema.

**MADENI YA MABILIONI**

Biteko alisema hadi kufikia mwezi huu, jumla ya leseni 18,341 kati ya 30,937 zinadaiwa Sh. bilioni 116.67 na kuagiza tume hiyo kuziandikia hati za makosa na zilipe fedha hizo ndani ya siku 30.

"Na kama wakishindwa kulipa madeni hayo ndani ya muda huo leseni hizo zifutwe ndani ya siku saba baada ya mwisho wa hati za makosa kwa mujibu wa kifungu cha 63 cha Sheria ya Madini," alisema.

Aliongeza: "Katika zoezi hili lisiangalie nani anamiliki leseni hiyo hata kama taasisi ya serikali, hata ile leseni ya Liganga na Mchuchuma ambayo inamilikiwa na NDC na mbia wake na najua inadaiwa ada Dola za Marekani zaidi ya 375,000 sheria ifuate mkondo wake."

Alifafanua kuwa katika madeni hayo leseni kubwa za utafiti(PL) zinadaiwa Sh. bilioni 61.67, leseni za uchimbaji mkubwa (SML) Sh. bilioni

INAENDELEA UK 8

# Nape ajutia bao la mkono

**Na Mary Geofrey**

MBUNGE wa Mtama, Nape Nnauye, amesema kati ya alama alizo nazo mgongoni atakayoenda nayo kaburini ni kauli aliyoitoa miaka minne iliyopita kwamba, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kingeshinda katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 hata kwa bao la mkono.

Nape alitoa kauli hiyo ya kushtusha Juni 22, 2015, akiwa katika mkutano wa CCM uliofanyika Viwanja vya Nyehunge, Sengerema mkoani Mwanza.

Mkutano huo ulikuwa miongoni mwa iliyoandaliwa katika ziara za aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Abdulrhaman Kinana, kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa chama hicho.

"Sitaki kujitetea katika hili, ingawa nia yangu haikuwa mbaya. Nami nimeshakubali, kama ni alama iliyo mgongoni kwangu ambayo nitaenda nayo kaburini, ni hii ya bao la mkono," Nape alisema jana akiwa katika mahojiano na moja ya vituo vya runinga jijini Dar es Salaam.

Alisema ameibeba kauli hiyo kama lilivyotafsiriwa huku akidai kuwa hakuwa na maana inayochukuliwa na wengi, wakiwamo wanaomtukana kutokana na kauli hiyo.

Nape aliweka wazi kuwa kabla ya suala hilo kuandikwa kwenye vyombo vya habari, Kinana alimweleza kuwa kauli hiyo haikuwa sahihi kulingana na mazingira na wakati aliotamka na akamtaka kujiandaa kwa tafsiri tofauti.

Nape ambaye wakati huo alikuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, alisema kuwa wakati anatoa kauli hiyo, alimaanisha kwamba, kwenye ushindani wa kisiasa, ni kama mpira, hivyo kunaweza kutokea mazingira ya aliyefungwa kutoridhishwa na matokeo ya kufungwa, lakini kama refa hakuona kosa, unabakia kuwa ushindi.

Alisema katika siasa, unaposhindana na mtu, anaweza kusogeza kura na kushinda kama mazingira yanaridhisha na katika mataifa makubwa kama Marekani wanafanya hivyo, lakini kauli yake ilitafsiriwa vibaya na kuonekana CCM ilijipanga kushinda kwa goli la mkono (yaani ushindi usio wa haki).

**KUTISHIWA BASTOLA**

Nape pia alizungumzia sakata la kutishiwa kupigwa kwa bastola na anayedaiwa kuwa ni askari polisi, wakati akitaka kuzungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya uteuzi wake katika nafasi ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutenguliwa.

Alidai anamfahamu aliyemtishia kumpiga kwa bastola, waliomtuma na waliosuka mpango huo katika mkutano wake na waandishi wa habari uliokuwa ufanyike hotelini, lakini ukafanyika kando ya barabara Machi 23, 2017.

"Hatua kubwa niliyochukua baada ya kutishiwa kwa bastola niliamua kusamehe. Mimi nimelelewa na mcha Mungu na unapofanyiwa jambo la kuumiza sana moyo wako, njia sahihi ni kusamehe," Nape alisema.

Alisema aliwasamehe wote waliohusika na utaratibu mzima na alipokea ushauri wa wanasheria waliomtaka kufungua kesi kwa kuwa alikuwa na nafasi kubwa serikalini, ili kuwa funzo kwa wenye kufanya vitendo kama hivyo, lakini hakuona kama ingekuwa na matokeo mazuri.

Alisema hawezi kuwataja waliohusika, lakini si watu wa mtaani na hakuripoti tukio hilo kwa Jeshi la Polisi kwa kuwa aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni wakati huo, Suzan Kaganda, alikuwapo eneo la tukio.

"Niliamua kuwasamehe wote kwa sababu sikuona kama itakuwa na matokeo mazuri na sikuripoti polisi kwa sababu walikuwapo eneo la tukio, nikaona sasa hapa nitamshtaki nani kwa nani, kwa sababu RPC alikuwapo na polisi wengi waliovaa sare na waliovalia kiraia walilishuhudia tukio zima," Nape alisema.

Alisema haamini kama aliyemtishia kumpiga kwa bastola alikuwa na nia ya dhati ya kumpiga, bali alipaniki kulingana na mazingira ya tukio lile.

Nape alisema alibisha kutofanya mkutano kama alivyotakiwa na mtu huyo kwa sababu alikatazwa kwa amri na si kwa hoja ilhali anazifahamu haki zake na sheria za nchi.

"Walikuja kwa lengo la kunivurugia mkutano, nikasema sawa, tukatoka nje kwa ajili ya kufanya mkutano, lakini akaja kijana, hajavaa sare, akaniambia nisifanye mkutano niingine kwenye gari, sijamtambua ni nani, nikamwambia hapana, 'we(we) ni nani na kwanini unanizuia?' Nikaonekana nakaidi amri ambayo ni ujinga," Nape alisema.

Nape alisema asilimia 99 ya watu aliozungumza nao baada ya uteuzi wake kutenguliwa na Rais John Magufuli, walimshauri asifanye mkutano na waandishi wa habari.

Alisema alifanya uamuzi wa mwisho baada ya kupokea ushauri huo kwa kuwa lilikuwa ni jambo kubwa lililotaka kufungwa kwa mjadala wake ambao baadaye ungemuumiza zaidi.

"Lile jambo lilikuwa ni kubwa na lilikuwa limekamata mioyo ya watu, 'media' (vyombo vya habari) imekamata mioyo ya watu. Sasa usipofunga agenda, mjadala ungekuwa mkubwa na ungeniumiza mimi, ningelazimika kuanza kujieleza. Hivyo, nilifanya vile ili kuokoa taswira ya nchi yangu," alisema.

INAENDELEA UK 8



Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, akiwapungia wanachama na mashabiki wa chama hicho, wakati yeye na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko (wa pili kushoto), wakijiandaa kuingia kwenye gari la Magereza kurudi rumande, baada ya shauri kusikilizwa katika Mahakama ya Rufani Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Bwana harusi afariki dunia akitoka kuoa

**Na Beatrice Moses**

WATU watano wa familia moja, akiwamo bwana harusi, wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa wakati wakitoka kwenye harusi iliyofanyika Mlalo, Lushoto mkoani Tanga.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Dk. Aziz Msuya, aliliambia gazeti hili jana kuwa juzi alfajiri walipokea na kuihifadhi miili ya watu hao katika Hospitali ya Bagamoyo mkoani Pwani.

Dk. Msuya aliwataja waliokufa kuwa ni Elias Fidelis (40), Twaiba Mohamed (63), Hassan Mainde (33), Fatumati Singano (54) na Frank Mwangosi (53), waliokuwa kwenye gari aina ya Toyota Noah.

"Tulipokea miili tu majeruhi hawakuletwa hapa, ndugu tayari wamechukua miili hiyo na umebaki mwili mmoja tu hapa," alisema Dk. Msuya.

Mmoja wa ndugu wa marehemu ambaye hakuwa tayari kutajwa jina lake gazetini, alisema mwili wa bwana harusi Hassan Mainde, ulisafirishwa juzi na kuzikwa Handeni mkoani Tanga.

Mwili wa Twaiba ambaye anatajwa kuwa bibi wa bwana harusi na Fatumati imesafirishwa na kuzikwa katika maeneo tofauti wilayani Handeni.

"Hali ya bibi harusi si nzuri ingawa hakupata majeraha makubwa. Amezidiwa na uchungu wa kufiwa na mume," alisema ndugu huyo.

Taarifa kutoka kwa Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Barnabas Mwakalukwa, ilisema ajali hiyo ilitokea juzi saa nane usiku katika kijiji cha Makole kwenye Barabara ya Segera - Chalinze, mkoani Pwani.

Taarifa hiyo ilisema gari lenye namba T 367 CRY aina ya Toyota Noah, likiendeshwa na dereva ambaye jina lake bado halijafahamika, liligongana uso kwa uso na gari lenye namba T 135 ALG aina ya Toyota Hilux.

Gari hilo lilikuwa likitokea Dar es Salaam kwenda Mkata na lilikuwa likiendeshwa na Ramadhani Abdallah (23).

Ilisema hawajapata majina ya waliokufa, lakini waliwataja majeruhi kuwa ni Mwanaidi Awadh (50), Hamis Idd (17) wote wakazi wa Dar es Salaam na dereva Abdallah ambaye ni mkazi wa Handeni, Tanga.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, chanzo cha ajali ni dereva wa Noah aliyekuwa akiyapita magari mengine katika eneo ambalo haliruhusiwi ndipo gari lake likagongana uso kwa uso na Toyota Hilux.

Taarifa hiyo ilisema polisi wanamsaka dereva wa Noah ambaye alikimbia baada ya ajali hiyo.

"Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani linamtaka dereva aliyesababisha ajali hiyo ajisalimishe mara moja katika kituo chochote cha polisi, vinginevyo tutamsaka popote alipokimbilia na kuchukulia hatua kali za kisheria," alisema Mwakalukwa katika taarifa hiyo.

Pia iliwataka madereva wote kuendesha vyombo vyao vya moto kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani, ili kuepusha matukio mabaya ya ajali.

HABARI KITAIFA

# Fatma Karume amwagiwa sifa kila kona

**Na Enock Charles**

SIKU moja baada ya Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Fatma Karume, kutangaza rasmi kutowania tena uongozi katika chama hicho, wadau mbalimbali wa sheria na wanachama wamemwelezea kuwa mwanamke wa kwanza alionyesha uwezo mkubwa.

Bob Wangwe, mtoto wa mbunge wa zamani wa Tarime, Chacha Wangwe, alisema jana kuwa kwa kipindi kifupi alichoongoza TLS ameonyesha uwezo mkubwa tofauti na ilivyodhaniwa hapo kabla.

Wangwe ambaye ni mshirika mkubwa wa mwanasheria huyo machachari, alisema: "Fatma ni mtu ambaye ana uwezo na ameonyesha uwezo wake na uamuzi wake wa kutogombea umenisikitisha sana. Wengi tulipenda aendelee lakini sasa hatuna jinsi," alisema Bob.

Kuhusu kauli ya kiongozi huyo kuwa mahakama inachagua watu wa kufanya nao kazi na kutopendelea kufanya kazi na wanaharakati, alisema ni pigo kwa ustawi wa mahakama na ni jambo la kusikitisha.

"Kama ni kweli basi ni pigo kubwa sana kwa ustawi wa mahakama. Ikitokea kwamba mahakama inabagua wanaharakati basi ni jambo la kusikitisha sana, tunatarajia mahakama labda ikatae kufanya kazi na wezi na wahalifu wengine lakini si wanaharakati," alisema Bob.

Naye Wakili Jebra Kambole, ambaye ni mwanachama wa TLS, alisema Fatma alifanikiwa katika sera zake nyingi, hivyo kumfanya kuwa mmoja wa marais waliopata mafanikio katika kukiongoza chama hicho.

"Uongozi wake ulikuwa mzuri, alifanikiwa kuisemea TLS na wananchi mahali panapokuwa na mkwamo kiuhusiano, kuwasemea wafungwa na kuweka wazi msimamo wake juu ya wakuu wa mikoa na wilaya kuweka holela watu ndani," alisema.

Fatma Karume ambaye ni mtoto wa Rais wa zamani wa Zanzibar Amani Abeid Karume, alishinda kiti cha urais wa chama hicho cha wanasheria mwaka jana, akirithi mikoba ya Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, baada ya kuwabwaga Godwin Mwapongo, Godfrey Wasonga na Godwin Ngwilimi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki, akizungumza na wajumbe wa bodi na wafanyakazi wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwenyekiti wa TPSF, Salum Shamte. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Polepole awaita Chadema wakorofi

**Na Enock Charles**

SIKU chache baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kutoa maazimio ya kufanya mikutano ya hadhara nchi nzima, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, amedai hatua hiyo ni ukorofi na uvunjifu wa sheria.

Wiki iliyopita, Chadema kupitia kwa Katibu Mkuu wake, Dk. Vincent Mashinji, ilitangaza kuwa Kamati Kuu ya chama hicho imeamua waanze kufanya mikutano ya hadhara nchi nzima licha ya kuwapo kwa zuio la serikali kufanya mikutano hiyo na maandamano.

Dk. Mashinji alisema licha ya kuwapo kwa zuio hilo, CCM kimekuwa kikifanya mikutano ya hadhara maeneo mbalimbali nchini, akitolea mfano mikutano ya aina hiyo iliyofanyika hivi karibuni Karatu na Arumeru.

Akizungumza na Nipashe jana, Polepole alidai CCM haijawahi kufanya mikutano ya hadhara tangu kutolewa kwa zuio la mikutano hiyo.

Alisema kuwa kama Chadema wameamua kufanya mikutano ya hadhara, wasitafute kisingizio kwamba CCM inafanya mikutano ya aina hiyo. Alidai CCM inafanya mikutano ya ndani.

"Unajua mtu mkorofi ni mkorofi tu. Nimemsikia Katibu Mkuu wa Chadema (Dk. Mashinji) anasema sisi (CCM) tunafanya mikutano ya hadhara. Sisi tunafanya mikutano ya ndani, mimi nimekwenda Karatu, CCM tuna ofisi yenye uwanja mkubwa na kuna geti na maeneo mengine Arusha, Meru, Longido kote nimefanya mikutano ya ndani," Polepole alisema.

Juni 23, 2016, Rais John Magufuli alitangaza kupiga marufuku vyama kufanya mikutano ya siasa mpaka baada ya miaka mitano ili wananchi wahoji wanasiasa kama wametekeleza yale waliyoyaahidi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Alitoa kauli hiyo Ikulu Dar es Salaam baada ya kukabidhiwa ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Damian Lubuva.

"Niwaombe wanasiasa wenzangu, wafanye siasa za ushindani kwa nguvu zote baada ya miaka mitano ili wananchi watuhoji tuliyoyaahidi kama tumeyatekeleza au hatujayatekeleza.

"Kila nchi hata zile zilizobobea kwenye demokrasia, unapokwisha uchaguzi unakuwa ni wakati wa kazi. Haiwezekani mkawa kila siku ni siasa, watu watalima saa ngapi?

"Kila siku ni siasa, ni vyema tukatimiza wajibu wetu tuliopewa na wananchi na watatupima kwenye hilo.

"Ni matumaini yangu kuwa Watanzania tunaowaongoza wanataka maendeleo. Iwe kwa bahati nzuri au mbaya, serikali inayoongoza ni ya Chama Cha Mapinduzi.

"Yapo tuliyoyaahidi kuyatekeleza kwa wananchi katika kipindi cha miaka mitano, nisingependa kuona mtu yeyote ananichelewesha kutekeleza hayo niliyoahidi kwa kipindi cha miaka mitano," alisema.

Alisema ushindani ambao unatakiwa ufanywe kwa nguvu ni kwa wale wawakilishi waliopewa mamlaka na wananchi kupeleka hoja zao kwenye maeneo yao.

"Kama ni madiwani, wakapeleke hoja kwa nguvu zote kwenye maeneo yao, kama ni wabunge wakazungumze kwa nguvu sana bungeni, lakini hata kuziba midomo nayo ni demokrasia, hiyo ni demokrasia ya mwelekeo wa aina yake," Rais Magufuli alisema.

# TPSF yashtaki ma-RC, ma-DC kisa wawekezaji

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imetoa mapendekezo tisa kwa serikali likiwamo la kuitaka iwachukulie hatua baadhi ya wakuu wa mikoa, wilaya na watendaji wengine wanaowaweka ndani wawekezaji bila sababu za msingi.

Imesema vitendo kama hivyo vya kuwanyanyasa wawekezaji kumesababisha athari kwenye kuvutia uwekezaji mpya kuja nchini.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salam na Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Salum Shamte, wakati akiwasilisha mapendekezo hayo kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Uwekezaji, Angella Kairuki, ambaye alitembelea ofisi za TPSF.

Shamte alisema wamefurahishwa na uamuzi wa Rais John Magufuli kukemea vitendo hivyo vinavyofanywa na baadhi ya watendaji wake.

Alisema kumekuwa na unyanyasaji wa wawekezaji ambapo baadhi ya wakuu wa mikoa, wilaya na watendaji wa wizara na taasisi za umma wamekuwa wakiwanyanyasa wawekezaji na wakati mwingine kuwaweka ndani.

"Wamekuwa wakiwaweka ndani wawekezaji bila sababu za msingi, ni vizuri viongozi wa namna hii wachukuliwe hatua za utovu wa nidhamu kwa sababu athari kwenye kuvutia uwekezaji inakuwa mbaya," alisema.

Alitaja pendekezo lingine ni kuharakishwa kwa utekelezaji wa mwongozo wa marekebisho ya kanuni za udhibiti ili kuboresha mazingira ya biashara 'blueprint' ambayo waliifanyia kazi zaidi ya miaka mitatu na kuwasilishwa serikalini.

"Kinachotukwamisha kuhusu mazingira ya uwekezaji siyo kwamba hatufanyi maboresho, kasi yetu ya utekelezaji wa yale tuliyopanga na kukubaliana kuyaboresha ni ndogo," alisema.

Shamte aliyataja mapendekezo mengine ni kuongeza kasi ya ushiriki wa sekta binafsi katika miradi ya ubia

INAENDELEA UK 8


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 22/02/2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Mtwara** kuelekea **Mbeya,** magari hayo yana namba za usajili:

**T221BYM/T887DJB**
**T636DFA/T837DJB**
**T133CCP/T574BZB**
**T296CZS/T900BAZ**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 27.0
Upana - mita 5.50
Kimo - mita 6.40

3. Njia itakayotumika: **Mtwara hadi Mbeya** Kupitia **Makambako,**
Magari yatasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 06:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

2150659O2

# DPP aomba rufani ya Mbowe itupwe mbali

**Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa Mashtaka nchini (DPP), ambaye ni mlalamikaji katika rufani ya kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kusikiliza rufani namba 344 dhidi ya Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na mwenzake, ameomba itupiliwe mbali.

Mbali na Mbowe, mlalamikiwa mwingine katika kesi hiyo ni Mbunge wa Tarime Mjini (Chadema), Esther Matiko.

Kadhalika DPP ameomba rufani hiyo itupiliwe mbali kwa madai kwamba ni kinyume cha kifungu cha 362 kidogo cha (1) cha Mwenendo wa Sheria ya Makosa ya Jinai (CPA) sura ya 20 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Rufani hiyo ilisikilizwa jana mbele ya jopo la majaji watatu, likiongozwa na Mwenyekiti Stella Mgasha. Wengine ni Gerald Ndika na Mwanaisha Kwaliko.

Upande wa mlalamikaji uliongozwa na mawakili wa serikali wakuu Faraja Nchimbi, Paul Kadushi na Wakili wa Serikali Simon Wankyo.

Nchimbi alidai kuwa kwa mujibu wa kifungu hicho, rufani lazima iambatanishwe na mwenendo wa kesi na uamuzi mdogo unaobishaniwa Mahakama Kuu mbele ya Jaji Sam Rumanyika, aliyepangiwa kusikiliza rufani hiyo.

"Upande wa walalamikiwa ulifungua rufani hiyo bila kuambatanisha mwenendo wa kesi na uamuzi wa mahakama ya chini, hivyo tunaomba mahakama kutengua uamuzi wa Jaji Rumanyika kusikiliza rufani hiyo.

"Watukufu majaji, Mahakama Kuu iliyoketi chini ya Jaji Rumanyika ilipotoka kisheria kwa kuipanga na kuiita kwa ajili ya usikilizwaji rufani, huku akijua rufani hiyo iliwasilishwa kinyume cha kifungu cha 362 kidogo cha (1) cha CPA na kwamba hakutoa haki ya kutusikiliza walalamikiwa katika rufani hiyo," alidai Nchimbi.

Akijibu hoja za mlalamikaji, wakili wa walalamikiwa, Peter Kibatala, alidai madai ya kwamba hawakupewa muda wa kutosha wa kusikilizwa, si sahihi kwa kuwa rufani iliyoko Mahakama Kuu bado haijasikilizwa, kilichosikilizwa ni mapingamizi ya awali pekee.

Kibatala alidai kuwa rufani ya mlalamikaji haina mashiko kisheria, hivyo mahakama hiyo itupilie mbali.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, Jaji Mgasha kwa niaba ya jopo alisema mahakama inakwenda kupitia hoja hizo na kwamba itatoa uamuzi katika tarehe itakayopangwa.

Novemba 30, mwaka jana, Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Jaji Rumanyika, ilitupilia mbali pingamizi la awali la DPP dhidi ya rufani ya kupinga uamuzi wa kutengua dhamana ya Mbowe na Matiko.

Mbowe na Matiko wamefungua rufani ya kupinga uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu (kwa sasa Jaji wa Mahakama Kuu) Wilbard Mashauri kuwafutia dhamana kwa kukiuka masharti ya dhamana.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua madaftari ya wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Kassim Majaliwa, alipotembelea baadhi ya madarasa ya shule hiyo, iliyoko kwenye kambi ya wakimbizi ya Nduta wilayani Kibondo, Mkoa wa Kigoma jana. Wapili kushoto ni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (watatu kushoto) ni mkewe Mary Majaliwa. **PICHA: OWM**

# Onyo kwa atakayehujumu mkakati kufufua michikichi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali haitomvumilia mtu yeyote atakayebainika kuhujumu mkakati wake wa kulifufua zao la michikichi.

Amesema wanataka kuona wakulima wa zao hilo wakinufaika kama wengine wa mazao makuu ya biashara, hivyo haitomfumbia macho mtu atakayezembea.

Aliyasema hayo juzi baada ya kukagua shamba la michikichi la kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Bulombora mkoani Kigoma.

Alisema serikali inataka kuona wakulima wa zao hilo wakinufaika kama ilivyokuwa kwa wakulima wa korosho, chai, kahawa, pamba na tumbaku.

Alisema serikali imeamua kulifufua zao hilo kwa lengo la kumaliza tatizo la upatikanaji wa mafuta ya kula kwa kuwa inatumia fedha nyingi kuagiza nje ya nchi. Majaliwa aliwaagiza viongozi mkoani Kigoma kwamba suala la kilimo cha michikichi liwe ajenda ya kudumu kwenye vikao vyao.

Kadhalika, Waziri Mkuu, aliiagiza Wizara ya Kilimo ianzishe shamba darasa la zao la michikichi ili wananchi waweze kujifunza mbinu bora za kulima zao hilo.

Awali, Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kuboresha kilimo cha zao la michikichi.

Alisema kiasi hicho cha fedha kimetengwa kwa ajili hiyo katika bajeti ya wizara hiyo ya mwaka 2019/2020.

Alisema iwapo kilimo cha zao hilo kitaboreshwa, kitasaidia serikali kuokoa fedha nyingi za kigeni zilizokuwa zikitumika kuagiza mafuta kutoka nje.

Pia, Waziri Mgumba alisema wizara hiyo imeshaongeza watafiti zaidi ya 10 wa zao la michikichi katika kituo cha utafiti wa zao hilo cha Kihinga.

Mgumba alilipongeza Jeshi la Magereza na JKT kwa ushirikiano wanaoutoa kwa wizara katika kipindi hiki cha ufufuaji wa zao la michikichi.

Naye Waziri wa Ulinzi na Jeshi na JKT, Dk. Hussein Mwinyi, alimhakikishia Waziri Mkuu kuwa maelekezo yote aliyoyatoa kuhusu kilimo cha michikichi watayatekeleza.

# Mawaziri wajitosa mgogoro wa ardhi wananchi, JWTZ

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ambaye ni mwenyekiti wa kamati maalumu ya kushughulikia migogoro ya ardhi, amewataka wakazi wa Wilaya ya Ilemela mkoani Mwanza wenye migogoro ya ardhi na taasisi za jeshi na uwanja wa ndege kuwa watulivu, baada ya Rais John Magufuli kuagiza umalizwe.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kata ya Shibula wilayani humo, Lukuvi alisema Rais ameunda kamati hiyo kwa ajili ya kusikiliza mgogoro wa mitaa 11 na kupata ufumbuzi ambao utawezesha wananchi kulipwa fidia.

"Hapa Mwanza mgogoro ni mkubwa sana baina ya Uwanja wa Ndege, Jeshi la Wananchi (JWTZ) na wananchi ambao unahusisha mitaa 11, ndio maana sisi tumekuja hapa kuangalia maeneo yote ili kupata taarifa sahihi za taasisi hizo na wananchi ili tupeleka kwa Rais na kumshauri kutangaza kuwa wafuatao wataishi katika maeneo hayo milele," alisema Lukuvi.

Aidha, aliwataka wananchi wa maeneo husika walioambiwa wasiendeleze wabaki hivyo hivyo wasijenge, ingawa serikali imesitisha shughuli za kuwaondoa.

"Tumepata taarifa nzuri kutoka kwa pande zote mbili na nyaraka za taasisi na wananchi tumezipata, hivyo tutaenda kukaa na kutoa maamuzi yaliyo na tija kwa jamii, maeneo mengi tumepita migogoro mingi ni ya vijiji na hifadhi, lakini hili la Mwanza limekuwa tofauti," alisema Lukuvi.

Lukuvi alisema migogoro ya ardhi haitaisha katika wilaya za Ilemela na Nyamagana kutokana na kushindwa kupima ardhi, hali iliyosababisha wananchi kuvamia maeneo kutokana na uzembe wa halmashauri hizo.

Akisoma taarifa ya mitaa mitano ya Kata ya Shibula, Katibu wa Kamati ya kushughulikia migogoro Robert Luzili, alisema uwanja huo wa ndege ulihamishwa kutoka Sabasaba mwaka 1952 hadi 1958, ukajengwa eneo la Kisaka Kata ya Ilemela na wananchi kufidiwa kwa kulipwa na serikali katika vitongoji vya Kisaka, Bukungu na Buduku.

"Sisi hatuna pingamizi lolote juu ya kuhamishwa endapo serikali itatulipa fidia na kutuonyesha maeneo halali ya kujenga, maana mpaka sasa tunamaisha ya shida, tumeshindwa hata kuendele kimaisha nyumba taturuhusiwi kujenga wala kulima tunamwomba Rais atatulie tatizo hilo," alisema Luzili.

Katika ziara hiyo ya mawaziri nane ambao walifuatana na Lukuvi ni Luhaga Mpina (Mifugo na Uvuvi); Hussen Mwinyi (Ulinzi na JKT); Prof. Makame Mbarawa (Maji na Umwagiliaji); Hamisi Kigwangalla (Maliasili na Utalii); Selemani Jafo (Tamisemi); manaibu mawaziri Omary Mugumba (Kilimo) na Mussa Sima (Mazingira).

HABARI KITAIFA

# Blockbonds, Benki I & M wazindua huduma

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kuwezesha Watanzania wengi kumiliki akaunti binafsi na akaunti za biashara, Kampuni ya Blockbonds kwa kushirikiana na Benki I & M imezindua huduma ya Spenn inayomwezesha mtumiaji kutuma na kupokea fedha bila makato yoyote.

Huduma hiyo inayopatikana kwa kuwa na simu janja maarufu smartphone, itamwezesha mtumiaji kujisajili kwa kutumia kitambulisho cha taifa kabla ya kuanza kupata huduma kwa usalama na uhakika.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Blockbonds na Spenn, Jens Glaso, aliyaeleza hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika hafla ya uzinduzi wa huduma hiyo jijini Dar es Salaam jana.

Alisema lengo ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata fursa ya huduma za kifedha kupitia teknolojia yenye ubunifu wa hali ya juu.

"Huduma imeanza kupatikana Tanzania na nchi za Afrika, mwaka jana tuliweza kuizindua nchini Rwanda na tayari kuna watumiaji zaidi ya 130,000 ambao wameshajiunga," alisema Glaso.

Alisema mtu yoyote anaweza kufungua akaunti ambayo haina gharama za uendeshaji na kutuma na kupokea fedha, kufanya malipo katika maduka mbalimbali pamoja na kuweka na kutoa fedha katika tawi lolote la benki I&M.

Alieleza zaidi kuwa, huduma hiyo pia ina fursa ya kufanya biashara ya kuuza bidhaa na huduma kwa ufanisi kwa kumpa mtumiaji njia rahisi ya kupokea malipo bila kutumia fedha taslimu endapo atajisajili kuwa mtumiaji.

"Ni rahisi sana mtu yoyote anayemiliki simu aina ya smartphone, anaweza kujisajili na Spenn kwa urahisi, na ili kujisajili unapaswa kuwa na namba ya simu, jina kamili pamoja na kitambulisho cha taifa," alisema Glaso.

Pia, alisema lengo ni kuwafikia mamilioni ya Watanzania ambao hawana akaunti kwa ajili ya kujiwekea akiba kwa njia rahisi na isiyo na gharama.



Mkazi wa jiji akiandaa miguu ya ng'ombe kwa ajili ya kuwauzia wafanyabiashara wa supu ya kongoro, katika eneo la machinjioni Vingunguti, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanufaika wa Tasaf kwenda kutoa elimu DRC

**Na Elizabeth Zaya**

MAOFISA wanaoshughulikia mfuko wa huduma za jamii kutoka katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo(DRC), wamesema wanajipanga kuwatumia wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) kwenda kutoa elimu katika nchi yao, namna wanavyotumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kujiongezea kipato.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa mfuko huo wa DRC, Ruphin Bo Elongo, katika ziara ya maofisa zaidi ya 10 waliyoifanya nchini kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kujifunza namna Tanzania kupitia Tasaf ilivyofanikiwa kupunguza umaskini.

Akizungumza baada ya kuhitimisha ziara hiyo Tanzania Bara kwa kutembelea walengwa wa mpango wa uhawilishaji fedha katika Wilaya ya Temeke, Elongo, alisema wameona itasaidia kwa kiwango kikubwa endapo watachukua baadhi ya walengwa wa Tanzania kwenda nchini DRC kwa ajili ya kwenda kutoa mafunzo

INAENDELEA UK. 8

# Maandamano wachimbaji kumfagilia JPM yashika kasi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WACHIMBAJI wadogo wa madini wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, wamempongeza Rais John Magufuli kwa hatua aliyoichukua ya kukutana na wadau wa sekta ya madini na kusikiliza kero zao pamoja na kutoa uamuzi wa kuboreshewa shughuli zao.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wadogo wilayani Tunduru (RUVREMA), Christopher Simkoko, wakati akisoma risala ya wachimbaji wadogo ya kumpongeza Rais Magufuli kwa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Juma Homera, baada ya kupokea maandamano yao ya amani.

Simkoko alisema wachimbaji wadogo wa madini wameamua kwa dhati kumpongeza Rais Magufuli kwa kukubali kusikiliza kero za sekta ya madini na kupeleka muswada wa dharura bungeni kwa lengo la marekebisho ya sheria ya madini, jambo ambalo limeleta faraja kubwa kwa wachimbaji wadogo nchini.

Alisema kutokana na hali hiyo, wachimbaji wadogo Wilaya ya Tunduru kwa hiari yao baada ya kuona Rais Magufuli amewafanyia mambo mazuri, waliamua kufanya maandamano ya amani ya kumpongeza pamoja na serikali yake kwa kusikiliza matatizo mbalimbali ya wachimbaji wadogo wa madini. Aliiomba serikali ione umuhimu wa kuwatafutia masoko ya uhakika ya madini ambayo yamekuwa yakiuzwa katika mazingira hatarishi pamoja na kulipwa bei ndogo, hivyo rasilimali hiyo kututoa mchango katika uchumi wa taifa.

Kwa mujibu wa Homera, azima ya Rais Magufuli ni kuhakikisha wachimbaji wadogo wanafanya kazi kwa uhakika na sekta ya madini inachangia katika uchumi.

Alifafanua kuwa serikali imeweka mikakati kadhaa, ikiwamo kuwa na minada ya madini ambayo itasababisha kuwapo soko la uhakika ambalo litabadilisha maisha ya wachimbaji wadogo.

Hata hivyo, aliwaonya wachimbaji wadogo kutochimba madini kwenye eneo la pori la akiba la Selous ambako inadaiwa kuna wachimbaji wamekuwa wakivamia kuchimba, na kwamba wachimbaji wote wa madini waone umuhimu wa kuwa na vitambulisho vya ujasiriamali ili wafanye kazi zao bila usumbufu.

Maandamano ya wachimbaji hao ni mwendelezo wa maandamano ya wachimbaji wadogo katika maeneo kadhaa nchini yaliyoanza wiki iliyopita kwa lengo la kumpongeza Rais Magufuli.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wananchi sasa wachukue tahadhari dhidi ya mauaji

**WIMBI** la matukio ya mauaji katika siku za karibuni katika maeneo kadhaa ya nchi yetu, yametufumbua kikubwa ni kwa wananchi kuchukua hatua za kushirikiana kuweka na kuimarisha usalama katika maeneo waliyopo.

Matukio ya mauaji yenye utata yanayofanywa na watu wasiojulikana yamesharipotiwa yamefanyika katika maeneo kadhaa kwenye mikoa ya Njombe, Simiyu na Arusha.

Vyombo vya dola kwa upande wake vimeshachukua hatua mbalimbali zikiwamo kuwatia mbaroni na kuwafikisha katika vyombo vya sheria baadhi ya watuhumiwa mkoani Njombe.

Kwa upande wa mkoani Simiyu, hatua za kuwasaka wahalifu hao zilikuwa zinaendelea na Mkuu wa Mkoa huo, Anthony Mtaka, wiki iliyopita aliitisha mkutano wilayani Busega kujadili changamoto za usalama, ambao aliutumia kuwataka wananchi kupiga kura za siri kwa lengo la kuwataja majina wote wanaowahisi kuhusika.

Uamuzi wa kupiga kura hizo ulitokana na maazimio ya wananchi hao katika kikao chao na Mtaka, baada ya baadhi yao katika Kata ya Ramadi kusema kuwa hawana imani na Jeshi la Polisi kutokana na kuwakamata wanaodhaniwa kuwa watuhumiwa kisha kuwaachia, na kuwaacha watuhumiwa halisi wa matukio kadhaa ya mauaji ya watoto.

Wakati hatua hizo zikichukuliwa Simiyu, mwishoni mwa wiki zimepatikana habari nyingine za kutisha zenye sura ya ukatili uliopitiliza ambazo zinadai kuwapo kwa matukio ya ubakaji na mauaji ya wanawake katika eneo la Mto wa Mbu wilayani Monduli, mkoani Arusha.

Wakazi wa Mto wa Mbu inadaiwa kuwa wameingiwa na hofu kubwa kutokana na matukio hayo ya ukatili wa kutisha, ambapo Jumapili waliwasilisha kilio chao kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alipofanya nao kikao cha kusikiliza malalamiko hayo.

Baada ya kuelezwa hali halisi, Waziri Lugola alitoa wiki moja kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha linafanya uchunguzi wa kina kwa kuwakamata watuhumiwa waliofanya matukio hayo ya kikatili.

Waziri Lugola alimuagiza Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, kushirikiana na Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo, na kusimamiwa na Mkuu wa Wilaya hiyo kuhakikisha uchunguzi wa kiitelijensia unafanyika juu ya watu wanaohusika kufanya vitendo hivyo vya kikatili katika eneo hilo.

Lugola aliongeza kuwa, haiwezekani wananchi wa eneo hilo wawe wanaishi kwa wasiwasi, wanateswa, kuuawa na kudhalilishwa wakati Serikali ipo, Polisi wapo, na wananchi wapo, kwa hatua hiyo lazima mauaji hayo yafikie kikomo.

Sababu ya kuibuka wimbi la vitendo vya mauaji ya watoto na wanawake pamoja na ukatili wa ubakaji wanawake katika maeneo yote ya mikoa ya mitatu hadi sasa hazijulikani.

Hata hivyo, matukio haya ni utamaduni mpya katika nchi yetu kwa kuwa katika historia hayajawahi kutokea, hivyo ni wakati mwafaka wa jamii yetu kujitafakari kuhusu ni mambo yapi yafanyike ili kukabiliana nayo.

Tunaona kwamba upo umuhimu wa kubadili mwenendo wa maisha kwa wananchi kuwa na tahadhari ya kiusalama katika maeneo yao ili iwe rahisi kuwabaini watu ambao wana shaka nao.

Kwa mfano, miaka ya nyuma utaratibu wa mabalozi wa nyumba 10 ulisaidia kuwatambua wageni wote waliokuwa wanaingia katika nyumba 10 iwe mijini au vijijini. Ni jambo ambalo kuna haja ya kulirejesha na kuliwekea utaratibu mzuri.

Vilevile, wananchi wajenge utamaduni wa kutoa taarifa katika vyombo vya ulinzi na usalama pale wanapoona kuna watu wanawatilia shaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

BUSARA

**MSAMIATI USIOUJUA UTATUMIAJE**
**KILA LUGHA INA MANENO YAKE AU MSAMIATI WA KUTUMIA. KAMA MANENO YA KIMASAI HUYAJUI KAMWE HUWEZI KUYATUMIA. KATIKA MAENDELEO HALI NI HIYO HIYO. MIKAKATI MIPYA YA MAENDELEO USIIPARAMIE BILA KUJIFUNZA KWANZA.**
**NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Salome Kitomari

## Kampuni za bima zitembelee wakulima kwa ustawi wao

**YUMKINI** kuna mambo mengi ya msingi ambayo yanatakiwa kuwafikia wakulima kwa minajili ya kuongeza tija ya kilimo chao na ustawi kwa ujumla.

Lakini ambalo ni kama limesahaulika ni la kuwapatia bima ambayo itawawezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotokana na shughuli yao hiyo ya kiuchumi.

Kazi ya kilimo inakabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi inayoendana na ukame wa muda mrefu, mabadiliko ya msimu wa mvua, mafuriko na kimbunga. Lakini yapo majanga yanayosababishwa na binadamu kama ya ng'ombe kula mazao, majanga ya moto na mengine.

Katika hali kama hii ndipo umuhimu wa bima unapojitokeza kwa ajili ya fidia kwa mkulima pale hasara inapojitokeza. NI kwa maana hiyo Muungwana anakubaliana na hatua ya Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA).

TIRA imekuja na utaratibu wa kuwaelimisha wakulima juu ya umuhimu wa kuwa na bima za kilimo zitakazowasaidia wakulima kupunguza hasara wanayoweza kuipata kutokana na visababishi nilivyovitaja hapo juu.

Visababishi hivyo huchangia wakulima wengi kupata hasara ambayo sasa inaweza kufidiwa na bima.

Mfumo wa bima ni wa kujazilishia wanaokutwa na majanga yanayohitaji kulipwa na bima.

Ni utaratibu ambao unatumika sana nchini kwani kuna bima za afya, magari, nyumba na sasa bima za wakulima.

Hata mifuko ya hifadhi ya jamii inajiendesha kwa mfumo wa bima kwa maana wapo wanaostaafu na kupata stahiki zao, huku wengine wakiwa hawaufikii umri huo wa kustaafu.

Aidha, wapo wanaonufaika na mafao mbalimbali kama fao la uzazi, ulemavu, ukosefu wa ajira, yote hayo yakiwa yanatolewa kwa mwanachama aliyepatwa na majanga.

Inapotokea kwamba kwa kipindi chote cha maisha hadi kustaafu mhusika hajapata tatizo, maana yake hawezi kunufaika na mfumo huo, na kupata mafao yake ya mkupuo na mafao ya kila mwezi.

Lakini wapo ambao hufariki siku chache kabla ya kustaafu na wengine wanapostaafu hufariki miaka michache kabla ya kulipwa mafao yao ya kila mwezi, hata kwa zaidi ya miezi sita.

Hapo ndipo utakapoona kwamba bima inafanyaje kazi, kwa kuwa wapo wanaofanya kujazilia wengine, huku wengine wakifanya na kunufaika na kile kinachowekezwa.

Vivyo hivyo kwa bima ya afya wapo ambao wanapata huduma za afya kwa kipindi chote na wakati mwingine matibabu yao yakiwa yenye gharama kubwa, lakini wapo ambao huishi bila kuugua kwa kipindi kirefu na hivyo kutotumia sehemu yoyote ya fedha waliyochangia kwenye mfuko wa bima.

Ndivyo itakavyokuwa kwa bima ya wakulima, itakayokuwa ikilipa fidia kwa waliopata majanga.

Kwa ujumla bima ni muhimu kwa wakulima ili kuwapunguzia machungu ya changamoto zinazotokana na majanga mbalimbali ya maisha.

Iwapo wakulima watakuwa na bima, maana yake wataweza kuendelea na shughuli zao za kila siku kwa uhakika zaidi kwani lolote likitokea bima itafidia.

Hiyo ni tofauti na sasa ambako wakulima wengi wamejikuta kwenye majanga makubwa ya kupoteza mali zao kukiwa hakuna kifuta machozi cha aina yoyote. Kwamba wangekuwa na bima, maana yake wangeweza kupata fidia dhidi ya majanga wanayokumbana nayo.

Ni vyema kampuni za bima zikawatembelea wakulima maeneo mbalimbali nchini na kuwaelimisha faida zilizopo za kujiunga na bima, nini kifanyike kuhakikisha kuwa wanajiunga na kunufaika na mfumo huo kwa manufaa yao wenyewe.

Iwapo wakulima watakuwa na uhakika wa bima maana yake wataweza kuendelea na kilimo kwa uhakika.

Hiyo ni kwa sababu wana uhakika wa shughuli zao za kila siku, kwamba hata pale wanapokumbana na majanga yanayogharimu kilimo chao, ipo fidia watapata.

Ni kweli siyo kila wakati watapata hasara lakini kama nilivyoeleza hapo juu kuna ambao moja kwa moja watanufaika na wengine watakuwa wamewafidia wengine katika utaratibu huo.

# MJADALA

## Serikali itatue kero hii

**Mhariri**

*NINAJITOKEZA katika ukurasa wako wa maoni ili niweze kueleza kero ya muda mrefu inayotupata sisi wakazi wa Maramba Mawili, Wilaya mpya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam.*

*Kero ninayoieleza kwa leo ni ya ukosefu wa huduma ya uhakika ya maji ya bomba katika eneo letu, tofauti na ilivyo katika maeneo mengine ya jiji hili.*

*Kwa muda mrefu tumeahidiwa na serikali yetu kupatiwa huduma hiyo ya maji ya bomba ambayo kimsingi, ndiyo huduma ya uhakika zaidi, ikilinganishwa na vyanzo vingine kama ya maji ya visima.*

*Kulikuwa na mradi wa kutandaza mabomba ya maji uliolikuwa ukijengwa na Wachina karibu miaka 10 iliyopita, lakini pamoja na kulazwa kwa mabomba hayo, lakini hadi leo bado maji hakuna.*

*Ninaomba kupitia kwako Mhariri kwa serikali na hasa walio na mamlaka katika sekta ya maji, wasikie kilio chetu cha muda mrefu, na hatimaye watuletee huduma hii muhimu kwa maisha ya binadamu.*

*Kupatikana kwa huduma hii kutatupunguzia kero tunayoipata ya kupoteza muda na raslimali tukitafuta maji na hivyo kuathiri shughuli zetu za kujitafutia maendeleo.*

**Muathirika, Maramba Mawili-Dar**

## Taaluma hii itendewe haki

**Mhariri,**

*NIPATIE fursa ya kuzungumzia kidogo ninachoona ni tatizo kwa baadhi ya watangazaji wa redio, pale wanapokuwa wanajadili ama kuongoza mada iliyoko mezani katika baadhi ya vituo vya televisheni na redio.*

*Kilichonivuta niweke hili suala kwako, ni baada ya kumsikia mtangazaji mmoja aliyekuwa akisoma taarifa mbalimbali zilizoandikwa magazetini, akishangaa kwa nini mikopo kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu inayotolewa na bodi wanapewa pia wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo vya elimu ya juu, vinavyomilikiwa na watu binafsi.*

*Nilivyomuelewa mimi, mtangazaji huyo alikuwa anamaanisha kwa ufahamu wake kuwa, mikopo kwa ajili ya kusoma vyuo vya elimu ya juu nchini, ni maalumu kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya umma tu.*

*Nimeamua kusema hili baada ya kung'amua kuwa, baadhi ya watangazaji wetu kwenye baadhi ya redio na televisheni nchini wanakuwa hawana ufahamu wa kutosha wakati mwingine kuhusiana na wanachochangia kwenye baadhi ya mada wanazoziendesha.*

*Ninaomba kupitia kwako mhariri, kwa baadhi ya vituo vya redio na televisheni zikaona umuhimu wa kuweka watu wenye ufahamu wa kutosha kwenye mada zinazowasilishwa mezani, ama wanapochangia kwenye habari na makala zilizoandikwa magazetini.*

**Mpenda ukweli, Dar es Salaam**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz




# Tuzingatie marufuku zinazotolewa na serikali kuepusha vifo, majanga

**Na Sabato Kasika**

**NENO** marufuku linatafsiriwa kwa namna mbalimbali, ambazo wataalam wa Kiswahili wamekuwa wakizitaja, lakini zote zikiwa na maana moja, kwamba ni kukataza au kuzuia jambo lisifanyike ama lisitendeke.

Kwa mfano, mtu anaweza kupiga marufuku kitu fulani kisifanyike nyumbani kwake au katika kampuni yake na pia serikali inaweza kupiga marufuku mambo, ambayo inaona yanaweza kuleta hatari kwa wananchi wake.

Ninataja neno hili marufuku, kutokana na jinsi, ambavyo jamii imekuwa ikifanya uzembe kwenye baadhi ya mambo ya hatari, ambayo serikali imezuia yasifanyike, lakini kwasababu ambazo jamii inajua yenyewe, imekuwa ikiyafanya.

Mojawapo ya marufuku ya serikali ni ile ya daladala kutojaza mafuta kwenye vituo vya mafuta, zikiwa na abiria, lakini cha kushangaza baadhi ya madereva hawazingatii hilo na wanaendelea kukiuka marufuku hiyo kana kwamba hakuna maelekezo yaliyotolewa.

Madereva wa daladala wamekuwa wakifika katika vituo vya mafuta wakiwa na abiria, wakati mwingine wamejaza kupita kiasi, hali ambayo likitokea tatizo wanaweza kushindwa kujiokoa.

Hivi kweli ikitokea ajali watakuwa na la kujitetea? Kwanini wanakuwa wagumu kuheshimu maelekezo wanayopewa kwa ajili ya usalama wao na abiria?

Mtindo huu wa kutoheshimu maelekezo upo pia kwa madereva wa bodaboda, ambao wanatakiwa wasibebe abiria zaidi ya mmoja na tena wavae kofia, lakini baadhi yao hawafanyi hivyo.

Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani lilishapiga marufuku madereva bodaboda kupakia watoto wenye umri chini ya miaka tisa, lakini bado wanaendelea kuwapakia kana kwamba hawajazuiwa!

Hawa watu wanataka aje nani awaambie ndipo watekeleze, na ni kwanini watii sheria kwa kushurutishwa? Kwa mtindo huu ni bora kuwafuatilia ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Bila kufuatiliwa na kuchukuliwa hatua za kisheria, wanaweza kusababisha madhara makubwa kwa watu wasio na hatia, kwasababu tu ya uzembe wao, ambao kimsingi wanatakiwa kuachana nao.

Kutii sheria bila shurti ni jambo la msingi na linamjengea mtu heshima na uaminifu kuliko kufanya mambo kienyeji kama kwamba hakuna sheria zinazowaongoza.

Katika mwendelezo huo wa kutozingatia maelekezo, unagusa pia upande huu wa unywaji wa pombe za viroba, ambayo ilikuwa inauzwa kwa bei nafuu na kusababisha watu wengi na hasa madereva wa bodaboda kuinunua kirahisi.

Serikali ilipiga marufuku ufungaji wa pombe katika viroba, lakini sasa wanywaji wamebuni mbinu nyingine, ambazo zinawafanya waendelee kunywa pombe hiyo kwa bei nafuu kama zamani.

Kwa sasa wauzaji hununua chupa kubwa ya konyagi na kuuza katika vipimo vidogo tofauti ili kila mteja aweze kupata kulingana na pesa yake, hali ambayo inasababisha vijana kuichangamkia kama kawaida.

Mtindo huo umesababisha vijana kuendelea kulewa kama zamani, kwasababu pombe hiyo inapatikana kwa bei rahisi na hivyo kuwafanya walevi kuendelea kulewa wakati wote na hasa madereva wa bodaboda, ambao walikuwa wakituhumiwa kusababisha ajali kwa ulevi.

Yapo mambo mengi, ambayo serikali imepiga marufuku, kwa ajili ya usalama wa raia wake, lakini nimetaja hayo machache ili kuonyesha ni jinsi gani jamii inashindwa kubadilika na kuzingatia maelekezo.

Hatua ya serikali kupiga marufuku jambo fulani kwa ajili ya usalama wa wananchi wake ni elimu tosha, ambayo wangeizingatia ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi.

Kwa ujumla, kutii sheria bila shuruti ni jambo la msingi ingawa baadhi ya vijana wanaona kama ni kazi ngumu, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba wahusika wazingatie marufuku hizo.

Inawezekana kukiuka marufuku huku kunakofanywa na baadhi ya wananchi kunatokana na kukosa elimu sahihi juu ya matumizi ya vyombo hivyo, lakini sidhani kwamba hakuna elimu ambayo madereva wa daladala na bodaboda walioipata.

Tumeshuhudia ajali nyingi za bodaboda zinazosababisha watu kupoteza maisha huku wengine wakipata ulemavu wa kudumu, hali iliyosababisha serikali na baadhi ya taasisi za kijamii kutoa elimu.

Lakini hadi sasa bado unakuta kuna madereva wa bodaboda wanaobeba abiria zaidi ya mmoja, hawavai kofia na wanabeba watoto wa chini ya miaka tisa.

Pia wenzao wa daladala vilevile ni kawaida yao kujaza mafuta kwenye vituo vya mafuta wakiwa na abiria.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Walimu watano shule iliyoshika mkia kidato cha nne wajifukuza

**Na Beatrice Shayo**

WALIMU watano wa Shule ya Sekondari Masjid Qubah Muslim Seminary ya jijini Dar es Salaam, ambayo imeshika mkia katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne mwaka jana, wametimka kabla ya kufukuzwa.

Katika matokeo ya mtihani huo yaliyotangazwa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (Necta), Dk. Charles Msonde, shule hiyo iliyoko Kijitonyama ilikamilisha orodha za shule 10 zilizofanywa vibaya zaidi kitaifa.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Abubakar Musa, aliliambia Nipashe jana kuwa, walimu watano wameamua kujiondoa kabla ya kufukuzwa.

"Mabadiliko yameanza kufanyika shuleni maana kuna walimu watano wamejiondoa wenyewe, waliobakia ni wachache," Musa ambaye mwezi uliopita aliiambia Nipashe kuwa atafukuza walimu wote walioko shuleni kwake na kuajiri wapya kutokana na matokeo mabaya waliyoyapata.

Mkurugenzi huyo aliongeza: "Wamejiondoa kwa sababu wamesikia taarifa niliyosema nitawafukuza, naona wameona kuliko kusubiria kufukuzwa, bora wajiondoe, yaani wamejiongeza."

Musa alisema walimu waliobaki shuleni huko huenda wakawa wana sababu lakini akasisitiza kuwa atakwenda kuwasikiliza na kujua nini cha kufanya.

Alisema alikuwa ana ziara ya mwezi mmoja mikoani na kwamba juma hili atarejea Dar es Salaam kulishughulikia suala hilo.

Mwezi uliopita, Musa alisema kuwa baada ya kuchukua uongozi wa shule hiyo mwishoni mwa mwaka jana, hatua ya kwanza waliyofanya Desemba ni kumwondoa mkuu wa shule.

Kutokana na matokeo mabaya yaliyotangazwa, Musa alisema wameamua kuwaondoa walimu wote 12 waliokuwa wakifundisha shuleni hapo.

"Tulianza kuisafisha shule kwa kumwondoa mkuu wa shule kwa sababu hali haikuwa nzuri na matokeo ndiyo kama yanavyoonekana watoto wamefeli wote. Walimu hawa 12 tuliwaambia tutawapima kutokana na ufaulu wa wanafunzi lakini kwa matokeo haya wote tunawafukuza," alisema.

"Hatuwezi kuendelea na walimu hawa, kama ulivyoona matokeo, kwa kweli siyo mazuri yamechafua shule. Tutaajiri walimu wapya, tunataka kurudisha sifa ya shule kwa sababu hata ukiangalia matokeo ya nyuma shule haijawahi kushika mkia kama hivi.

# Nape ajutia bao la mkono

INATOKA UK 2

Alisema kuwa anaamini kuwa, kama mkutano wake na waandishi wa habari ungefanyika salama, ungesaidia kuokoa taswira ya nchi, serikali ingebaki na chama kingebaki salama.

"Nilikuwa nimeandika ninachotaka kusema na 'nikashare' (nikasambaza) na baadhi ya viongozi wa dola waone kama kuna tatizo na wakasema hawaoni tatizo. Nikaruhusiwa niende na nikaenda, nikakuta vyombo vya dola vimetanda," Nape alisema.

Aliendelea kueleza kuwa, watu waliofika kwenye mkutano huo, ni wengi, akibainisha kuwa mbali na waandishi wa habari tu, dada zake ambao hawakuwa na taarifa zake, pia walihudhuria.

Nape (pichani) alidai kuwa, wakati ananyooshewa silaha, naye alikuwa nayo na mlinzi wake pia alikuwa nayo, hivyo kama wangeamua kuzitumia, amani ingetoweka.

**BUNGE LIVE**

Katika mahojiano hayo, Nape pia alisema Bunge kutorushwa moja kwa moja lilikuta katika uongozi wake wizarani, lakini anacholaumiwa hadi sasa ni kuzuia Bunge kutorushwa moja kwa moja kupitia Televisheni ya Taifa (TBC) kwa gharama zake ambazo zilikuwa Sh. bilioni nne kwa mwaka.

Nape alisema kuwa wakati huo, TBC ilikuwa ikitumia fedha nyingi ilhali Bunge lilikuwa limeshaanza kuandaa chombo chake cha kurusha



matangazo moja kwa moja, hivyo alilitaka Bunge kukiendeleza kituo chake ili kifanye kazi hiyo.

"Wapi tulikosea? Tulitakiwa tujadili Kanuni za Bunge ziweje, tukajisahau, tukaanza makelele Nape Nape badala ya kushikilia wadau wa kutunga kanuni hizo na suala ni nani anarusha 'live' (moja kwa moja) au anatakiwa kufanya hivyo, waliotunga kanuni, ndiyo walipaswa kufahamu na kutekeleza hilo," Nape alisema.

Mbunge huyo alisema wananchi wanahisia kuwa serikali haikuwatendea haki na ushiriki wa wananchi kwenye Bunge umeshuka kwa sababu hawana fursa ya kufuatilia.

Alisema mjadala wa umma ni kuhoji kwanini vyombo vya habari vimezuiwa kuweka matangazo kwenye matangazo ya moja kwa moja ya Bunge wakati wanarusha kwa gharama zao binafsi.

**NAPE NA SIASA**

Alisema anaamini kitu chake na kukisimamia na ili kuamini kitu kingine, ashawishiwe kwa hoja, lakini hali hiyo imekuwa ikimfanya aonekane ni mpinzani.

Nape alisema amejifunza siasa kwa Rais mstaafu Benjamin Mkapa kuwa, mwanasiasa wa kweli ni yule anayeweza kujenga hoja yake na kubomoa hoja ya mwenzake na si vinginevyo.

Alisema hatamani kuona kukiwa na uadui kwenye siasa, badala yake kuwa kitu kimoja kwenye shughuli za kijamii na kushindana kwa hoja katika mambo ya msingi.

"Naamini uzalendo ni kuipenda nchi na mazuri yake, na kubishana kwa hoja ya kuboresha maendeleo ya nchi badala ya kuandamana mlengo fulani, kuonekana anapinga," Nape alisema na kuongeza kuwa anatamani mbwembwe na vijembe vya kishkaji kwenye kampeni zilizokuwako miaka ya nyuma.

Nape pia alisema si sahihi kumlinganisha kiongozi aliye madarakani na aliyepita, akiwataka watu kuacha kutoa kauli kwamba 'viatu vya Nape havimtoshi Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole'.

# Waziri aipa maagizo manane Tume Madini

INATOKA UK 2

6.41, uchimbaji wa kati (ML) Sh. bilioni 28.28 na uchimbaji mdogo (PML) Sh. bilioni 19.51.

**LESENI KUFUTWA**

Waziri Biteko alisema leseni za utafiti 110 na leseni za uchimbaji wa kati 52 zilikuwa zimeshapewa hati ya makosa zifutwe ndani ya siku saba.

"Na ziandikiwe hati ya madai mara moja na wakishindwa kulipa madeni hayo ndani ya siku 30 wachukuliwe hatua kwa mujibu wa kifungu cha 93 cha Sheria ya Madini," alisema.

Pamoja na hayo, Biteko aliagiza tume hiyo kufuta leseni zote za utafiti ambazo zipo hai na hazina madeni, lakini toka zitolewe imepita miezi mitatu bila kuanza kuandaa na kukusanya vifaa stahiki kwa ajili ya utafiti.

"Pia miezi zaidi ya sita imepita bila kuanza utafiti kwa kuwa ni kinyume cha kifungu cha 36(1) cha sheria," alisema.

**WATENDAJI WATUMBULIWA**

Kadhalika, aliagiza kusimamishwa kazi watumishi watano wa wizara hiyo kwa makosa mbalimbali ikiwamo kutoa leseni za uchimbaji mdogo kwa raia wa kigeni na kubadilisha leseni za maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kuwapatia wakubwa.

"Kuna baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo likiwamo la Melela lipo Mvomero Morogoro, yametolewa leseni bila kufuata taratibu za utoaji leseni," alisema.

Aliwataja wanaosimamishwa kwa kosa hilo ni Hamis Komba, Lucy Kimaro na Bakari Shemsanga.

"Haiwezekani tutenge maeneo kwa wachimbaji wadogo wao wakafanye wanavyojisikia wao kwa tamaa zao," alisema.

Pia alisema kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Madini kinakataza leseni ndogo za uchimbaji kutolewa kwa wageni.

"Leseni namba PML003227NZ, PML003387NZ, PML003427NZ zimetolewa kwa mtu ambaye ni raia wa Kenya, lakini pia maombi yake namba PML12823/NZ, PML13036/NZ, PML13066/NZ, PML14632/NZ, PML23158/NZ, PML23159/NZ, PML25398/NZ, PML25786/NZ na PML25789NZ yapo katika hatua mbalimbali ya kupatiwa leseni kinyume cha sheria," alisema.

Aliagiza tume hiyo kuwachukulia hatua walioshiriki kutoa leseni hizo ambao ni Fredrick Massawe na Elias Azaria.

**WACHIMBAJI WADOGO WADAIWA BIL.1.7/-**

Biteko alisema kuna wachimbaji hasa wadogo wamejenga mitambo ya kuchenjua dhahabu bila kufuata utaratibu, ambapo hadi kufikia mwezi huu takribani mitambo 639 haina leseni na imesababisha hasara ya Sh. bilioni 1.76.

Alisema fedha hizo zinatokana na ada ya maombi na ada ya mwaka ya mitambo hiyo, na kuagiza tume hiyo kuhakikisha kuwa mitambo yote inapatiwa leseni ndani ya siku 30.

"Mitambo ambayo itakuwa haijapata leseni ndani ya muda huo haitaruhusiwa kuendelea kufanya kazi na wahusika wote wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

**MARUFUKU KUTOA LESENI MPYA**

Waziri Biteko alipiga marufuku utoaji leseni mpya kwa kampuni au mtu binafsi aliyepewa Hati ya Makosa na kushindwa kurekebisha makosa hayo kwa kuwa ni kinyume cha kifungu cha 31(b) cha Sheria ya Madini.

Aliagiza tume kwa kushirikiana na wakuu wa mikoa nchini kutenga eneo moja kwa kila mkoa na kusimamia ujenzi wa mitambo ya uchenjuaji madini ndani ya miezi mitatu.

## TPSF yashtaki ma-RC

INATOKA UK 3

na kukamilisha sera ya kuendeleza sekta binafsi.

"TPSF inatimiza miaka 20 tangu kuanzishwa, tumeandaa majadiliano makubwa ya siku tatu ya viongozi wa serikali, sekta binafsi na wasomi na tumewaalika marais wastaafu wote kushiriki, tunapendekeza serikali mtusaidie kuhamasisha ushiriki wa viongozi sekta ya umma," alisema.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Waziri Kairuki alisema tangu aingie kwenye wizara hiyo mambo mengi yanayohusu sekta binafsi na uwekezaji yanafanyiwa kazi.

"Mapendekezo yenu mliyoyatoa kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) mengi yameanza kufanyiwa kazi na nilipofika wizarani niliitisha jalada la TNBC ili kuona utekelezaji wa masuala yote, masuala nitakayotilia mkazo ni kuwezesha na kuunganisha jitihada zote za wadau ikiwamo TPSF," alisema.

Waziri Kairuki aliihakikishia TPSF kuwa anayo dhamira ya dhati ya kufanya kazi nao na zaidi kutekeleza mapendekezo ya Rais Magufuli aliyowapatia wakati wakikaa naye kwenye vikao mbalimbali.

Waziri Kairuki alisema kwa maelekezo aliyonayo kutoka kwa Rais Magufuli ni kutatua vikwazo vyote vya uwekezaji.

## Wanufaika wa Tasaf

INATOKA UK 5

juu ya mbinu walizozitumia kufika hapo walipo sasa.

"Tumetembelea walengwa wa mpango unaoendeshwa na Tasaf Tanzania, kwa kweli wametupa 'challenge' (changamoto) tumebaki tunajiuliza ni kwa namna gani na sisi tutafika hapo walipofika wao," alisema Elongo na kuongeza:

"Tumejadiliana kwamba tuwaombe Tasaf watupe baadhi ya maofisa waje watuonyeshe mbinu walizotumia hasa namna ya walengwa wanavyojimudu katika kutumia kiwango kidogo cha fedha ya ruzuku kufanyia ujasiriamali na kujiongezea kipato, lakini pia itatubidi tuchukue baadhi ya walengwa waje kwetu kutoa mafunzo na ushuhuda."

Mwenyekiti wa kikundi cha Tujikwamue Barabara ya Mwinyi wanaotoka katika kundi la wanufaika wa mradi wa uhawilishaji fedha katika Kata ya Kilakala, Wilaya ya Temeke, Mariam Yakub, alisema baada ya kupewa elimu ya ujasiriamali na namna ya kutumia sehemu ndogo ya fedha wanayopewa na Tasaf waliunda kikundi hicho na kuanza kujiwekea akiba ambayo iliwasaidia kuanzisha miradi mbalimbali ya ujasiriamali.

"Sisi kabla ya kuingizwa katika mradi na Tasaf kwa kweli tulikuwa na hali ngumu hata mlo mmoja ilikuwa ni shida kuupata, lakini tulipoingizwa katika mradi na kupewa elimu ya ujasiriamali tulianzisha kikundi tukawa tunajiwekea Sh.1,000 kutoka katika sehemu ya ruzuku tunayopewa, tulifanya hivyo tukawa tunaongeza kiwango cha akiba hadi Sh. 2,000 kwa wiki na hivi sasa tunakopeshana hadi Sh.100,000 kwa ajili ya kufanya shughuli zetu wenyewe na pia tuna miradi ya kikundi," alisema.

## Barabara kuu sasa kutangaza utalii

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imeshauriwa kuangalia uwezekano wa kuweka alama katika barabara kuu zinazohusu vivutio vya makumbusho ambayo vipo katika mkoa husika ili kuongeza idadi ya utalii.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Utalii (Awotta), Merry Kalikawe, wakati wa maonyesho ya ndani ya utalii, na kwamba kuwekwa kwa makumbusho hayo katika barabara hizo itasaidia watu kujua vivutio hivyo na kuvitembelea.

"Kwenye njia kuu kila mkoa uweke makumbusho ndogo ya mkoa husika, tunaamini ikiwekwa na kuonyesha kuwa kilometa 50 kabla ya kufika katika makumbusho hiyo atafika na kupata historia ya mkoa huo na kufanya utalii. Hii itasaidia kuongeza utalii wa ndani," alisema.

Aidha, alisema Awotta wanafanya kazi kwa kushirikiana na wadau pamoja na wizara ikiwa na lengo la kuutangaza utalii wa nchini ili nchi inufaike kupitia rasilimali hiyo.

"Utalii sio kutembelea mbuga za wanyama pekee yake kuna mambo mengi hata ukisafiri kwenda mkoa mwingine kufuata matibabu huo ni utalii, hivyo wananchi tuweke utamaduni wa kufanya utalii itasaidia kukuza uchumi wetu," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Masoko kutoka Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Ernest Mwamaja, alisema lengo la maonyesho hayo ni kutunza utalii wa ndani na kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio vya nchini.

# Wataka marekebisho ya sheria umri wa mtoto

**Na Daniel Limbe**, CHATO

WANANCHI wilayani Chato mkoni Geita, wameiomba serikali kupeleka bungeni mapendekezo ya kurekebisha baadhi ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo inamtambua mtoto kuwa ni yule mwenye umri wa chini ya miaka 18.

Uamuzi huo unakuja kufuatia ongezeko la mimba shuleni kutokana na wanafunzi kujihusisha na ngono, huku wakitumia kisingizio cha kurubuniwa.

Mapendekezo hayo yametolewa na baadhi ya wakazi wa Kata ya Chato, wakati wakizungumza na Mkuu wa Wilaya hiyo, Mhandisi Mtemi Msafiri, kwenye mkutano wa dharura wa kijiji uliohusisha wazazi na walezi wa wanafunzi wanaosoma kwenye Shule ya Msingi Kalema.

Ni baada ya kaimu mtendaji wa kata hiyo, Paulo Samuel, kueleza kuwa Shule ya Msingi Kitela ndiyo imeonekana kinara kwa wanafunzi kubeba mimba kwa mwaka 2018, baada ya wasichana wawili kugundulika kuwa na ujauzito kati ya shule nne zilizoko ndani ya kata hiyo.

> **Cha kushangaza ni pale serikali inapotambua kuwa eti wanafunzi wanaobeba mimba hurubuniwa kufanya ngono...hii siyo kweli hata kidogo kwa maana hakuna mtoto anayeweza kubeba mimba...**

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao wakalazimika kuitupia lawama serikali kushindwa kutoa adhabu kali kwa aliyesababisha kupatikana mimba pamoja na aliyebebeshwa kwa madai kuwa wanapofanya tendo la ngono huwa wamekubaliana.

"Cha kushangaza ni pale serikali inapotambua kuwa eti wanafunzi wanaobeba mimba hurubuniwa kufanya ngono...hii siyo kweli hata kidogo kwa maana hakuna mtoto anayeweza kubeba mimba...anayebeba mimba huwa tayari amekomaa," alisema Helena Busumilo na kuongeza:

"Hayupo mtoto mdogo anayeweza kutoka nyumbani kwenda shule akiwaameficha kanga au kitenge cha mzazi ili akifika huko mtaani anabadili au kujifunika nguo hiyo ili watu wasimwelewe haraka...anakwenda kufanya uzinzi halafu sisi tunadanganyana eti huyo ni mtoto mdogo karubuniwa huo ni uongo."

Herman Kisumo, aliitaka serikali kutoa adhabu kali kwa pande zote mbili za wakosaji (mwenye mimba na aliyeibeba) badala ya adhabu hiyo kumwegamia mwanaume pekee, na kwamba sababu hiyo inachangia kwa kiwango kikubwa mabinti kutoogopa kufanya mapenzi katika umri mdogo.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu huyo wa wilaya alisema mkakati wa halmashauri hiyo ni kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaanza darasa la kwanza hadi la saba na kuendelea, na kwamba suala la mimba hatua kali zitachukuliwa kwa binti na mvulana watakaobainika kujihusisha na mapenzi.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola (kushoto), akimsalimia Kamanda wa Polisi Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha, SP Mussa Gumbo, waziri huyo alipokuwa anawasili mjini Karatu kwa ajili ya ziara ya kikazi. **PICHA: WMN**

# Wakulima wadogo wa migomba wahimizwa vikundi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wadogo wa migomba na mananasi wameshauriwa kujiunga kwenye vikundi vitakavyowawezesha kunufaika moja kwa moja na huduma zake.

Ushauri huo umetolewa na Kampuni ya Kilimo ya Organo iliyopo Jijini Dar es Salaam ambayo huzalisha miche kwa njia ya maabara.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Ammar Mussaji, alisema kampuni yake imelenga kuwainua wakulima wadogo na wale wa kati ili waweze kufaidika na shughuli zao za kilimo.

"Tumekuwa tukifanya kazi na wakulima wakubwa ambao ni wateja wetu wengi. Lakini kama kampuni ya Kitanzania tumejipanga kuwainua wakulima wadogo kupitia vikundi vyao ili waweze kunufaika na huduma zetu," alisema.

Mussaji alisema lengo la kampuni yake ni kuwafanya wakulima washiriki katika kilimo chenye tija na kuleta manufaa kwa mkulima mmoja mmoja na uchumi kwa ujumla wake.

"Wakulima wadogo ambao wamekuwa na changamoto nyingi ikiwamo ukosefu wa mitaji, hivyo tunawashauri waungane kwenye vikundi ambavyo vitawafanya wapate mikopo kwenye benki na hatimaye kupata huduma zetu ambazo zitakazowasaidia kujiimarisha katika sekta," alisema Mussaji.

Aidha, aliwatoa hofu wakulima wadogo kuhusu kupata mikopo benki kwa kuwa umoja wao utawafanya wawe na nguvu na kampuni yake itawasimamia kuanzia hatua ya mwanzo mpaka ya mwisho ikiwamo kuwahakikishia soko la ndani na nje ya nchi kwa mazao watakayokuwa wamezalisha.

"Serikali ya Rais John Magufuli imeshachukua hatua mbalimbali muhimu zenye lengo la kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya kilimo, hivyo ni nafasi ya wakulima wadogo hapa nchini kuanza kuchangamkia fursa hizo," alisema.

Alisema mazao ya ndizi na mananasi yana soko kubwa sana ndani na nje ya nchi kwa sababu kampuni yake imeshapata masoko ya uhakika nje na bidhaa hizo zinahitaji kwa kiasi kikubwa katika nchi za Asia na Marekani ya Kusini.

Mussaji alieleza sababu ya wakulima wadogo wengi kushindwa kuwa na kilimo chenye tija ni kutokana na kutopenda mabadiliko ikiwamo kilimo cha mazoea na kutopima afya ya udongo.

"Kilimo Organo imekuja na suluhisho la changamoto zinazowakabili wakulima wa migomba, mananasi na mihogo hapa nchini," alisema na kuongeza kuwa kilimo biashara kina nafasi kubwa ya kuchagiza maendeleo ya sekta ya viwanda Tanzania.

Kampuni hiyo ya Kitanzania ambayo imesajiliwa na kuanza rasmi shughuli zake mwaka 2016 imejikita katika kuzalisha miche mbalimbali ikiwamo migomba, mananasi, mihogo pamoja na aina nyingine mbalimbali kutokana na mahitaji ya soko, hutoa pia elimu juu ya afya ya udongo.

# Mkakati wasukwa kuongeza watalii

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, inatarajia kuanza mkakati maalumu wa kuongeza idadi ya watalii wenye umri mkubwa kuanzia miaka 50 na kuendelea.

Mkakati huo pia utalenga kundi la watalii wenye bima za maisha zinazowaruhusu kusafiri na ndege kubwa zenye marubani wawili zitakazotua moja kwa moja kwenye hifadhi pamoja na wale wasioweza kusafiri kwa njia ya barabara kwa muda mrefu.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na Uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro katika ziara yake ya kikazi Moshi mkoani Kilimanjaro.

Alisema mambo yaliyomo katika mkakati huo ni pamoja na kuanzisha magari yatakayokuwa yakitembea kwenye nyaya (cable cars) kwa ajili ya kutumiwa na watalii wenye umri mkubwa kupanda Mlima Kilimanjaro ambao kutokana na umri wao hawawezi kupanda kwa njia ya kawaida.

**Magari hayo yatasaidia kukuza utalii hata kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 kufika katika kilele cha mlima huo.**

Kanyasu alisema nchi imekuwa ikikosa pesa nyingi zinazotokana na watalii wa kundi hilo ambao ndio wengi wanaoingia nchini kwa ajili ya kutalii baada ya kustaafu.

Aliongeza kuwa magari hayo yatasaidia kukuza utalii hata kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 kufika katika kilele cha mlima huo.

Aidha, Kanyasu alisema serikali inatarajia kujenga viwanja vya ndege vikubwa kwa baadhi ya hifadhi zikiwamo Selous na Ruaha, ikilenga kundi la watalii wenye bima za maisha ambazo zinawaruhusu kusafiri kwenye ndege kubwa na zenye marubani wawili hali itakayosababisha kutua moja kwa moja katika hifadhi hizo tofauti na ilivyo sasa.

Naibu Waziri alifafanua kuwa kundi hilo limekuwa likikosa fursa ya kutembelea vivutio vya utalii kwa vile bima zao zimekuwa haziwaruhusu kutumia ndege ndogo zinazotua kwenye viwanja vidogo vya tope vilivyoko kwenye hifadhi nchini.

Katika hatua nyingine, Kanyasu alisema serikali imeanza kupitia baadhi ya masuala kutokana na malalamiko ya baadhi ya wadau wa utalii wa ndani ya nje ya nchi kudai kuwa utalii wa Tanzania ni wa ghali kulinganisha na nchi zingine.

"Tumeamua kuanza kulifanyia kazi suala hili kuwa "Tanzania is an expensive destination". Lengo letu ni kuongeza idadi ya watalii pamoja na mapato ambayo ni lengo kuu la serikali ya awamu ya tano.

Naye Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, Beatrice Looiboki, alimweleza Naibu Waziri kuwa tayari kampuni mbili kutoka China zimeonyesha nia ya kuanzisha magari ya waya yatakayokuwa yakiendeshwa kwa umeme katika mlima huo na taratibu zinaendelea.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akisalimiana na David Birigtoness, pamoja na watalii wengine alipotembelea kwa ajili ya kuzungumza na uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro pamoja na wadau wa utalii. **PICHA: WMU**

# Daktari bingwa atoboa siri upofu

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

DAKTARI bingwa wa magonjwa ya macho katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida, Dk. Ng'hungu Kuzenza, amesema kati ya watu waliochunguzwa na wataalamu wa macho, asilimia 94 ya waliokutwa na ugonjwa wa upofu, wana upofu unaozuilika na asilimia sita tu ya watu hao ndiyo wenye upofu usioweza kuzuilika.

Dk. Kuzenza alitoa takwimu hizo alipokuwa akielezea hali halisi ya ugonjwa wa mtoto wa jicho katika Mkoa wa Singida wakati wa hutolewa huduma ya upasuaji ya mtoto wa jicho kwa ufadhili wa Shirika lisilokuwa na kiserikali la Sight Saver.

Aidha, Dk. Kuzenza ambaye pia ni mganga mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida, alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa kwa ufadhili wa shirika hilo mwaka 2017, unaonyesha kwamba tatizo la ugonjwa huo bado ni kubwa.

"Kwa hiyo sana sana ni watu kujitokeza kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma ili waweze kupata huduma hizo, wasisubiri mpaka wafike kabisa kwenye sehemu ya kutokuona au anapofuka halafu anaendelea kubaki nyumbani wakati wataalamu tupo kuweza kuwasaidia," alisisitiza.

Naye Mwakilishi wa shirika la kidini kutoka Madrasa Al-Wahida, Abdulkarimu Juma Nkusui, aliyataja madhumuni pamoja na malengo ya shirika hilo la kidini kuwa ni kutoa huduma kwa wananchi kutokana na kuamini kwamba jamii inakabiliwa na mambo au changamoto mbalimbali katika maisha.

Hata hivyo, Nkusui alizitaja baadhi ya changamoto hizo ni magonjwa ya macho yamekuwa yakiwasumbua sana kutokana na mazingira yaliyopo ya kuwapo kwa vumbi na moshi.




# Majaliwa kuanza ziara ya Kagera

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuanza ziara ya kikazi ya siku tatu kuanzia leo mkoani Kagera, kwa kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kufanya vikao vya ndani vya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema Majaliwa baada ya kuwasili atatembelea na kukagua kituo cha afya Nyakanazi ambacho baadhi ya majengo yamejengwa na kukarabatiwa kwa gharama ya shilingi milioni 500 zilizotolewa na serikali kuu na baadaye kufanya mkutano wa hadhara katika uwanja wa Shule ya Msingi Nyakanazi wilayani Biharamulo.

Gaguti alisema kuwa Waziri Mkuu ataendelea na ziara yake katika wilaya za Missenyi na Karagwe, ambapo atafanya shughuli za chama na baadaye Februari 21 atakagua miradi ya CCM na kuhitimisha ziara yake mchana na kurejea mkoani Dodoma.

Gaguti aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi katika maeneo atakayotembelea Waziri Mkuu.

## CCM yawaonya viongozi mitaa

**Na Mwandishi Wetu,** LONGIDO

CHAMA Cha Mapinduzi, (CCM), kimewaonya viongozi wa serikali za mitaa ambao hawatimizi majukumu yao kwamba hakitarudisha majina yao kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mapema mwaka huu.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, (NEC), Itikadi na Uenezi, Humphery Polepole, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa vikao vyake na halmashauri kuu za baadhi ya kata katika Jiji la Arusha.

Kata hizo ni Engutoto, Lemara, Murieti Terrat, Olasiti pamoja na Osunyai.Polepole ambaye yupo mkoani hapa kwa ziara ya kikazi ya siku 14 alisema kuna baadhi ya wenyeviti wa mitaa ambao hawasomi taarifa ya mapato na matumizi kwa mujibu wa sheria, lakini pia hawafanyi mikutano mikuu katika mitaa yao.

Aidha, alisema baadhi ya viongozi hao wa serikali za mitaa pia wamekuwa hawatatui kero za wananchi zinazowakabili kwenye maeneo yao jambo ambalo haliendani la katiba ya CCM.

"Ndugu zangu naomba niwaonye muache mara moja tabia ya kutotekeleza majukumu yenu ya uongozi kwenye mitaa yenu. Viongozi wenye tabia hii katika uchaguzi huu wa serikali za mitaa unaofanyika mwaka huu tutakula vichwa vyao," alisema.

Alikemea vikali baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa wenye tabia za kuomba rushwa lakini pia kutoa rushwa kwa ajili ya kupata nafasi za uongozi. Alisema wajibu wa viongozi hao ni kuwatumikia wananchi katika maeneo yao na siyo kutengeneza mazingira ya kuwataka wananchi kutoa rushwa ili waweze kusaidiwa shida zao.

Kwa mujibu wa Polepole, uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka huu ni tofauti na chaguzi za miaka mingine kwa kuwa upembuzi yakinifu utafanyika dhidi ya wagombea wote wanaotaka nafasi za uongozi kwenye serikali za mitaa na vijiji.

Polepole alitumia fursa hiyo kuwataka viongozi hao wanahakikisha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanapata mikopo ya asilimia kumi inayotolewa na halmashauri zote nchini bila kubagua kikundi chochote.

"Rais Magufuli aliagiza halmashauri zote kutenga asilimia 10 kutoka kwenye mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi kwa kutoa mikopo vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Niwaombe wenyeviti wahakikishe makundi hayo yanapata mikopo bila mizengwe yoyote ile," alisema.

# Wanakijiji wachangia ujenzi wa madarasa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKAZI wa Kijiji cha Ilikiding'a katika Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, kwa kushirikiana na wadau wa elimu wamechanga fedha kiasi cha Sh. 3,300,000 na mifuko 390 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu ili kupunguza uhaba wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ilikiding'a.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi wenzake, wakati harambee ya kuchangia ujenzi wa madarasa, Mungaya Meshak, alisema kutokana na shule hiyo kuwa na upungufu wa madarasa wananchi walifikia maamuzi ya kuchangia fedha na saruji kwa ajili ya kujenga vyumba vitatu vya madarasa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

**Mimi binafsi nimeguswa na changamoto hii inayoikabili shule yetu na nimechangia fedha kiasi cha Sh. 1,000,000 pamoja na mifuko 200 ya saruji kuungana na wananchi wengine kujenga miundombinu ya shule yetu ya sekondari ili kuboresha mazingira ya wanafunzi kusomea.**

"Mimi binafsi nimeguswa na changamoto hii inayoikabili shule yetu na nimechangia fedha kiasi cha Sh. 1,000,000 pamoja na mifuko 200 ya saruji kuungana na wananchi wengine kujenga miundombinu ya shule yetu ya sekondari ili kuboresha mazingira ya wanafunzi kusomea," alisema.

Akisoma risala mbele ya mgeni rasmi Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, James Nchembe, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Ivan Mmari, alisema shule hiyo, ina mahitaji ya vyumba 24, vya madarasa na yaliyopo ni madarasa 18 tu na wanaupungufu wa vyumba vya madarasa sita.

Kwa upande wa nyumba za walimu, alisema wanauhitaji wa nyumba 54 na nyumba zilizopo ni tano upungufu ni wa nyumba 49, pamoja na mahitaji ya matundu ya vyoo 49, na matundu yaliyopo ni 16, upungufu ni wa matudu 33.

Aliongeza hadi sasa ujenzi wa vyumba 18 vya madarasa unaendelea, kwa mfumo wa ghorofa na kati ya madarasa hayo 18, madarasa matatu yameshakamilika na ujenzi huo umegharimu kiasi cha Sh. 280,000,000 hadi kukamilika.

Alisema hadi sasa ujenzi huo, umeshatumia Sh. milioni 57 kati ya fedha hizo Sh. milioni 40 zimetolewa na Halmashauri ya Arusha DC na Sh. milioni 17 ni michango ya wananchi.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Arumeru, James Nchembe, alisema lengo la serikali hadi kufikia mwaka 2020 itahakikisha wanaiboresha sekta ya elimu kwa kujenga madarasa, maabara pamoja na kupeleka vitendea kazi vya kufundishia shuleni.

Aliongeza uhaba wa madarasa umekuwa ukiathiri mfumo wa elimu katika nchi yetu kutokana uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza na mfumo wa elimu bila malipo ambapo umesababisha ongezeko la ufaulu kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Wilson Mahera, alisema kwenye shule hiyo, wanafunzi waliopangiwa kujiunga na kidato cha kwanza ni 286, hivyo halmashauri itahakikisha wanasimamia ujenzi wa madarasa hayo, kukamilika kwa wakati ili wanafunzi waanze kuyatumia.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (kushoto), akiweka jiwe la msingi la kituo cha pamoja cha biashara ya madini ya tanzanite, katika Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tamisemi yataka walimu wake kuongeza juhudi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Tixon Mzunda, amewataka walimu wa shule za serikali kuongeza juhudi na maarifa katika ufundishaji ili kuzishinda shule binafsi na kujenga heshima kwa shule za umma.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akifunga mafunzo ya walimu 600 kutoka shule za msingi za Arusha, Kilimanjaro na Manyara.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na Shirika la Helvetas kupitia mradi wa uboreshaji elimu kwa mfumo wa Queets.

"Shule za umma zina kila kitu, zana za ufundishaji, vyuo vizuri na hata mbinu bora wanazopewa walimu ni nzuri kuliko wa shule binafsi, lakini hata baadhi ya shule mishahara inalingana na walimu wetu wa serikali sasa iweje katika matokeo shule zao ziongoze kuliko zetu, ebu kaongezeni bidii mrudishe heshima za shule za serikali," alisema.

Alisema ili kufanikiwa ni lazima walimu washirikiane na kuacha majungu kazini, pamoja na kuwapenda wanafunzi wao kwa kuwafanya marafiki.

Mzunda aliahidi mwalimu atakayeongoza katika kufaulisha wanafunzi wake kwenye somo lake atapandishwa daraja na mshahara na hata ikibidi kupewa uongozi kwenye kata, wilaya au mkoa.

Alisema utafiti mdogo alioufanya hivi karibuni amebaini kinachochangia anguko katika shule hizo ni utoro asilimia 12 wa walimu kazini, asilimia 37 wapo darasani, lakini wanafundisha rejareja kwa kuingia darasani na kutoka na asilimia 51 wanazingatia taaluma na hao ameahidi kuwapandisha madaraja mara moja.

Alisema atapenda matokeo yajayo ya darasa la saba na kidato cha nne kwenye shule hizo, yafikie asilimia 85 ya kiwango cha ufaulu na hapo na endapo hayatafika hapo kila mwalimu na shule zao wajitathimini.

Pia alisema pamoja anatambua kuna jitihada za baadhi ya walimu na mikoa kuongeza kiwango cha ufaulu, lakini wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa walimu zaidi ya 80,000 kwa shule za msingi.

# Mbunge ajitosa malalamiko ya kampuni ujenzi Ujerumani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MBUNGE wa Moshi Vijijini, Anthony Komu, ameahidi kushughulikia malalamiko ya wafadhili wa kampuni ya ujenzi ya Ujerumani ambayo yamejitoa kusaidia ujenzi wa jengo la ghorofa mbili la makazi ya kudumu ya jamii ya watu wenye ulemavu katika Kata ya Uru Kusini, Moshi Vijijini.

Makazi hayo yatatumika kuwasitiri waliotelekezwa na familia zao na wengine kufukuzwa na wazazi wao kutokana na kupata ulemavu.

Akizungumza jana na wafadhili hao waliotembelea eneo la mradi wa ujenzi huo katika Kijiji cha Okaseni, Kata ya Uru Kusini, Komu alisema atatumia nafasi yake, mahusiano yake na serikali na jamii kuhakikisha kwamba kunapatikana nafuu ya kodi katika vifaa vyote vya ujenzi vitakavyoingizwa awamu ya pili kutoka nchini Ujerumani.

**Kuna nafuu ya kodi ambayo inatolewa, sasa mimi nitatumia nafasi yangu na mahusiano yangu na jamii kuhakikisha kwamba hizo nafuu za namna hiyo tunazipata.**

"Hili la vifaa vingine vyote vitakavyokuja tena, nitazungumza na Father Apollianaris Ngao (Padri) mapema ili kabla ya kuanza kusafirisha vifaa vingine, tuwe tumeshafanya utaratibu ambao upo kwa sheria zetu hasa kwa vitu vya msaada kama hivi; na vinavyokuja kwa mambo ambayo sio ya biashara visitozwe kodi.

"Kuna nafuu ya kodi ambayo inatolewa, sasa mimi nitatumia nafasi yangu na mahusiano yangu na jamii kuhakikisha kwamba hizo nafuu za namna hiyo tunazipata. Tumepata bahati kwa Padri Ngao ambaye ni mzaliwa wa Parokia ya Mawela alivyotimiza Jubilee yake ya miaka yake 25 akaamua michango ambayo ingetumika kwa sherehe, pongezi aitoe kwa ajili ya kujenga Rehabilitation Centre (kituo cha walemavu) kwa ajili ya watoto wetu."

Mwasisi wa wazo hilo, Padri Apollianaris Ngao, anayeishi Ujerumani akifanya kazi za kichungaji na Muungano wa Parokia tano zikiwamo za St. Paul, St. Joseph na Konrad zinazosimamiwa na Jimbo Katoliki la Ausburgy.

Wafadhili kutoka Ujerumani waliounga mkono ujenzi huo ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Uhandisi ya Bauunternehmen XGERBL, Franze Gerbl na wakurugenzi wenza wa Kampuni ya Bureau Veritas 1828, Vitus Lenz na Waltraud Lenz. Ujenzi wa kituo hicho, unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.2.

Wakiwa katika eneo la mradi huo, Komu aliwashukuru Wajerumani hao ambao mmemuunga mkono Padri Ngao, ambapo amesema wanachotaka kwa sasa ni jambo hilo kufahamika kwa watu wenye mapenzi mema ndani ya nchi yetu na nje ya nchi yetu ili walichangie likamilike kwa haraka kadiri inavyowezekana.

Awali, mmoja wa wafadhili hao, Franze Gerbl, alimweleza mbunge huyo kwamba walivyoleta kontena lenye vifaa vya ujenzi kama mbao, nguzo za chuma na vifaa vingine vingi kama mashine za kuchanganya zege na mashine ya kukatia vyuma, wamelipishwa kodi ya Euro 10,000 ambayo ni (Sh.milioni 24,307).

Akitafsiri ujumbe wao kutoka katika lugha ya Kijerumani, Mkalimani na mtaalamu wa Chuo cha Viungo Sanifu na Viungo Bandia (TATCOT) cha Hospitali ya Rufani ya KCMC, Hortensia Mallya, alisema Franze ana kampuni yake, ana watoto wawili wa kike, lakini amekosa mrithi wa kazi yake na vitu vingi akaamua alete Tanzania.

Wakati, Vutus na mkewe Waltraud, nao wana watoto wao lakini hakuna ambaye ana nia ya kurithi kazi za majenzi, ndio maana wakaona nao wamsapoti Padri Ngao kwenye hiyo ndoto yake.



Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye (katikati) na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania PLC, Hisham Hendi (wa kwanza kushoto), wakisikiliza shughuli zinazofanywa na kitengo cha ufanisi wa mtandao kutoka kwa Mhandisi Pendo Boshe wa kitengo hicho, wakati wa ziara katika ofisi za Vodacom Tanzania jijini Dar es Salaam jana. Nditiye alijionea namna ambavyo kampuni hiyo inafanya kazi zake kidijitali. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ujauzito shuleni wamkera DC Warioba

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Wilaya ya Moshi, Kippi Warioba, ameeleza shauku yake ya kutaka kuona kesi zote zinazohusu ujauzito dhidi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, watuhumiwa hawapewi dhamana tofauti na mahakamani.

"Kesi zote za ujauzito zisiishie kwa watendaji wa vijiji na kata wala polisi, nataka ziende mpaka mahakamani na mtuhumiwa asiachiwe kirahisi, dhamana yake ipatikane mahakamani," amesema.

Warioba alieleza hayo wakati akizungumza na wataalamu wa kada mbalimbali, wadau wa maendeleo na wananchi katika kikao cha kamati ya ushauri ya Wilaya ya Moshi (DCC).

Mkuu huyo wa Wilaya alisema suala la ujauzito shuleni ni lazima lichukuliwe kwa uzito wake na jamii nzima iungane katika kuua mila za kuombana misamaha kindugu na kumaliza kesi za ujauzito katika ngazi za familia.

Tanzania ni nchi ya tatu katika nchi za Afrika Mashariki kuwa na kiwango cha juu cha ndoa na mimba za ututoni, baada ya Uganda na Sudan Kusini.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (Unicef) ya mwaka 2017.

Hivi sasa katika Mkoa wa Kilimanjaro, kampeni ya kupambana na tatizo la mimba na ndoa za ututoni inaendeshwa katika maeneo mbalimbali na Shirika la Kwieco, Tusonge na Ajiso, baada ya tafiti nyingi kuonyesha bado kuna tatizo hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tusonge, Agnatha Rutazaa, akizungumzia utashi huo wa Mkuu wa Wilaya, amesema kama watoto wa kike wataendelea kukatisha masomo yao kwa mimba na ndoa za ututoni, itakuwa vigumu kufikia ndoto ya Tanzania yenye viwanda, kwa sababu nguvu kazi inayoachwa njiani ni kubwa.

Rutazaa amesisitiza kwamba takwimu za Democratic and Health Survey, zinaonyesha tatizo la mimba za ututoni nchini limeongezeka kutoka asilimia 23 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 27 mwaka 2016/17, kutokana na ukosefu wa huduma pamoja na elimu ya afya ya uzazi kwa vijana wa umri kuanzia miaka 15 hadi 18.

# Mashambani waisubiri neema nyongeza mshahara

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAFANYAKAZI wa mashambani katika sekta binafsi mkoani Kilimanjaro ni kama 'wanachekelea' kimya kimya nyongeza ya mshahara, baada ya waajiri kukaidi amri na kukubali kupandisha kima cha chini kutoka Sh.100, 000 hadi kufikia wastani wa Sh. 180,000 kwa mwezi.

Hayo yamo katika taarifa ya Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Mashambani na Kilimo (TPAWU) Kanda ya Kilimanjaro, Juma Mdolo.

Mdolo alitangaza ujio wa neema hiyo kwenye Mkutano Mkuu wa Kamati ya Utendaji ya Kanda, uliofanyika mjini hapa.

"Tumefanikiwa kuwapigania wanachama wetu katika nyongeza ya mshahara kutoka kima cha chini cha mshahara kwa sekta ya kilimo mashambani ambacho walikuwa wanalipwa wafanyakazi shilingi 100,000 kwa mwezi na tumekubaliana na waajiri kuanza kuwalipa wafanyakazi hao shilingi 180,000 kwa mwezi kwa lengo la kuwafanya wawe na maisha bora.

"Sisi viongozi tukiwa kama wawakilishi wa wafanyakazi mashambani tumekubaliana kuwa kuwapo kwa maslahi bora zaidi ya ajira kwa wafanyakazi wote walioajiriwa na wanachama wote wanalindwa na sheria na hakutakuwapo na vitisho vya aina yoyote," Mdolo.

TPAWU, Kanda ya Kilimanjaro ina jumla ya wafanyakazi 9,375 ambapo kati yao wanachama ni 3,850 na wafanyakazi wasio wanachama ni 5,525.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 19, 2019
TEKNOLOJIA . ELIMU . SAYANSI



Ukurasa 18

## UTAFITI
POMBE INAVYOATHIRI DNA NA KUONGEZA HAMU YA KUNYWA ZAIDI



## Wazazi walivyo chanzo cha mimba za utotoni Bariadi

Ukurasa 19



# KCMC yaleta nuru wagonjwa wa saratani Kanda ya Kaskazini

Ukurasa 16



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Salaam aleikum jamii!

'SALAAM ALEIKUM' ni tamko la maamkizi yenye dua wanayopeana watu wanapokutana. 'Jamii' ina maana zaidi ya moja lakini kwa muktadha huu ni 'wote pamoja.'

Siku hizi baadhi ya maneno ya Kiswahili hutumiwa ndivyo sivyo, yaani tofauti kabisa na maudhui (wazo linaloelezwa katika maandishi au katika kusema) yake.

Baadhi ya maneno yanayochanganywa ni 'mazishi' na 'maziko.' Maneno haya hutumika tofauti kidogo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar kama ninavyoeleza hapa chini.

Kwa Tanzania Bara, 'mazishi' ni shughuli na taratibu zinazohusu maziko yaani matayarisho kabla ya kuzika. 'Maziko' ni tendo la kumtia au kumhifadhi mfu kaburini. Mtu anaposema anakwenda mazishini maana yake anakwenda mahali palipofiwa.

Ndugu zetu wa Zanzibar, kidogo tumehitilafiana kwani 'maziko' ni mambo yote anayofanyiwa maiti hadi kuzikwa. Kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha la Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), 'maziko' na 'mazishi' ni maneno yenye maana moja tofauti na ilivyo Bara.

Huku Bara twatumia neno 'hani' kwa maana moja tu: enda kutoa rambirambi, enda kutoa pole kwa wafiwa. Zanzibar neno hilo latumiwa kwa maana mbili: i) kwenda kumpa faraja kwa maneno mtu aliyepata msiba; ii) kitendo cha kumpongeza mwingine (wenyewe husema 'mwengine').

Kamusi hilo pia laeleza kuwa baadhi ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili, kwa kutojua au kutokuwa makini, hulitamka neno Mrabaha kwa kuzibadilisha nafasi za silabi 'ba' na 'ha' na kulitamka 'mrahaba' yaani linazalisha neno jipya ambalo halimo katika lugha ya Kiswahili!

Aidha yasisitizwa kuwa maneno 'hafla' na 'ghafla' hutumiwa vibaya. Kitamkwa kimoja tu katika neno kinapotamkwa visivyo huweza kuleta tofauti/tafauti ya maana ya neno au kupoteza maana yake halisi.

'Hafla' na 'ghafla' ni maneno mawili yenye maana tofauti/tafauti. 'Hafla' ni shughuli inayofanywa kusherehekea (sio 'sheherekea') jambo maalumu. Mfano: "Hafla ya kuwaaga wastaafu ilifana." Kwa upande mwingine, 'ghafla' ni neno linaloeleza utokeaji wa jambo bila kutazamiwa. Mfano: "Wageni walikuja ghafla bila taarifa."

Neno lingine tunalohitilafiana kati ya Bara na Visiwani (Zanzibar) ni 'mrengu.' Bara tunatumia neno 'mrengu' kwa maana mbili, yaani ubao unaopigiliwa juu ya kingo za ghalawa ili iwe na uzito sawa pande zote; parapi, ndubi. Pili ni mwelekeo au msimamo wa kiitikadi au kisiasa. Mfano: Chama chake ni cha mrengu wa kushoto.

Zanzibar neno 'mrengu' limepewa maana moja tu nayo ni boriti inayofungwa kwenye ngalawa kushikilia mbera; =ndubi, parapi, mbera: mrengu wa mbele; mrengu wa nyuma.

Maneno mengine yatumiwayo vibaya ni 'shaka' na 'mashaka' kwa dhana kuwa neno hili la mwisho (mashaka) ni 'wingi' wa lile la kwanza (shaka) kumbe sivyo. 'Shaka' kama lilivyo halina wingi kama idhaniwavyo na wengi.

'Shaka' ni hali ya mtu kuwa na wasiwasi juu ya jambo; mushkili; udhanifu kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha. Kamusi ya Karne ya 21 neno 'shaka' linaelezwa kuwa na maana mbili: i) hali ya kujawa na wasiwasi na kukosa uhakika wa jambo; hatihati, wahaka (nahau) tia shaka (a) bila shaka (b) pasi na wasiwasi wowote. 'Shaka' ii) ni fukuza; shunga, winga, furusha.

'Mashaka' ni matatizo, shida au masahibu yanayompata mtu katika maisha. Kwa mfano yaweza kusemwa: "siku hizi watu wanaishi kwa mashaka" au "maisha ya siku hizi ni ya mashaka." Ni kosa, kwa mfano kuulizwa "kesho utakuwa tayari kwenda safari uliyopanga?" nawe ukajibu "sina mashaka" ni kosa. Jibu sahihi ni "hapana shaka," yaani utakwenda bila kizuizi chochote.

Wahenga walisema "Kikulacho ki nguoni mwako." Maana yake kikulacho huwa ndani ya nguo uliyoivaa au uliyonayo mwilini.

Methali hii hutukumbusha kuwa mtu anayeweza kutudhuru ni yule anayetufahamu vizuri. Mathalani anayeweza kukuhasiri ni rafiki yako au jamaa wa karibu.

Kwa miaka kadhaa sasa nimekuwa nikiandika makala za Kiswahili kwa kukosoa maneno yatumiwayo vibaya na kuyatolea maana yake halisi. Yasikitisha kuwa gazeti ninalolitumia kusahihisha na kueleza maana ya maneno yanayopotoshwa, nalo limo kwenye mkumbo wa kuwapotosha wasomaji!

Wallahi (tamko la kiapo kuthibitisha kuwa linalosemwa ni kweli) kikulacho ki nguoni mwako!

Soma hii: "Vera anapopagawa na penzi la Calisah. Mrembo maarufu kutoka Kenya, Vera Sidika, amefanya kufuru baada ya kumnunulia gari la kifahari mpenzi wake mpya Mtanzania Calisah."

'Pagawa' ni pandwa na pepo yaani kiumbe asiyeonekana na anayedaiwa kuwa humwingia mtu kichwani na kusema anayotaka kupitia mtu huyo ambaye kwa wakati ule ni kiti cha pepo! Je, Vera Sidika alipandwa na pepo hata kumnunulia mpenziwe gari?

'Kufuru' ni sema, fanya au amini jambo kinyume na mafunzo ya dini yako, dharau dini yako; maneno au mambo yaliyo kinyume na mafunzo ya dini yako. Je, Vera Sidika alifanya kinyume na imani yake ya dini kwa kumnunulia mpenzi wake gari? Dini gani inayomkataza mtu kumnunulia mpenziwe gari

Namalizia makala yangu kwa kuwapa wasomaji wangu mtihani: Maneno haya yana maana gani? Hoho, mhenga, na mhanga (lenye maana tatu). Nitumieni majibu yenu kwa maandishi kwa kutumia namba 0784 334 096.

**Methali: Mvunja nchi ni mwananchi.**

***marobarnabas@yahoo.com***
***0715/0784 33 40 96***

## ELIMU KUTOKA POLISI




Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola. **PICHA: MTANDAO**

# FAHAMU HISTORIA YA JESHI LA POLISI TANZANIA

JESHI la Polisi Tanzania lilianza katika kipindi cha ukoloni ambapo mnamo mwaka 1885, Wajerumani waliofika Tanganyika kwa lengo la kuitawala waliamua kuunda kikundi cha watu kilichofanya kazi ya Polisi ili kurahisisha shughuli zao za kiutawala.

Mwaka 1916 wakati wa Vita kuu ya kwanza ikiendelea Ulaya na Afrika, kundi la Maofisa 31 (NCO) kutoka Afrika Kusini wakiwa na silaha (Rifle) walifika Tanganyika kufanya kazi za Polisi.

Miaka mitatu baadaye, mnamo Agosti 25, 1919 Serikali ya Kiingereza ilitangaza katika Gazeti la Serikali Namba Vol.1 No.21-2583 kuwa Jeshi la Polisi Tanganyika limeanzishwa rasmi.

Makao Makuu ya Jeshi hilo yalikuwa Wilayani Lushoto chini ya uongozi wa Major S.T DAVIS.

Mnamo mwaka 1921 kundi lingine la Wakaguzi kutoka Ulaya lilifika nchini Tanganyika kuanzisha shule ya mafunzo ya Polisi huko Morogoro.

Mwaka 1925 Kituo cha kwanza rasmi cha Polisi nchini kilifunguliwa huko Lupa Tingatinga kwenye machimbo ya dhahabu Chunya ambapo ilipofika mwaka 1930 Makao Makuu ya Polisi yalihamishwa kutoka Lushoto kuja Dar es Salaam.

Mnamo mwaka 1949 kikosi maalumu cha kutuliza ghasia kichokuwa kikijulikana kwa jina la Motorized Company kwa sasa ni F.F.U kilianzishwa rasmi kwa lengo la kurejesha amani penye vurugu.

Kipindi hicho ndipo Vijana mbalimbali wa Kiafrika kutoka shule mbalimbali za Sekondari nchini walichaguliwa kujiunga na Jeshi la Polisi na kuwa Wakaguzi chini ya uangalizi (Probation Inspectors).

Ili kurahisisha mawasiliano ndani ya Jeshi la Polisi, mwaka 1952 Kikosi cha Mawasiliano (Signals Branch) kilianzishwa katika Polisi bila kutumia nyaya za simu.

Ilipofika mwaka 1958 askari wa Polisi wa Kike (Women Police) walijiunga kwa wingi na Jeshi la Polisi chini ya uongozi wa Miss Payee.

Jeshi la Polisi lilianza kubadili mwelekeo baada ya Tanganyika kupata uhuru mnamo Desemba 9, mwaka 1961 ambapo mfumo ulibadilika kutoka Jeshi la Polisi linalowatumikia Wakoloni na kuwa Jeshi linalowatumikia Wananchi kwa mujibu wa sera za Serikali ya Wananchi.

Mwaka 1962, kwa mara ya kwanza nafasi ya Kamishna wa Polisi aliyekuwa Mzungu Mr. M.S Wilson - CP, ilichukuliwa na Mwafrika Elangwa Shaidi - CP.

Mnamo mwaka huo 1962 ndio ulikuwa mwaka wa neema ambapo Maofisa 10 Waafrika waliteuliwa kuchukua nafasi za Wakuu wa Polisi wa Mikoa (Regional Police Commanders) kwa lengo la kuhakikisha mikoa hiyo inakuwa katika hali ya usalama.

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwezi Aprili mwaka 1964 na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya Jeshi la Polisi kuwa la Muungano na Kamishna wa Polisi mwafrika Elangwa Shaidi alipandishwa cheo na kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) na kukabidhiwa madaraka ya kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano,**
**Makao Makuu ya Polisi,**
**S.L.P 9141**
**Dar es Salaam.**
**Baruapepe:habariphq@yahoo.com**
**habari.phq@tpf.go.tz**

ELIMU

## NA PROFESA ISSA OMARI

# Elimu Tanzania inahitaji kupewa kipaumbele na kuchangamka

KWA sisi ambao tumeingia darasa la kwanza mwaka 1951 na sasa ni walimu wa elimu ya walimu, tunaweza kusema juu ya elimu hapa Tanzania kwa majivuno na masikitiko.

Nilimaliza masomo yangu yote mwaka 1972 na nimekuwa naendelea kufundisha na kujielimisha juu ya elimu ya Tanzania wakati wote huo. Kwa hiyo ninaweza kuchangia mawazo katika elimu.

Kwa upande wa kuporomoka kwa elimu yetu, hatuna budi kwenda mbali.

Mwaka huu majibu ya kidato cha nne kwa mwaka 2018 yametoka, ufaulu ama mafanikio katika somo la hesabu yalikuwa duni, ni asilimia 20 tu, yakifuatiwa na hesabu za biashara (book keeping).

Ukilinganisha na Kiswahili, ufaulu ulikuwa ni asilimia 90. Pamoja na kwamba wanafunzi wanafaulu vizuri Kiswahili, lakini hawapati kazi huko tunakokwenda kwenye ulimwengu wa hesabu, sayansi, teknolojia na Kiingereza.

Tusidanganyane kwamba hivyo ndivyo ulimwengu utakavyokuwa, tujiandae tusije tukalalamika kwamba hakutujua.

Hapa Tanzania unaambiwa mtoto wa darasa la saba hawezi alfabeti (ABCDE...), wala kuandika jina lake sawasawa!

Unaambiwa mwanafunzi wa kidato cha nne hawezi kujieleza kwa kuandika au mazungumzo hata kwa Kiswahili, anakuangalia tu!!

Kijana anamaliza chuo kikuu hawezi kuandika barua sahihi ya kuomba kazi au kukaa kwenye mazungumzo, mahojiano (interview) ya kuajiriwa.

Unajiuliza kuna tatizo gani hapa? Sasa tuwe wakweli kuna wanafunzi ambao wanajiweza, hata hivyo wengi hawajiwezi na kwa maana hiyo hawaajiriki.

Inabidi kutafuta sana na kutengeneza mazingira mazuri ya kujifunza kazini, kama wanajiweza...wengine hata motisha hawana.

Tuendelee kwenye mapambano ya kubadili hali hii ambayo hata kwa nchi za Afrika Mashariki na Kusini ni aibu tupu.

Inajulikana ulimwengu mzima kuwa elimu ni walimu. Walimu wetu wana upungufu mkubwa sana kwenye masomo wanayofundisha, maana walifanya vibaya shuleni na bado tunao wengi wa daraja la A na diploma.

Siku hizi wenye shahada wanafundisha shule za msingi na sekondari katika nchi nyingi na lazima wawe walifaulu vizuri katika masomo wanayofundisha.

Ni muhimu mwalimu ajue pia kwamba ana kazi tatu ngumu shuleni. Kwamba mwanafunzi ajue somo jina lake kikamilifu, lakini pia mwanafunzi anyoke kama mwanadamu kwenye mahusiano na mazungumzo.



Wanafunzi kama hawa wanahitaji uwekezaji mkubwa ili kunyanyua ubora wa elimu. **PICHA: MTANDAO**

"Nchi zingine kama vile Amerika, walitangaza 'National at Risk' (Taifa liko hatarini) walipoona wanapitwa katika elimu, kweli likawa janga kuanzia kwa rais wa nchi mpaka huku chini shuleni, wimbo mmoja.

Na hatimaye mwanafunzi ajue kujiendeleza akiwa shule na baada ya hapo, hivyo asome na kujiandaa kwa maisha.

Mwanafunzi anastahili kuona mazingira ya shule kuwa ni ya maendeleo. Hii ya kusomea chini ya miti na kuketi chini darasani na kuandika kwenye udongo, haimfundishi mwanafunzi maisha ya baadaye.

Kazi ya kuengeneza shule na mazingira yake iwe ni ya serikali kuu kwanza. Si ya kuwaachia wanafunzi na wazee ambao wengine hawakusoma!!!

Wanafunzi wajifunze kutengeneza shule na mazingira yake lakini si waachiwe. Kama Mheshimiwa Waitara alivyosema Februari 2, mwaka huu: "Schools have become badly dilapidated, from becoming totally forgotten" (The Guardian p4).

Wanafunzi wasipopenda shule si ajabu ni kwa vile mazingira hayavutii. Suluhisho si kuwaadhibu bali kutengeneza mazingira mazuri!!!

Mwanafunzi ajue kuwa anavyokwenda juu, uwezekano wa kuajiriwa kwenye fani na kazi anayoipenda upo katika muda mrefu ujao. Kazi kubwa ya serikali ni kutengeneza mazingira ya kazi kwa wanaohitimu.

Tunajua kuwa shida ipo lakini hapa ni kuwasomesha na kuwaambia wajitegemee kwa kuuza vitumbua barabarani!!

Sawa kuna wachache wanaojitegemea, lakini isiwe kwa amri ya serikali kwa wanaosoma na kujitegemea. Serikali ina wajibu kuwasaidia wanafunzi, walimu na wananchi huko karibu na mashuleni.

Sikiliza haya kwa waliojitokeza na kuandika katika magazeti yetu, inasikitisha:

'Ni aibu wanafunzi kusomea chini ya miti, jamii inasubiri serikali' au na serikali inasubiri jamii? (Nipashe Februari 6, 2019 p.6)

'Wanafunzi 673 Ngara watoroka shule kwa sababu mbalimbali (Mtanzania Februari 5, 2019, p.8)

'Poverty in Tanzania traced as consequences of the education sector in the country' (Daily News Februari 4, 2019 p.8)

Hii ni mifano tu ambayo imejaa kwenye magazeti yetu yanayotufanyia kazi nzuri sana ya kufichua uozo uliopo kwenye elimu yetu ambayo tunaipenda na kuienzi. Mimi imenifikisiha hapa nilipo, lakini tuko wangapi?

**MATATIZO YAKO WAPI?**

Kwanza lazima tukubali kwamba matatizo ni makubwa, mazito na ya kutisha.

Kwanza kabisa ni kiasi kidogo sana cha asilimia 15 tu ya matumizi yote ya serikali ndiyo hutumika katika elimu.

Ukienda Kenya, ni takriban asilimia 25. Senegal, Gambia hivyo hivyo. Uganda kama asilimia 29.

Sisi tuko nyuma sana, na bila kuwekeza katika elimu, tutabaki hivi hivi na malalamiko yetu. Lazima tupandishe kwango hicho na Benki ya Dunia (WB) inasema kiasi cha chini kabisa kiwe asilimia 20.

Pili idadi ya wanafunzi iliyopo shuleni na vyuoni ni ndogo sana. Katika ngazi ya msingi, tumepita asilimia 90, hivyo tuko sawa kwa idadi tu, acha ubora ambao unatisha kwa ubaya.

Kwa sekondari tumefikia asilimia 35 ambayo ni ndogo sana katika ulimwengu wa leo. Wenzetu wako mbali huko kwenye asilimia 75.

Katika Elimu ya Juu na Teknolojia, hatujafika hata asilimia tano (5%)!!! Kama tunataka kuwa na uchumi wa kati na ulio na mizizi katika teknolojia, tunahitaji kufikia asilimia 15.

Angalia umbali tulipo na ndoto zetu za maendeleo! Mifano ipo Asia, tunaweza kuiga.

Tatu mazingira ya kusomea kuanzia chini mpaka juu, tumekuwa wabadhirifu tu. Shule zilizojengwa kabla na uhuru, ni sasa tunakumbuka kwamba zinahitaji matengenezo ya mara kwa mara. We don't have 'maintenance culture' -utamaduni ya kukarabati.

Angalia shule za sekondari za Ilboru, Minaki, Pugu na Tabora, mpaka wanafunzi wanazikimbia kwa sababu ya kuumwa kunguni!!!

Angalia design ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)!! At best can say archaic!!!

**JANGA LA TAIFA**

Majuzi aliyekuwa mkuu wa nchi, Benjamin Mkapa alitangaza kwamba 'Elimu ilikuwa janga la taifa' Hakuna aliyeshtuka au kugutuka!!!

Nchi zingine kama vile Amerika, walitangaza 'National at Risk' (Taifa liko hatarini) walipoona wanapitwa katika elimu, kweli likawa janga kuanzia kwa rais wa nchi mpaka huku chini shuleni, wimbo mmoja.

Hivi ndivyo tunaitaka Tanzania iwe, tupunguze katika 'mega projects (Miradi mikubwa) of interest to the ruling elite na wasanii/tourism (utalii) and fund and manage education well (tuwekeze na kusimamia elimu vizuri. Hili ni janga la Taifa Rais.

**Issa Mcholo Omari,**
**Profesa wa Elimu Chuo Kikuu,**
**S.L.P 33875, Dar es Salaam.**
**Simu: 0713332541 e-mail:**
**issaomari88@yahoo.com**

SAYANSI

**NA MARY MOSHA, MOSHI**

# KCMC yaleta nuru wagonjwa wa saratani Kanda ya Kaskazini

## ■ Inajenga jengo maalum la wagonjwa wa saratani na jengo la mionzi

SARATANI ya shingo ya kizazi ni ugonjwa ambao hutokana na mabadiliko ya mfumo wa chembechembe au cells zilizo katika shingo ya kizazi.

Mabadiliko hayo hupelekea chembe chembe hizo kushamiri na kuzaliana kwa kasi kinyume na mpangilio wa maumbile.

Saratani ya Shingo ya kizazi yasemekana kuongoza kwa kusababisha vifo vya wanawake kwenye nchi zinazoendelea.

Ripoti ya mwaka 2012 ya Shirika la Afya Duniani (WHO), inasema kati ya matukio 75,000 ya waathirika wa saratani ya kizazi barani Afrika, wagonjwa 50,000 walifariki dunia.

> "Mionzi hii haina maumivu na madhara yake ni uchovu, tupu kuwa nyembamba sana (narrowing of vagina) na mgonjwa kupungukiwa na damu,"

**KINACHOSABISHA SARATANI YA SHINGO YA UZAZI**

Ufafanuzi wa swali hili unatolewa na Dk. Severini Furaha, Mkuu wa Kitengo cha Saratani katika Hospitali ya Rufaa ya KCMC iliyo Manispaa ya Moshi, Mkoani Kilimanjaro.

Anatoa ufafanuzi huu katika Kilele cha Siku ya Saratani Duniani kwa mwaka huu wa 2019, alipofanya mahojiano na Mwandishi wa makala haya.

Dk. Furaha anasema ripoti za utafiti wa kisayansi zimeafiki kuwa asilimia 99 ya saratani ya shingo ya kizazi, hutokana na maambukizi ya virusi vya 'Human Papillomavirus' au HPV vilivyoko katika jamii ya papilloma.

Anasema baadhi ya virusi hivyo vyenye aina zaidi ya 100 huambukizwa kwa njia mbalimbali ikiwemo kujamiana hasa katika umri mdogo au chini ya miaka 18.

Mbali na njia hiyo, mtaalamu huyo anataja sababu zingine kwamba ni kuwa na wenzi tofauti au mwenzi aliye na wapenzi tofauti na uvutaji wa sigara, kwani hupunguza nguvu ya kinga mwilini (impairs immune system).

Mtaalamu huyu anasema saratani hii pia huwashambulia watu wenye kinga hafifu ya mwili au magonjwa kama Ukimwi na wenye uzazi wa mara kwa mara.

**DALILI ZAKE**

Dk. Furaha anataja dalili za ugonjwa huo kuwa ni kutokwa na majimaji au uchafu wenye harufu kali ukeni, kutokwa na damu ukeni mbali na siku za mwezi au baada ya tendo la ndoa.

Zingine ni pamoja na maumivu makali ya sehemu ya chini ya tumbo (pelvic area), kuhisi maumivu makali wakati wa kujamiana na kupungua kwa uzito wa mwili bila kukusudia.

Aidha, mkojo wenye matone ya damu.

**DHANA POTOFU**

Pamoja na kuwepo kwa dhana potofu kuwa ukipata saratani ya shingo ya kizazi hauwezi kupona, Dk. Furaha anasema Saratani ya shingo ya kizazi inaweza kutibika iwapo itagundulika mapema.



Mmoja wa wanafunzi waliopatiwa chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi kutoka shule ya msingi Kapera, wilayani Bukombe, Agnes Ezekiel. **PICHA: MTANDAO**



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

**VIPIMO VYAKE**

Dk. Furaha anasema vipo vipimo vingi ambavyo vinafanyika ili kubaini kuwepo kwa viashiria vya saratani hiyo.

Anabainisha (Pap smear), Chembechembe au seli za shingo ya kizazi huchukuliwa na kuchunguzwa kwa kutumia Darubini.

Anasema kipimo cha Cervical Biopsy, kinahusisha uchukuaji wa kipande cha nyama kutoka kwenye uvimbe katika shingo ya kizazi ambacho hupelekwa maabara kuchunguzwa kama kuna saratani au la.

Ni kipimo kinachothibitisha uwepo wa saratani.

**COLPOSCOPY**

Colposcopy anaitaja Dk. Furaha kuwa ni aina ya darubini inayotumiwa kuchunguza shingo ya kizazi ili kuangalia kama kuna tishu ambayo si ya kawaida.

Anasema kipimo hiki kinaweza kufanywa na daktari bingwa wa magonjwa ya kina mama.

**CONE BIOPSY**

Kipimo kingine anachokitaja Dk. Furaha ni Cone Biopsy.

Anasema, kipimo hiki hufanywa kwa kuchukua nyama kutoka katika shingo ya kizazi mfano wa koni kwa uchunguzi zaidi na hufanywa katika chumba cha upasuaji mgonjwa akiwa amepewa dawa ya nusu kaputi.

Anafafanua kipimo hiki kinaweza kutumiwa kama njia moja ya kutibu saratani ambayo haijaenea na ambayo ni ndogo sana kuondolewa kwa njia hii.

Anabainisha kwamba kuna aina mbili za kufanya kipimo hiki.

Anasema aina ya kwanza ni ya kukata kipande cha nyama kutoka katika shingo ya kizazi kwa kutumia nyaya ya umeme inayojulikana kitaalamu kama loop electrosurgical excision procedure (LEEP).

"Aina ya pili ni ya kukata nyama ya shingo ya kizazi kwa kutumia visu maalum vya upasuaji au laser PET Scan...kipimo hiki pia huweza kuthibitisha uwepo wa saratani," anasema na kuongeza:

"Na kuangalia maendeleo ya mgonjwa baada ya kupata tiba Blood test, Vipimo vya damu, kuangalia wingi wa damu, kwa sababu wagonjwa wengi wanakuwa na upungufu wa damu kutokana na kuvuja damu mara kwa mara."

Aidha, Dk. Furaha anataja kipimo cha CT Scan ambacho huangalia kibofu cha mkojo kama kimeathirika au la.

"Lakini pia huangalia kama saratani imesambaa kwenye mifupa, ini, figo na sehemu nyingine za mwili," anasema.

**MAKUNDI YA SARATANI YA SHINGO YA KIZAZI**

Mkuu huyu wa Kitengo anasema saratani ya shingo ya kizazi ina makundi yake ambayo yamegawanyika kulingana na ngazi ama hatua zake (TNM ama FGO-Classification).

Dk. Furaha anataja ngazi ama hatua ya kwanza (stage 1) kuwa ni Saratani iliyo kwenye chembechembe au seli za aina ya epithelium, lakini haifiki kwenye nyama za ndani za shingo ya kizazi.

Ngazi ya pili au hatua ya pili (stage II) anayoitaja mtaalamu huyu ni ile ya Saratani iliyosambaa hadi kwenye tupu ya mwanamke sehemu ya juu kwa 2/3.

Anataja ngazi au hatua ya tatu (Stage III) kuwa ni ile ya Saratani iliyosambaa hadi kwenye ukuta wa nyonga na sehemu ya chini ya uke kwa 1/3, ambayo inaleta madhara katika figo.

"Ngazi au hatua ya nne (stage IV) ni ile Saratani iliyosambaa hadi nje ya tupu ya mwanamke na pia husambaa hadi kwenye sehemu zingine za mwili kama mapafu, figo na mifupa," anasema.

**JE SARATANI INATIBIKA?**

Dk. Furaha anasema saratani inatibika kwa tiba ya kuchoma (cauterization).

Anasema tiba hii hutolewa kwa wagonjwa wenye matatizo ya shingo ya kizazi kabla haijawa saratani na hutumia joto kali, umeme au kemikali kuchoma sehemu iliyoathirika.

Aidha, mtaalamu huyu anasema ipo pia tiba ya dawa (Chemotherapy), ambayo mgonjwa hutumia dawa za saratani zinazoua chembechembe au seli za saratani ya shingo ya kizazi.

"Dawa hizi hutolewa kwa mgonjwa ambaye saratani imeshasambaa mwilini na inahusisha dawa moja pekee au mchanganyiko wa dawa zaidi ya moja ambazo mgonjwa hupewa kwa njia ya dripu au kumeza kupitia mdomoni,"anasema.

**TIBA YA MIONZI**

Dk. Furaha anabainisha kwamba ipo pia tiba ya mionzi (radiation therapy) ambayo hutumia mionzi ya X-ray, gamma na neutrons ambayo huua seli za saratani hii.

"Mionzi hii haina maumivu na madhara yake ni uchovu, tupu kuwa nyembamba sana (narrowing of vagina) na mgonjwa kupungukiwa na damu," anasema.

**MKURUGENZI**

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Gileard Masenga anasema Hospitali ya KCMC iko katika mpango wa kujenga jengo maalum kwa ajili ya wagonjwa wa saratani pamoja na jengo la Mionzi.




Hospitali ya Rufaa ya KCMC, inayotarajia kujenga jengo la saratani.

Endelea Uk.18

JIELIMISHE



Kiti kilicho na alama ya nazi katika mikono yake. **PICHA: MTANDAO**

# Michoro ya Hitler yakosa mnunuzi kwenye mnada

PICHA tano zinazodaiwa kuchorwa na kiongozi wa Nazi Adolf Hitler, zimekosa mnunuzi katika mnada nchini Ujerumani.

Mnada wa Jumba la Wiedler ulilenga kuchangisha Paundi za Uingereza 40,000 kutoka kwa mchoro huo unaouzwa bei ghali.

Madai ya kughushi bidhaa hizo yaliukumba mnada huo na meya wa mji huo Ulrich Malu, alitaja kuwapo watu wenye nia mbaya.

Mauzo hayo yalifanyika mjini Nuremberg, Ujerumani, mji ambao una sifa za kuandaa mikutano ya Nazi ambapo viongozi wakuu wa Nazi walishtakiwa kwa uhalifu wa vita.

Mauzo pia yalishirikisha bidhaa zinazodaiwa kumilikiwa na dikteta huyo kikiwemo chombo cha kuwekea maua na kiti kilicho na alama ya Nazi katika mkono wake.

Chini ya uongozi wa Hitler kati ya 1933-45, Nazi walianza vita vya dunia vya pili wakiwa na nia ya kutekeleza sera yao ya mauaji ya kimbari ambayo yalisababisha mauaji ya Wayahudi milioni sita, mamilioni ya raia wengine pamoja na wapiganaji.

Onyesho la alama hiyo ya Nazi hadharani haliruhusiwi nchini Ujerumani, isipokuwa kwa ajili ya masuala ya elimu ama sababu za kihistoria.

Jumba la mnada huo lilifanikiwa kuzunguka sheria kwa kuficha alama hiyo.

**MNADA WAKABILIWA NA CHANGAMOTO**

Makumi ya michoro, ikiwemo ile iliyoandaliwa kuuzwa ilikamatwa kutoka kwenye jumba hilo la mnada wiki iliyopita na maofisa wa polisi wa Ujerumani.

Waendesha mashtaka wanasema kuwa takriban michoro 63 iliyo na saini ya AH ilikamatwa kutokana na madai ya kughushi.

Uchunguzi ulianzishwa dhidi ya watu ambao hawakutambulika kwa tuhuma za kughushi bidhaa hizo, mbali na kufanya udanganyifu, mwendesha mashtaka wa Nuremberg, aliambia AFP.

Alithibitisha kuwa jumba la mnada huo lilishirikiana nao kutoa michoro kwa kujitolea.

Mauzo ya michoro hiyo inayodaiwa kutoka kwa dikteta huyo mara kwa mara huzua hisia na tuhuma za kughushi.

Mwezi uliopita maofisa wa polisi wa Ujerumani walipata vitu vya Hitler wakiwa na wasiwasi kuhusu kule ambako vilikuwa vikitoka.

Hitler ambaye alikataliwa mara mbili na shule ya uchoraji ya Vienna, anajulikana kuuza kazi zake akiwa kijana.

Kazi zake nyingi zilizodaiwa na wataalam kuwa za kiwango cha chini zimeuzwa katika miaka ya hivi karibuni.

Mwaka 2015, Jumba la mnada la Wiedler liliuza zaidi ya makumi ya michoro inayodaiwa kutoka kwa Hitler kwa Euro 400,000.

Wanunuzi walitoka Ujerumani, China, Ufaransa, Brazil na UAE.

Mwaka 2014, jumba hilo la mnada liliuza mchoro wa rangi za maji kuhusu mji mkuu wa Munich kwa Euro 130,000.

Uuzaji wa kumbukumbu za Nazi ni suala linalosalia kuzua mgawanyiko duniani.

Wanunuzi wengine wanasema kuwa wananunua kutokana na sababu za kihistoria, lakini wanaharakati wanaonya kwamba vitu hivyo pia hununuliwa na watu wa mrengo wa kulia ambao wanatii utawala wa Hitler.

**BBC**

## JE, WAJUA?



Chui aina ya Tiger aliyekutwa ametelekezwa katika jumba lisilokaliwa na watu nchini Marekani. **PICHA: MTANDAO**

# Akutana na chui akivuta bangi kwenye maficho

JAMAA mmoja ambaye aliingia kwenye nyumba iliyotelekezwa nchini Marekani ili avute bangi, alipatwa na mshtuko asioutarajia baada ya kukutana na Chui mkubwa aina ya Tiger ambaye alikuwa ametelekezwa.

Polisi jijini Houston, Texas wanasema awali mwananchi huyo alipowapigia simu, walidhani kuwa yupo kwenye njozi baada ya kuvuta bangi.

Lakini maofisa hao walipofika walimkuta Tiger mkubwa amefungiwa ndani ya kizimba.

Hakukuwa na alama yeyote iliyoonyesha kuwa kuna watu waliokuwa wakiishi kwenye jengo hilo, japo kulikuwa na nyama mbichi karibu na kizimba hicho.

Polisi sasa wanasema watafanya uchunguzi ili kubaini namna gani mnyama huyo alifika hapo.

Wameeleza kuwa 'raia mwema' ambaye aligundua uwepo wa tiger huyo hakuwa akiishi kwenye nyumba hiyo, na aliingia tu ili 'avute bangi'.

"Tuliwauliza iwapo kama wamelewa dawa za kulevya (bangi) ama kweli wamemuona tiger," msemaji wa polisi amewaambia waandishi wa habari.

Polisi pia wameeleza kuwa kizimba hicho hakikuwa madhubuti, na kilikuwa kimefungwa na bisibisi na kamba ya plastiki.

Japo mnyama huyo hakuwa mwenye hasira, ilibidi kwanza apigwe dawa ya usingizi kabla ya kumtoa kwenye nyumba hiyo ya kupelekwa kwenye maskani ya wanyama.

Tiger ni aina ya Chui wanaopatikana Kusini na Kusini Mashariki mwa Asia na Mashariki ya mbali ya Urusi.

Ni wanyama ambao wapo katika hatari ya kupotea. Inakadiriwa kuwa wamebaki 4,000 tu mwituni.

**BBC**

## UTAFITI

# Jinsi pombe inavyoathiri DNA na kuongeza hamu ya kunywa zaidi

UTAFITI unaonyesha kuwa imani za zamani kwamba glasi moja ya mvinyo wakati wa chakula ni muhimu ni potofu.

Kwamba unywaji wa pombe kupita kiasi si mzuri kwa afya yako, ni kitu kilichothibitishwa kisayansi miaka kadhaa iliyopita.

Lakini kulikuwa na nadharia kwamba glasi moja ya mvinyo ni muhimu wakati wa chakula, lakini utafiti wa sasa unaonyesha kwamba hilo si kweli.

Matokeo haya yanazidi kubainisha kwamba athari za unywaji wa pombe zinazidi kujulikana.

**ATHARI CHEMBECHEMBE ZA DNA**

Na ndiyo maana kundi moja la wanasayansi kutoka Chuo Kikuu cha Rutgers nchini Marekani, pamoja na watafiti kutoka Chuo cha Yale nchini humo, wamegundua kwamba unywaji wa pombe unaweza kuathiri chembechembe za mtu za DNA na kumfanya ahisi anataka kukibugia kinywaji hicho zaidi.

Aidha, wengi pia wanabainisha kwamba kinywaji kimoja kina athari mbaya kwa afya zetu.

**HAMU YA KUNYWA ZAIDI**

Hadi kufikia hapo kundi hilo la watafiti liliamua kuangazia uchanganuzi wake katika jeni mbili zinazohusiana na udhibiti wa tabia wakati mtu anapokuwa chini ya shinikizo la pombe.

Moja ni ile ya PER2 inayoshawishi maisha ya miili yetu na nyingine ni ya POMC, ambayo inadhibiti utaratibu wetu wa kukabiliana na dhiki.

Ukilinganisha wanywaji wa wastani na wale wanaobugia pombe kwa wingi, wanasayansi wamegundua kwamba jeni za watu wanaokunywa pombe kwa wingi hubadilika.

Kwa wale wanaobugia kwa wingi, jeni zao hutoa protini polepole na hupata hamu ya kunywa wakati wanapokumbwa na matatizo.

Na kwa wale wanaopenda kunywa ili kukabiliana na matatizo, ni muhimu wakatambua kwamba mabadiliko ya jeni huongezeka kutokana na kinywaji zaidi.

Unapobugia pombe sana unazidi kuharibu jeni, hatua inayotufanya kuwa na hamu ya kunywa pombe zaidi na zaidi.

"Tumegudua kwamba watu wanaokunywa pombe nyingi wanabadilisha chembechembe zao za DNA katika njia inayowafanya kutaka kunywa zaidi," anasema Profesa Dipak Sarkar, mwanzilishi wa utafiti huo unaongozwa na Chuo Kikuu cha Rutgers.

"Hii inaweza kusaidia kuthibitisha kwa nini pombe ina mvuto mkubwa," anaongeza.

Watafiti wanatumaini kwamba ugunduzi wao utatoa fursa ya kutambua viashiria vinavyoweza kupimwa kama vile protini au jeni zilizobadilishwa, kutabiri hatari ya mtu anayekuwa na unywaji wa kiwango cha juu na namna atavyolindwa asiweze kunywa zaidi.

**BBC**

## KCMC yaleta nuru wagonjwa wa saratani

**Inatoka Uk.17**

"Hatua hii tunaichukua kutokana na wagonjwa wa saratani kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo jijini Dar es Salaam," anasema.

Dk. Masenga anasema jengo hilo linalotarajia kugharimu zaidi ya Sh. Bilioni 5 linatarajiwa kuwa na vitanda 60 kwa ajili ya wagonjwa hao.

"Takwimu zetu zinaonyesha kuwa wagonjwa wa Saratani wamekuwa wakiongezeka ambapo mwaka 2016 hadi 2018 kulikuwa na jumla ya wagonjwa 9,312, huku idadi ya wagonjwa wapya ikiwa ni 1,445 hadi kufikia hivi sasa,"anasema .

Anabainisha kwamba mwaka 2016 katika harambee maalumu iliyohusisha wananchi kwa ajili ya kujenga wodi hiyo, jumla ya shilingi milioni 230 zilikusanywa.

Aidha, anafafanua kuwa tayari wameshatafuta wafadhili kutoka nchi mbalimbali watakaosaidia kukamilisha ujenzi wa jengo hilo.

"Wagonjwa wa saratani wamekuwa wakipata changamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya mionzi katika Hospitali ya Ocean Road jijini Dar es Salaam, lakini pia wapo wanaoshindwa kwenda kutokana na hali ngumu ya kifedha," anasema na kuongeza:

"Sisi katika Hospitali ya KCMC tumeona haja ya kutoa huduma hiyo ambapo tumeshatengeneza bajeti na michoro ya jengo na tumeshaiwasilisha Serikalini... Katika bajeti ya mwaka 2018/19 Serikali imetenga kiasi cha Sh. Bilioni moja kwa ajili ya kuanza ujenzi huo."

Mkurugenzi anasema kuwa mpaka sasa wameshapata wafadhili watakaonunua mashine maalum ya mionzi na kwamba wanachosubiri ni kukamilika kwa jengo hilo ili waweze kuleta mashine, huduma zianze mara moja.

"Serikali ya Jamhuri wa Mungano wa Tanzania imetenga Sh. Bilioni moja kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kununua dawa za ugonjwa wa saratani kwa hospitali yetu ya KCMC ambapo wagonjwa wamekuwa wakipewa dawa hizo bure," anasema.

**KINA MAMA**

Baadhi ya wanawake waliohudhuria kilele cha siku hiyo wameiasa serikali ihakikishe inapitisha ajenda ya utoaji elimu kuanzia ngazi ya kijiji, kata hadi wilayani ili kujenga uelewa juu ya saratani hiyo inayoathiri wanawake wengi.

Suzani Kavishe ni mmoja wa kina mama hao anasema mbali na wananchi kukosa elimu ya kutosha juu ya magonjwa ya saratani lakini pia kuna dhana potofu ya kutokuwapo kwa tiba ya saratani.

"Lakini pia tatizo jingine ni la uchumi duni miongoni mwa wananchi unaowakwamisha kina mama wengi kufika katika Hospitali ya Rufani ya KCMC kufanya vipimo vya awali," anasema.



Utafiti unaonyesha kwamba unywaji pombe kama huu unaathiri chembechembe za mtu za DNA na kumfanya ahisi anataka kunywa zaidi. **PICHA: VODACOM**

ELIMU

**NA HAPPY SEVERINE, BARIADI**

# Wazazi walivyo chanzo cha mimba za utotoni Bariadi

- Ni kwa kutokidhi mahitaji ya msingi kwa watoto wa kike
- Baadhi walaumiwa kuwageuza watoto vitega uchumi

SALOME Masunga (16) mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mahaha, Bariadi, Mkoa wa Simiyu ana ujumbe mzito kwa wazazi wa watoto wa kike.

"Kama wazazi na jamii wangekuwa wanatutimizia mahitaji yetu ya msingi sisi watoto wa kike, ni dhahiri baadhi ya changamoto zinazotishia kuvunja ndoto zetu za kielimu zisingekuwa zinatupata," anasimulia.

Salome anasema kuwa jukumu kubwa na la msingi katika kuhakikisha ustawi wa mtoto wa kike ni la kuzingatiwa kwa mahitaji yake ya msingi, usaidizi wa makuzi pamoja na malezi kutoka kwa wazazi, mambo ambayo baadhi ya walezi wilayani Bariadi hawayafanyi.

Anabainisha, tangu aanze kujifahamu amekuwa akikutana na changamoto na vishawishi vingi na wenzake walio katika shule mbalimbali Wilayani humo, kutokana na kukosa usaidizi wa karibu na usimamizi kutoka kwa wazazi wao.

Kwa mujibu wa maelezo yake, masuala ya msingi ya mtoto wa kike ni lazima yaguse mahitaji muhimu kwao ili kuwaepusha dhidi ya makundi mabaya yanayoweza kukwamisha kuzifikia ndoto zao za kitaaluma.

"Mzazi anayejua umuhimu wa mwanaye na kutambua jukumu lake kwa mtoto wake...lazima atimize wajibu wake bila kulazimishwa wala kupigiwa kelele, lakini kwa baadhi yetu imekuwa tofauti kwani wazazi wetu hawahangaiki wala kujishughulisha na mahitaji yetu muhimu," anasema.

Anaongeza kuwa wazazi wengi wilayani Bariadi hawajajua au kuelewa majukumu yao kwa watoto wao wa kike, ukitofautisha wa wale wa kiume.

"Wazazi wamekuwa wazembe kutimiza majukumu yao kwa watoto wao wa kike, hali ambayo imekuwa ikinifanya kujiuliza mara kwa mara kwamba je ni kutokana na hali ngumu ya maisha au ni hulka tu ya wazazi kukwepa majukumu yao?" anauliza na kuongeza:

"Mwisho wa yote sisi wa watoto wa kike tunajikuta tukitumbukia katika dimbwi la mahusiano ya kimapenzi ili tuweze kujikimu."

Anabainisha kuwa yeye binafsi amekuwa akikosa mahitaji ya msingi kutoka kwa wazazi, kwamba hata anapomshirikisha mama yake kwa mahitaji kama nguo za ndani na taulo za kike, siku zote huishia kuambiwa hana pesa za kumnunulia mahitaji hayo.

"Na kibaya zaidi, mama husema kwamba hata yeye mwenyewe hawezi kumudu kujikamilishia mahitaji yake," anasema.

**MWONGOZO WA MALEZI**

Salome anasema wasichana wengi katika wilaya hiyo wamekuwa wakiishi na kukua bila kupata malezi stahiki na mwongozo thabiti wa mabadiliko ya miili yao.

Anabainisha kwamba upungufu huo ndio kwa kiasi kikubwa umekuwa ukiwaathiri na kujikuta wakidondokea mikononi mwa wanaume wadanganyifu na kuishia kupata mimba zisizotarajiwa.

Anafafanua kwamba sasa akiwa na umri wa miaka 16, hajawahi kupata mafunzo yoyote yanayohusu mabadiliko ya mwili kutoka kwa mzazi wake na badala yake alijifunza masuala hayo kutoka kwa wenzake.

**IRENE PASCHAL**

Kwa upande wake Irene Pachal (12) mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kidinda, anasema amekuwa akishuhudia wenzake



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bariadi waliobainisha changamoto ya kutopata huduma zao za msingi kutoka kwa wazazi wao. **PICHA ZOTE: HAPPY SEVERINE**

> "Endapo wazazi wangekuwa wanazungumza na mabinti na hata vijana wa kiume wangetambua na kujua umuhimu wa kuhudumia watoto katika masuala ya msingi na hivyo kuwanusuru kutoka kwenye vishawishi vinavyosababisha ndoa za utotoni pamoja na mimba zisizotarajiwa."



Irene Paschal, mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kidinda, anayekiri wanafunzi wengi wa kike kutopatiwa mahitaji yao ya msingi na hivyo kujikuta wakidondokea katika janga la mimba zisizotarajiwa.

wakilalamika kutopata mahitaji yao kutoka kwa wazazi wao.

"Wazazi wengi hawana tabia na mazoea ya kuwahudumia watoto wao na badala yake wanawageuza kuwa kitega uchumi," anasema.

Anafafanua kwamba kuna tabia isiyofaa na isiyozoeleka kutoka kwa wazazi wa Wilaya ya Bariadi ya kukwepa majukumu ya kuwahudumia watoto wao na badala yake hutaka kuwageuza vitega uchumi cha familia kwa kuwafanyisha biashara na vibarua vidogo vidogo.

Irene anasema, ingawa yeye anapata mahitaji yake mara moja moja kutoka kwa mama yake, lakini anaona jinsi wenzake wanavyonyemelewa na hatari kwa kukosa mahitaji ya msingi hali inayowalazimu 'kujishughulisha' ili wajikimu katika mahitaji yao.

**WAZAZI**

Bahati Sonda ni mkazi wa Bariadi. Anakiri kuwa kuna tatizo la baadhi ya wazazi kutohudumia watoto wao wa jinsia zote kwa ujumla kwa mahitaji yao ya msingi.

Anasema familia nyingi wilayani Bariadi hazina kipato kikubwa hali inayowalazimu wazazi kuwatumia watoto wao kwa nyakati zingine kama kitega uchumi kwa kuwaingiza kwenye biashara ndogondogo na vibarua bila kujua madhara yanayowapata watoto hao.

"Wazazi wengi hapa Bariadi wanakwepa majukumu ya kuhudumia watoto wao na wamewageuza kuwa vitega uchumi vya kuwatafutia pesa za kuhudumia familia, hali inayowanyima watoto wao haki za msingi," anasema.

Sonda anabainisha kuwa karibu asilimia 70 hadi 80 ya wanafunzi wengi wenye umri kati ya miaka 7 na 13 wamekuwa wakifanyishwa kazi na kunyimwa mahitaji yao ya msingi huku fedha wanazozipata katika biashara ndogondogo wazifanyazo katika magulio na minada zikitumika kulisha familia zao.

Anasema asilimia kubwa ya wanafunzi wanaotumika kufanya biashara katika magulio na minada wilayani humo ni wanafunzi wa kike wakiwa kati ya darasa la kwanza hadi la sita.

Sonda anafafanua kwamba kwa muda mwingi watoto hao wanalazimika kufanya biashara kama ya kuuza karanga, mboga mboga, kuosha utumbo wa mifugo machinjioni ama kuajiriwa kwenye migahawa na vilabu vya pombe.

"Sasa hali hiyo inawakosesha haki, mahitaji yao ya msingi na kuwasukuma katika mahusiano na wanaume na hatimaye wakishakubebeshwa mimba hutelekezwa," anasema.

**MATHIAS**

Costantine Mathias ni mkazi mwingine wa Bariadi, akiwa baba wa watoto wawili.

Aidha, Mathias ni mtetezi wa haki za watoto Bariadi ambaye anasema suala la wazazi wilayani humo kutohudumia watoto wao linagusa watoto wa jinsia zote.

Anafafanua kwamba suala hilo ni gumu kwa kuwa hata wazazi na hasa akina mama historia, wakati wanakua nao hawakupata haki hizo, hivyo hawaoni kuwa ni tatizo.

Hata hivyo, Mathias anasema kuwa baadhi ya familia zina hali duni ya kiuchumi kwani hata ndani ya familia kuna wazazi wanaoshindwa kabisa kumudu mahitaji ya msingi ya familia.

Anataja sababu nyingine kuwa ni wazazi wengi, hasa kina mama, kutokuwa na tabia ya kuzungumza na watoto wao juu ya afya ya uzazi, makuzi na malezi kwa kuwa mambo hayo yanachukuliwa kuwa yasiyofaa kutajwatajwa.

"Endapo wazazi wangekuwa wanazungumza na mabinti na hata vijana wa kiume wangetambua na kujua umuhimu wa kuhudumia watoto katika masuala ya msingi na hivyo kuwanusuru kutoka kwenye vishawishi vinavyosababisha ndoa za utotoni pamoja na mimba zisizotarajiwa.

**NDOA ZA MITAALA**

Kwa upande wake, Neema Elias ambaye pia ni mkazi wa Bariadi, anasema ndoa za mitaala (wake wengi) zilizoshamiri wilayani Bariadi ndizo chanzo cha wazazi wengi kutotekeleza majukumu yao ya kuhudumia watoto na familia zao kwa ujumla.

Anasema mitaala husababisha wanaume kushindwa kukidhi mahitaji ya familia zao kutokana na idadi kubwa ya jamaa wanaohitaji kuhudumiwa, hali inayosababisha watoto kugeuka kuwa wasimamizi wa familia.



WADAU

**SABATO KASIKA**

# MAMLAKA ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya imebaini kuwapo pipi hatari zinazodaiwa kuchanganywa na dawa za kulevya na kusambazwa shuleni kuuzia wanafunzi.

Wadau wanasemaje?



**ERESWIDA MOSHI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

INANIWIA vigumu kuamini mara moja kuhusu kuwapo kwa pipi za aina hiyo zinazodaiwa kuuzwa katika maeneo ya shule za awali hadi sekondari.

Suala hili linaweza kuwa ni uzushi kwani tangu miaka ya 1990 tukiwa tunasoma shule ya msingi tulikuwa tunaambiwa hivyo.

Pengine dawa za kulevya zimekuwa zikifungashwa kama pipi kama mbinu za kuficha dawa hizo.

Au pia zaweza kuwa mbinu za wazazi na walezi za kutaka kuwadhibiti watoto wao wasile pipi ovyo.

Binafsi sidhani kwamba kuna pipi za aina hiyo kwenye maeneo ya shule.

Ninasema hivyo nikiwa na sababu hii, kwamba Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ipo na ingeshatoa taarifa.

Hivyo ni vyema tusubirie TFDA watuambie ingawa pia kuna haja ya kila mmoja wetu kuwa makini na hali hiyo, kwasababu kama zitakuwepo, basi siyo kwamba zitakuwa zinauzwa shuleni tu bali hata mitaani.

Lakini kama nilivyosema jambo kubwa ni TFDA kufuatilia na kutoa jibu kamili ili kuondoa utata huu ambao nilianza kuusikia tangu miaka ya 1990 nikiwa shule ya msingi na sasa umejirudia tena.



**MWASITI RAJABU (MKAZI WA MJINI MOROGORO)**

HII sasa ni hatari zaidi, hivyo ipo haja kwa jamii kuchukua tahadhari juu ya pipi zenye dawa hizo, ambazo zinadaiwa kuuzwa katika maeneo ya shule mbalimbali kama ambavyo imeelezwa na mamlaka husika ya kudhibiti dawa hizo.

Waswahili wana msemo wao kwamba lisemwalo lipo na kama halipo, basi linakuja.


Binafsi niliwahi kusikia mbunge mmoja akilalamikia hali hii kwamba zimeingizwa nchini pipi zenye dawa za kulevya na zinauzwa shuleni.

Sikuamini hilo, lakini sasa nimeanza kuamini kutokana na kauli ya mamlaka husika kutoa tahadhari.

Ndio maana nikasema jamii ichukue tahadhari, kwani wazazi wamekuwa wakiwapa watoto wao pesa za kutumia wawapo shuleni na huko wananunua chochote wanachotaka.

Kwa hali hiyo kuna uwezekano mkubwa wameshatumia pipi hizo, kutokana na ukweli kwamba watoto wengi wanapenda pipi.

Wito wangu zaidi ni kwamba jamii isipuuzie kile ambacho kimesemwa kwani nchi hii vinaingia vitu vingi vikiwamo hata visivyofaa na tunakuja kuambiwa kuwa kitu fulani hakifai wakati tumeshaanza kukitumia.



**STEVEN MAJURA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

JAMBO hili linaweza kuwa na ukweli ndani yake. Sidhani kwamba Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya imekurupuka tu.

Itakuwa imefuatilia na kubaini kuwapo kwa pipi hizo hatari ambazo inasemekana zinachanganywa na dawa za kulevya.

Kwa hiyo kinachotakiwa ni wazazi na walezi kuwa makini sana kwani biashara hii kubwa duniani ina mbinu nyingi, ambazo zimekuwa zikitumiwa na wauzaji ili kujipatia fedha haramu.

Kwa maana hiyo taarifa hizi zisichukuliwe kimzaa tu bali kila chombo kinachohusika katika uchunguzi kifanye kazi.

Kwa upande wa wazazi na walezi ni muhimu kuwa makini na kuacha mtindo wa kuwanunulia watoto pipi ovyo kwa kudhani kwamba wanawapenda na kumbe wanawaharibu. Umakini ni wa msingi sana katika kila jambo.

Tumepewa taarifa, kinachofuata ni sisi kuchukua hatua, ambazo zitawafanya watoto au wanafunzi kwa ujumla wawe salama wawapo shuleni na nyumbani, wasile vyakula au pipi ambazo zinadaiwa kuwekwa dawa za kulevya.



**DEOGRATIUS DAVID (MKAZI WA MJINI MOROGORO)**

KWA hali hii ninaona ni bora pipi za aina zote zisiuzwe ili ufanyike uchunguzi wa kubaini zile zinazodaiwa kuwekwa dawa za kulevya ndipo wauzaji waendelee kufanya biashara hiyo.

Sidhani kama pipi wanazosema kuwa zimewekewa dawa za kulevya zinajulikana, ndio maana nikasema ni bora kuzuia kuuza pipi zote kwanza hadi zitakapobainika.

Vinginevyo watoto ambao ni wapenzi wa pipi wataendelea kupewa dawa za kulevya bila wao kujua.

Taarifa ya kwamba Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na taasisi nyingine zisizo za kiserikali, wamefanya kampeni kwenye baadhi ya shule jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kuwaelimisha wanafunzi athari za dawa hizo, kwa lengo la kuwaepusha na madhara hayo ni njema na ninawaombea waendelee kufanya hivyo.

Aidha, hatua yao ya kutaka kuanzisha msako maalum wa kuwakamata wahusika ni nzuri.

Hata hivyo, kikubwa ninachokiona ni kuzuia kwanza kila aina ya pipi hadi hapo zilizo na dawa zitapobainika na kuondolewa sokoni ndipo zile zisizo na madhara ziendelee kuuzwa katika maeneo yote ikiwamo shuleni.



**OTMARI NGAKWIRA (MWALIMU MKUU S/M UNUBINI DAR ES SALAAM)**

USHAURI wangu kwenye suala hili ni TFDA kupita katika maduka yote na kuchukua kila aina ya pipi na kwenda kuzipima ili kubaini zile, ambazo inasemekana zina dawa za kulevya, kwani huko ndiko wauzaji wanakozitoa.

Wakifanya hivyo wanaweza kubaini kirahisi kwamba kuna pipi za aina hiyo au hakuna.

Pia wanaweza kwenda katika shule na kutumia walimu kupata pipi kwa ajili ya kuzifanyia ukaguzi, kwasababu inawezekana wakawafuata wauzaji ikawa vigumu kuzipata, lakini wakitumia walimu ni rahisi.

Kiukweli ni kwamba kama kuna pipi za aina hiyo madhara yake ni makubwa kwa baadaye, hivyo biashara hiyo idhibitiwe haraka na pia ulaji wa pipi unaharibu meno ingawa watoto wanazipenda.

Umefika wakati sasa wazazi kuangalia vitu vya kuwazoeza watoto wao, kwani pipi zimekuwa na nafasi kubwa kana kwamba ni nzuri na watoto wanazipenda sana, lakini kimsingi madhara yake ni makubwa kuanzia kuoza meno na hata hilo tukio jipya la kuchanganya na dawa za kulevya ambalo ni baya zaidi.



# Ubakaji watoto waibua hofu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameingiwa na hofu baada ya kuibuka wimbi la ubakaji wa watoto unaotekelezwa na watu wasiojulikana huku vitendo hivyo vikihusishwa na imani za kishirikina.

Inadaiwa kuwa mpaka sasa watoto wanne wamenusurika kubakwa huku wabakaji hao wakifanikiwa kumbaka mtoto mmoja ambaye ni mwanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Mapinduzi wakati akitoka shuleni jioni.

Walieleza hofu ya kuibuka kwa wimbi hilo jana kwenye mkutano wa hadhara ambao ulifanyika katika Kitongoji cha Mapinduzi na kuhudhuriwa na makundi mbalimbali wakiwemo viongozi wa dini, viongozi wa mila, watetezi wa Haki za binaadamu na Jeshi la Polisi.

**Mmoja wa watoto hao alifanikiwa kukimbia na kwenda kutoa taarifa kanisani ndipo watu wakatoka kwenda kuangalia lakini mbakaji huyo akatimua mbio na kutokomea kusikojulikana.**

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mapinduzi, Tukubagha Mnyanya, alisema matukio hayo yalianza kusikika Februari 14 mwaka huu ambapo binti wa darasa la saba alibakwa na watu wasiojulikana wakati anatoka shuleni jioni.

Alisema baada ya tukio hilo wakati wanaendelea kutafakari na kuchukua hatua za kumsaidia mtoto huyo, mtoto mwingine wa miaka mitatu, alichukuliwa na mtu asiyejulikana na kuingia naye kwenye pagara kisha wakati anataka kubaka watu wakamshtukia na akakimbia kwa kuruka ukuta.

"Tumeona tuwahi kupambana na matukio haya maana yanatishia usalama wa watoto wetu, matukio haya yanadaiwa kuwa yanatokana na imani za kishirikina, wahusika wanataka utajiri, sasa tunaomba mungu hawa watu wapatikane," alisema Mnyanya.

Mchungaji wa Kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT), Vumilia Mwasenga, alieleza kuwa Februali 17 mwaka huu walipokuwa kanisani wanaendelea na ibada, mtu mmoja alitaka kuwabaka watoto watatu wenye kati ya miaka 12 na 13.

Alisema watoto hao akiwemo wa kwake walikuwa wanachuma mapera lakini akajitokeza mwanamume mmoja ambaye matunda sio yake akawaamuru washuke haraka akidai matunda ni ya kwake na akawachukua akaenda nao kwenye kichaka.

Alisema mmoja wa watoto hao alifanikiwa kukimbia na kwenda kutoa taarifa kanisani ndipo watu wakatoka kwenda kuangalia lakini mbakaji huyo akatimua mbio na kutokomea kusikojulikana.

Kwa upande wake Diwani wa Kata hiyo, Kisman Mwangomale, alisema katika Kitongoji cha Mapinduzi matukio ya ajabu yamekuwa yakitokea sana kwa madai kuwa kuna watu wamekuwa wakiuawa na kufichwa ndani.

Alisema pia katika maeneo ya Mapelele kuna baadhi ya watoto walikuwa wanauawa na kutupwa kwenye mapagala hali ambayo iliyopelekea kuzua hofu na watu wakawa wanaishi na watoto wao kwa hofu.

Alisema mbali na matukio hayo ya mauaji lakini pia watoto wamekuwa wakipotea mara kwa mara na kuwasababishia watu kuingiwa na hofu juu ya usalama wa watoto wao.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Mbeya, Debora Hokololo, alisema Jeshi la Polisi litafanya kila namna kuhakikisha wahusika wa matukio hayo wanakamatwa na kushughulikiwa.

Aliwataka wazazi na walezi kuimarisha ulinzi wa watoto wao kwa kuhakikisha hawawaachi peke yao majumbani ama kuwatuma peke yao kwenda madukani nyakati za usiku.

## Ukuta kuzunguka vituo vyote yatima

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAMANDA wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, ameagiza kujengwa kwa ukuta imara kuzunguka vituo vyote vya watoto yatima katika kila Halmashauri za Wilaya mkoani humo ikiwahakikishia usalama watoto hao.

Akizungumza juzi alipotembelea Kituo cha watoto yatima cha Nuru Orphan Center kilichopo katika Kata ya Uyole, Kamanda Matei alisema ukuta huo ambao utajengwa katika kila kituo cha watoto yatima, utasaidia kuwaepusha na wimbi la vitendo vya mauaji, ubakaji na ulawiti ambavyo tayari vimeripotiwa katika mkoa jirani wa Njombe.

"Nimeona hali halisi ya kituo hiki cha nuru wengi wanaolelewa hapa ni watoto wadogo na ukiangalia mkoa jirani wa njombe vitendo vya mauaji, ubakaji na ulawiti vimeshamiri, hivyo mkoa tumejipanga kukabiliana na jambo hilo na tumeanza na kuhamasisha ujenzi wa ukuta kwenye vituo vya yatima," alisema Matei.

Kamanda Matei alitoa rai kwa wananchi kuachana na imani potofu za kujipatia utajiri kwa kuwauwa watoto wadogo alisema Jeshi la Polisi limejipanga kukabiliana na vitendo hivyo.

Msimamizi wa kituo hicho, Jackson Sihavago mbali na kupokea agizo la ujenzi wa ukuta pia aliwaomba wadau kusaidia kufunga kamera ili kubaini matukio yeyote yanayoweza kutokea.

Alisema kamera hizo ambazo zitafungwa maeneo ya kituo hicho zitasaidia kufahamu matukio mbalimbali ya uhalifu ambayo yatafanywa.

Miongoni mwa wadau mkoani humo, Fredy Pole, alisema mbali na ujenzi wa ukuta kwenye vituo vya watoto yatima, lakini jamii pia iwakumbuke kwa kuwapatia vyakula, malazi na mavazi.



Mafundi wakiendelea na awamu ya kwanza ya upanuzi wa Barabara ya Morogoro inayoanzia Kimara mwisho hadi Kibaha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Waziri Jafo atoa angalizo rushwa shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jafo, ameutahadharisha uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya akiutaka kuepuka vitendo vya rushwa wakati wa udahili wa wanafunzi katika Shule za Msingi zenye mchepuo wa Kiingereza.

Alitoa tahadhari hiyo juzi alipofanya ziara ya kushtukiza jijini Mbeya na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo ikiwemo shule ya Msingi Azimio ambayo ni ya mchepuo wa Kiingereza na imeanza kupokea wanafunzi mwaka huu.

Waziri Jafo alisema shule ya Msingi Azimio imejengwa kwa ubora unaotakiwa na ameridhishwa nayo, lakini akaonya kuwa endapo kutatokea vitendo vya rushwa katika udahili ubora huo ukawa hauna maana.

Pia, aliwatahadharisha kuepuka kufanya upendeleo kwa watoto wa viongozi pekee huku watoto wa wananchi wa kawaida wakitengwa kwa madai kuwa vitendo hivyo havitakubalika na kiongozi yeyote.

"Isije ikatokea mtu yeyote akafanya vitendo ambavyo vinaashiria rushwa, mtu anataka mpaka apewe chochote ili akubali kumpokea mtoto katika shule hii hapana, mtoto yeyote atakayefikia viwango mnavyovihitaji katika shule hii mpokeeni," alisema Waziri Jafo. Alisisitiza kuwa vitendo vya rushwa vikiingia kwenye shule hiyo pamoja na shule nyingine yoyote ni ikathibitika, wahusika lazima watachukuliwa hatua za kisheria.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, James Kasusura, alimweleza Waziri Jafo kuwa ukarabati wa Shule hiyo umefanyika kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri hiyo.

Kasusura alisema ukarabati huo umefanywa na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kambi ya Itende jijini humo ndani ya miezi miwili pekee na kukamilika kwa viwango ambavyo walikubaliana.

Alisema mradi huo umekamilika haraka kutokana na kuwatumia vijana hao na kwamba wametumia takribani shilingi milioni 400 huku akidai kuwa wangewatumia wakandarasi ingechukua muda mrefu zaidi na hata gharama ingekuwa kubwa.

"Yale madarasa mawili yalikamilika kwa muda wa miezi sita kwa kujengwa na makandarasi wa kawaida lakini hii shule nzima imekarabatiwa kwa miezi miwili kwa kuwatumia wapiganaji wetu wa JKT," alisema Kasusura.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Azimio, Rebecca Tindwa, alisema mpaka sasa shule hiyo imeshapokea wanafunzi 825 ambao wanaendelea na masomo wakiwemo waliohamishwa kutoka katika shule mama ya Mkapa. Alisema wasichana wapo 425 na wavulana wapo 400 kuanzia darasa la awali mpaka la tatu huku akisisitiza kuwa miundombinu yote iko vizuri katika shule hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Katibu Tawala wa Wilaya, Hassan Mkwawa, alisema watahakikisha maelekezo yote ya uboreshaji wa shule hiyo yaliyotolewa na Waziri Jafo yanatekelezwa ipasavyo.





# Kitengo cha majeruhi wa ajali kuanzishwa BMH

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) imeanzisha kitengo maalum kwa ajili ya kuhudumia majeruhi wa ajali (Trauma care Unit), ili kuokoa maisha ya watu wanaopata ajali maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumzia kuhusu kuanzishwa kwa wodi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema serikali ya awamu ya tano iliingia makubaliano na serikali ya Israeli ya kuanzisha kitengo hicho.

Alisema hali hiyo inatokana na matukio yanayojitokeza kutokana na kuwa kwenye njia kuu ya kuelekea Dar es Salaam.

**Kwa hiyo kumekuwa na matukio mbalimbali ya ajali yanayotokea kwenye hii barabara, lakini hakukuwa na kitengo maalum kwa ajili ya kuhudumia majeruhi.**

"Kwa hiyo kumekuwa na matukio mbalimbali ya ajali yanayotokea kwenye hii barabara, lakini hakukuwa na kitengo maalum kwa ajili ya kuhudumia majeruhi," alisema.

Alifafanua kuwa serikali iliingia makubaliano hayo ili waletewe vifaa na wafundishe wataalamu wa hospitali hiyo kwa ajili ya kutoa huduma.

"Ninavyoongea tayari Waisraeli walishaleta vifaa na walikamilisha kufunga mwezi wa 12 mwaka jana vipo tayari kwa ajili ya kuanza kutumika," alisema.

Dk. Chandika alisema wameshafanya mawasiliano na wadau hao ambapo muda wowote kuanzia sasa timu ya walimu itakuja kwa ajili ya kufundisha wataalamu ili huduma zianze kutolewa.

"Tumejipanga kwa nyanja zote kuwa majeruhi watapata huduma hapa hapa Benjamin Mkapa kwa kuwa vipo vifaa vya kisasa kabisa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema vifaa hivyo vitaokoa maisha ya wananchi na watakapofika watapata huduma stahiki.

Alisema watu wengi wamekuwa wakipoteza maisha kwa kukosa huduma bora na kupunguza watu kutokumbwa na ulemavu.

"Baada ya wataalamu kumaliza watakabidhi kitengo kiwe chini yetu na wataendelea kutoa mafunzo kwa wataalamu wetu, na haya ni matunda kati ya Serikali ya Tanzania na Israeli," alisema.



Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Joseph Malongo (katikati), akikabidhi zawadi ya saa kwa Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Mazingira, Ester Makwaiya, ambaye amestaafu rasmi utumishi wa umma katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Mazingira, Prof. William Mwegoha. **PICHA: OMR**

# Waziri amtaja mwenye maombi leseni 700

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameagiza Tume ya Madini kufuta maombi ya leseni za watu na kampuni zote ambazo zimeshikilia leseni bila sababu za msingi ikiwamo maombi ya leseni zaidi ya 700 za kampuni ya Ntoku Limited.

Agizo hilo alilitoa jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuwaendeleza na kuwasaidia wachimbaji wadogo pamoja na kuimarisha utoaji na usimamizi wa leseni za madini nchini.

Alisema kuna baadhi ya watu na kampuni zimekuwa zikiomba leseni nyingi za utafiti na uchimbaji wakati hawana uwezo wa kuyafanyia kazi.

"Mfano Christopher Eliofo na kampuni yake ya Ntoku Limited wana maombi ya leseni zaidi ya 700 katika maeneo mbalimbali nchini na ameshindwa kulipia hata ada ya maombi," alisema.

Alieleza kuwa kitendo hicho kinawanyima haki watu wengine bila sababu za msingi na mtu huyo amekuwa akiingilia maeneo ya watu wengine na kusababisha migogoro isiyokuwa ya lazima.

"Naagiza Tume ya Madini kufuta maombi ya leseni za watu au kampuni zote ambazo zimeshikiliwa bila sababu na kuandaa utaratibu wa ukomo wa leseni kwa mtu au kampuni," alisema.

Biteko alisema kama kifungu cha kuweka kikomo hakijaainishwa kwenye Sheria ya Madini, tume hiyo ipeleke mapendekezo ili aweke kanuni zinazoonyesha ukomo wa leseni.

Alisema kwa mwaka huu wa fedha, wizara hiyo iliahidi kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2017.

"Tuliahidi kuwa tutafuta leseni zote zinazokiuka matakwa ya sheria hiyo ili kutoa nafasi kwa wawekezaji wengine wenye uwezo wa kuyaendeleza na maeneo mengi zaidi kutengwa kwa wachimbaji wadogo," alisema.

Aliongeza kuwa: "Ni bora tulaumiwe kwa kusimamia sheria."

Pamoja na hayo, Waziri Biteko alisema wizara hiyo inategemea kuanza kuzindua vituo vya umahiri na mfano mwezi ujao ambavyo vimegharimu zaidi ya Sh. bilioni 12.

# CWT yalalamikia walimu kufanya kazi wikiendi

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

CHAMA cha Walimu (CWT) Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, kimelalamikia walimu kufanyishwa kazi siku za mwisho wa wiki bila malipo wala chakula kinyume na kanuni na miongozo ya kazi.

Malalamiko hayo yalitolewa jana na Mwenyekiti wa CWT wilaya hiyo, Clement Mahemba, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wilayani hapo.

Mahemba alisema kwa mujibu wa sheria ya ajira na uhusiano kazini walimu hao wanafanyiwa kazi kinyume cha sheria.

Alisema utaratibu huo ambao umeandaliwa na ofisa elimu msingi wa wilaya hiyo, umekuwa ukinyanyasa walimu kutokana na kuwatumikisha siku za mapumziko ambazo ni Jumamosi na Jumapili.

Alisema pamoja na walimu hao kutumikishwa kazi katika siku za kwenda kufanya ibada, lakini pia katika mpango huo ambao afisa elimu huyo anauita kuwa ni vikao kazi, kumekuwa hakuna malipo yoyote wala chakula.

"Walimu wanafanyishwa kazi Jumamosi pamoja na Jumapili siku ambazo wengi wao wanatakiwa kufanya mapumziko kwa ajili ya kujiaanda Jumatatu kwenda kufundisha," alisema na kuongeza kuwa:

"Lakini walimu hawa wanatoka umbali mrefu, kuna walimu wanatoka kijiji cha Champumba kwenda Mlowa barabarani ni zaidi ya kilomita 80 kwenda kushiriki vikao kazi, hivyo kukosa muda wa kufanya maandalizi ya Jumatatu," alisema.

Mahemba aliongeza kuwa kitendo cha mwajiri kumwita mtumishi wake kazini siku za wikiendi anatakiwa kumlipa kama ambavyo sheria ya ajira na uhusiano kazini namba 6 ya mwaka 2004 kifungu cha 24(1)6 na 24(4) vinavyoelekeza.

"Ni lazima mwajiri azielewe hizi sheria na kwanini wawanyime walimu hata kwenda kufanya ibada au kwa sababu mkurugenzi ni Mwislamu pamoja na afisa elimu wake?" alihoji mwenyekiti huyo.

Akijibu malalamiko hayo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chamwino, Athumani Masasi, alisema anachofahamu yeye ni kuwa hakuna mwalimu aliyelazimishwa na kwamba wanafanya hivyo kwa utayari wao.

"Ninachokifahamu mimi mwandishi hawa walimu ni makubaliano yao, hivyo hakuna mwalimu yeyote ambaye amelazimishwa kufanya hivyo wanavyofanya sasa, lakini kama unataka kufahamu zaidi njoo ofisini," alisema Masasi.



## Wanaokwenda masomoni China wahimizwa maadili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi waliopata fursa ya masomo China, kulinda maadili, silka, utamaduni na heshima ya Zanzibar kwa kufanya juhudi katika masomo ili kufikia lengo la serikali.

Kauli hiyo aliitoa wakati wa hafla ya kukabidhi tiketi kwa wanafunzi 17 waliochaguliwa kujiunga na shahada ya udaktari wa wanyama na sayansi ya wanyama iliyofanyika ofisini kwake Mazizini.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kuendeleza heshima ya nchi yao, na kwa kufanya hivyo watamjengea matumaini makubwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, kutokana na jitihada anazozichukua kuwawezesha kwa vijana.

"Heshima iwe ndio dira yenu katika kuitangaza nchi yenu ya Tanzania ambayo imejaaliwa na mambo mengi ikiwamo amani na utulivu," alisema.

Alisema, mategemeo ya serikali ni kuona wanafunzi hao wanafanikiwa kufanya vizuri ili kuongeza idadi ya wataalamu wa mifugo nchini.

Hata hivyo, alieleza kuwa ni jambo la msingi kwa wanafunzi hao kuzingatia zaidi masomo yao na sio kwenda kufanya mambo yasiyofaa.

Waziri huyo alisema walioomba nafasi hizo ni wengi, hivyo wao wachache waliobahatika ni vyema kusoma kwa malengo kwa faida yao na taifa. Aliwashauri kuwahamasisha wanafunzi wenzao hasa wa kike kusoma kwa bidii ili nao waweze kupata fursa hizo.

Aidha, aliwasisitiza wanafunzi hao pia kuhakikisha wanarejesha mikopo wanayopatiwa pale watakapomaliza kusoma ili kuwapa fursa na wengine kusoma.

Naye mwanafunzi Hudhaima Mohammed Kheir, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alimpongeza Rais wa Zanzibar kwa juhudi anazozifanya kwa vijana kuhakikisha wanasoma na kuahidi kuwa watasoma kwa bidii ili kuja kuiendeleza nchi yao.

Wanafunzi hao wanatarajiwa kuondoka nchini Februari 27 wakiwamo wanawake 12 na wanaume watano kwenda China kwa miaka mitano.

# Shein: Kuimarika elimu kumeipa hadhi Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuimarika kwa huduma za elimu kumeipa Zanzibar hadhi.

Akizungumza baada ya kuzindua jengo la Shule ya Sekondari Kijini huko Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema hatua hiyo imetokana na kuimarika kwa huduma za elimu katika hatua za awali.

Alisema kwa sasa Zanzibar imekuwa na vyuo vikuu vyenye kutoa elimu sawa na nchi zingine, hali inayosababisha raia wa kigeni kufuata masomo mbalimbali Zanzibar.

**Lengo la serikali ni kuwaandaa wanafunzi ili kuwa na wataalamu katika fani tofauti, kwa lengo la kulisaidia taifa.**

Dk. Shein aliwataka wananchi kuunga mkono juhudi hizo za serikali kwa kuwahimiza watoto wao kufuatilia masomo yao ili kuleta mabadiliko na maendeleo.

Dk. Shein alisema mwaka 1948, Zanzibar ilikuwa na shule chache za msingi na sekondari, na kwamba Mkoa wa Kaskazini Unguja ulikuwa na Shule ya Mkwajuni pekee.

Alisema Wazanzibari wanyonge walishindwa kupata elimu, kwa kuwa ilikuwa ikitolewa kwa misingi ya matabaka na uwezo wa mtu.

Alieleza kuwa serikali inakamilisha ujenzi wa shule tisa za ghorofa katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba.

Alisema lengo la serikali ni kuwaandaa wanafunzi ili kuwa na wataalamu katika fani tofauti, kwa lengo la kulisaidia taifa.

Jengo hilo la shule limejengwa na mwekezaji kutoka kampuni ya "Andbeyond" iliyowekeza katika Hoteli ya Mnemba na limegharimu jumla ya shilingi milioni 148.

Naye Waziri wa Elimu, Riziki Pembe Juma, aliishukuru kampuni hiyo kwa misaada inayotoa kwa wananchi wa maeneo hayo, ikiwamo uimarishaji wa elimu.

Alisema misaada hiyo inakuja kutokana na mazingira bora yaliyowekwa na serikali kupitia sekta ya uwekezaji na kutoa fursa kwao ya kuisaidia jamii.

Aliwataka wazazi kutumia vyema fursa zinazotolewa na serikali na kushirikiana nayo ili kufanikisha dhana ya uimarishaji wa sekta ya elimu nchini.



Mjasiriamali akiandaa vitumbua kwa ajili ya wateja wake, katika eneo la Tazara Vetenari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sababu ongezeko maambukizi ya Virusi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUCHELEWA kwa wajawazito kuhudhuria kliniki kumechangia kuongezeka kwa maambukizi ya virusi vya Ukimwi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Hayo yameelezwa na mratibu wa huduma ya kuzuia maambukizi ya kwenda kwa mama na mtoto kutoka mradi shirikishi homa ya ini, kifua kikuu na Ukimwi, Khadija Abas, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mafunzo ya afya ya mama na mtoto na Ukimwi yaliyoandaliwa na Shirika la Utafiti wa Dawa Afrika (AMREF) kupitia mradi wa afya ya jamii yaliyofanyika mjini hapa.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2017 hadi 2018 watoto 24 walizaliwa Zanzibar walipata maambukizi ya VVU kutoka kwa mama zao wakiwa wajawazito.

Alisema utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya watoto wenye umri wa chini ya miaka 15 duniani wanaishi na VVU kupitia kwa mama zao wakati wa ujauzito, kujifungu ama hatua ya unyonyeshaji.

Alisema ili kupunguza uwezekano wa mjamzito kumwambukiza VVU mtoto, ni muhimu kupata huduma kwa usahihi na umakini, ikiwamo kupima damu.

Alieleza kuwa kuna changamoto katika kufanikisha kuondoa maambukizi

kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ikiwamo kinamama na watoto wao kuacha kutumia huduma kwa kutoroka katika hatua mbalimbali za huduma au kutohudhuria kabisa.

"Baadhi ya kinamama hao wanaokimbia kutumia dawa za kufubaza, wengine hukimbilia kwa waganga wa jadi na wengine hukimbia kutokana na unyanyapaa mkubwa kwa jamii," alisema.

Aidha, alieleza kuwa kuna kesi nyingi zinazojitokeza katika vituo vya upimaji VVU ambazo zinaonyesha kuwa kinamama wengi wanaopimwa hukutwa na maambukizi, lakini wenza wao hawana.

Mratibu huyo, aliwaomba wazazi ambao wanaishi na VVU kuharakisha kutumia dawa za kufubaza virusi (ARV) wanapobaini wamepata maambukizi pamoja na kuhakikisha wanawanyonyesha watoto wao kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuwakinga na maambukizi wakati wa unyonyeshaji.

Aliwasisitiza kuhakikisha wanajifungulia vituo vya afya kwa uzazi salama na mtoto kupatiwa dawa za kuzuia maambukizi mara tu anapozaliwa.

Msimamizi wa mradi wa afya kamilifu Zanzibar kutoka AMREF, Mohammed Hassan, alisema taasisi yao itahakikisha inasaidiana na serikali katika kuwajengea uwezo wataalamu wa afya za uzazi katika vituo vyake vya afya kwa lengo la kutoa huduma nzuri kwa wanajamii pamoja na kupunguza maambukizi mapya ya VVU kwa wajawazito na watoto.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 18 Feb**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 19 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 20 Feb**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 21 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 22 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 23 Feb**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Delirious
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 24 Feb**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 18 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Shamba shape up
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 19 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 20 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kipindi Maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 21 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Hatua
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Jungu Kuu
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Huduma ya kwanza rpt
18:30 Kipindi Maalum: Ewura
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 22 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi maalum: Tanesco
13:30 Kipindi Maalum rpt - Ewura
13:55 Habari za saa
14:00 Mapishi
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Uchumi na biashara
19:00 Kipindi maalum: TCRA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 23 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Hatua
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 24 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Green Light 2
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Kisasi cha utata
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


5 EATV
NIRVANA
LEO USIKU SAA 3:00

JUMANNE
11:00 DADAZ (live)
13:30 Kali Za Wana
14:00 Dakika10 Za Maangamizi
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 Nirvana
21:30 Wakilisha
22:00 Grace Na Asili Yangu
22:30 Bongo Hits
NIRVANA ni kipindi cha kisasa kinachoongelea mitindo, sanaa, urembo na staili za maisha. NIRVANA inawalenga wale wanao ongoza kuonyesha mitindo mipya kwenye jamii na wale wanaofuatilia

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise
88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

## Bomu la kutoa machozi laua Sudan

**KHARTOUM, Sudan**

MUUZAJI matunda raia wa Sudan, amefariki mjini Khartoum baada ya kuvuta hewa iliyotokana na kurushwa kwa bomu la kutoa machozi iliyotumiwa na maafisa wa usalama kuwatawanya waandamanaji.

Maafisa wa afya, na familia ya marehemu, wamesema mtu huyo mwenye umri wa miaka 62, mkazi wa Bhari, mtaa ulio kaskazini mwa Khartoum, alikufa akipata matibabu hospitalini.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo walieleza kuwa mabomu ya kutoa machozi walirushiwa waandamanaji waliokuwa wakiandamana barabarani, ambapo mtu huyo ambaye hakufahamika jina lake alifariki baada ya kuvuta hewa yake.

Maandamano nchini Sudan, yalianza Desemba 19, mwaka jana wakati serikali ilipopandisha bei ya mkate.

Tangu wakati huo, maandamano yameendelea na kumekuwapo mapambano kati ya polisi wa kuzuia ghasia na waandamanaji, lakini maandamano ya sasa yamegeuka na kuwa ya kumtaka Rais Omar Al-Bashir kuondoka madarakani.

Serikali ya Sudan inasema watu 31 wamekufa kufuatia maandamano hayo, lakini wachunguzi wa kimataifa wa haki za binadamu wanasema hadi sasa watu 51 wameuawa. ***VOA***

## Israeli yazuia msaada wa Wapalestina

**JERUSALEM, Israel**

ISRAEL imezuia msaada wa dola za Kimarekani milioni 138 iliyokuwa inapewa Palestina.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu fedha hizo zinahusiana na posho iliyotolewa mwaka 2018 na serikali ya Palestina kwa magaidi wanaozuiliwa jela, kwa familia zao na kwa wafungwa wa zamani.

Hata hivyo, viongozi wa Palestina wamepinga vikali hatua hiyo iliyochukuliwa na Israel.

Siku ya Jumapili Israeli ilitangaza nia yake ya kuzuia dola Milioni 138 (sawa na Euro milioni 122) ambazo wangelipwa Wapalestina. Serikali ya Israeli inalipa mara kwa mara malipo ya VAT kwa Mamlaka ya Palestina na ushuru wa forodha inayotoza kwenye bidhaa zilizoagizwa na Wapalestina.

Lakini mnamo Julai mwaka jana, Bunge la Israel lilipitisha sheria inayozuia malipo ya kiasi hicho cha posho kilichotolewa na serikali ya Palestina kwa wahusika wa mashambulizi dhidi ya Israel na familia zao. ***RFI***

# Waangalizi kimataifa kuingilia uchaguzi Nigeria

**LAGOS, Nigeria**

WAANGALIZI wa kimataifa katika uchaguzi mkuu uliosogezwa mbele nchini Nigeria wametoa wito kwa raia wa taifa hilo kuwa watulivu wakati maandalizi ya uchaguzi yakiendelea.

Uchaguzi huo ulipaswa kufanyika Februari 16 umesogezwa mbele hadi Februari 23 kutokana na mazingira mabaya ikiwamo hali mbaya ya hewa iliyosababisha kuchelewa kwa ndege zilizobeba vifaa, moto kwenye ofisi tatu za tume.

Uamuzi wa kuhairisha uchaguzi uliotangazwa saa tano kabla ya vituo vya kupiga kura kufunguliwa siku ya Jumamosi, na unatarajiwa kugharimu dola bilioni 2 za Kimarekani.

Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi Nigeria, Mahmood Yakubu alisema kuwa kuchelewa kwa uchaguzi huo hakuhusiani na ushawishi wa kisiasa kwa namna yeyote.

Alisema ni muhimu kuchelewesha uchaguzi huo kuipa tume nafasi ya kukabiliana na masuala muhimu na pia kusalia na hadhi katika uchaguzi.

Hata hivyo, Rais wa sasa Muhammadu Buhari na mpinzani wake Atiku Abubakar wameelezea kutoridhishwa kwao na hatua ya tume ya uchaguzi kusogeza mbele tarehe ya upigaji kura kwa madai ya kutokamiliaka kwa baadhi ya maandalizi muhimu.

Abubakar, alitoa wito kwa wananchi wa Nigeria kuwa watulivu na kujitokeza kupiga kura siku ya uchaguzi iliyotangazwa.

Naye, Mwenyekiti wa chama cha PDP, Uche Secondu, alisema kucheleweshwa kwa uchaguzi ni hatari kwa demokrasia, huku akimshutumu Rais Buhari kuendelea kubaki katika nafasi hiyo wakati Wanigeria wanataka aondoke madarakani.

Tangu kuairishwa kwa uchaguzi, wananchi wengi katika mitaa ya Nigeria wamekuwa na hasira na kulalamikia kuchelewa kwa uchaguzi huo.

Uchaguzi huo unajumuisha wagombea 73 waliosajiliwa katika uchaguzi wa urais, lakini kampeni zimegubikwa na Rais Muhammadu Buhari, mwenye umri wa miaka 76, na mpinzani wake mkuu, aliyekuwa makamu wa rais Atiku Abubakar, mwenye umri wa miaka 72.

Buhari anasema amejenga msingi madhubuti kwa ustawi, lakini mpinzani wake anasema Nigeria mambo hayaendi sawa. Wote wawili wanatoka eneo la kaskazini mwa nchi lenye idadi kubwa ya waislamu.

Wananchi wapatao milioni 84 waliosajiliwa kupiga kura wanatarajia kushiriki katika uchaguzi huo.

***BBC***




Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Mohammad Javad Zarif, akiwa kwenye mkutano wa usalama mjini Munich. **PICHA:ALLIANCE**

# Viongozi Israel, Iran washambuliana mkutanoni

**MUNICH, Ujerumani**

MKUTANO wa kimataifa uliohusu usalama uliofanyika mjini Munich, Kusini mwa Ujerumani, ulimalizika kwa majibizano makali kati ya Iran kwa upande mmoja na Marekani na Israel kwa upande mwingine.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Mohammad Javad Zarif, aliliambia jukwaa hilo la kimataifa kuhusu usalama ulimwenguni kwamba Israel na Marekani wanafanya matendo yanayovifanya vita vionekane jambo tukufu.

Akijibu tuhuma za nchi yake kujihusisha na mizozo kama ile ya Syria, Zarif alisema Iran iko Syria kwa kuwa ilialikwa rasmi na serikali ya Syria kwa lengo la kupambana na ugaidi, na si vinginevyo.

"Tupo Syria kwa mualiko wa serikali ya Syria kwa lengo moja tu la kupambana na ugaidi, hakuna sababu nyingine yoyote ya kuwako huko. Nadhani mara ya mwisho nilipoangalia sheria za kimataifa, nilikuta kuwa kuingilia anga la Lebanon na kulitumia kuipiga Syria ni kuvunja sheria za kimataifa na jumuiya ya kimataifa," alisema Zarif na kuongeza.

"Hata watu wa ulaya wanaoamini juu ya sheria za kimataifa kuwa msingi wa usalama duniani wanatulaumu sisi na sio Waisraeli kwa kuvunja sheria za kimataifa." Alisema.

Alipoulizwa na waandishi wa habari ikiwa alichokisema kinamaanisha kuwa kitisho cha vita na Israel ni kikubwa, Zarif alikiri kuwa ni kikubwa, na kusema kuwa ni kikubwa zaidi pale dunia ikiendelea kufumbia macho uvunjwaji mkubwa wa sheria za kimataifa.

Hapo awali, Saudi Arabia ambaye ni hasimu mkubwa wa Iran ilikataa kuhudhuria mkutano huo baada ya Waziri wa Mambo ya Nje, Adel bin Ahmed Al Jubeir kufuta ziara yake mjini Munich kwa kile kilichoelezewa kuwa ni sababu za kiratiba.

Hata Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu naye hakuhudhuria mkutano huo na badala yake jawabu la nchi yake kwa hotuba ya Zarif lilitolewa na Benny Gantz, mkuu wa zamani wa jeshi la Israel na mpinzani mkuu wa Netanyahu kwenye uchaguzi wa Aprili, ambaye aliendeleza vitisho dhidi ya Iran.

***DW***

# Wakazi Bonde Msimbazi kuhamishwa karibuni

Na Elizabeth Zaya

JIJI la Dar es Salaam linatarajia kuanza kuwahamisha wakazi waliojenga katika Bonde la Mto Msimbazi.

Akizungumza katika mkutano na wadau wa sekta binafsi na za serikali zinazoshughulika na masuala ya miundombinu ya usafirishaji, mawasiliano, Jeshi la Polisi na mazingira, Ofisa Mipango Miji wa Jiji la Dar es Salaam, Grace Mbena, alisema taratibu za kuwahamisha wakazi hao zimeshafanyika na kazi hiyo itaanza wakati wowote kuanzia sasa.

Alisema wakazi hao hawatalipwa fidia yoyote kwa sababu wamejenga katika mto huo kinyume cha sheria.

"Jiji la Dar es Salaam limejipanga kuimarisha miundombinu ya bonde la Mto Msimbazi kwa kujenga miundombinu upya na ili kukamilisha mkakati huo na limeandaa utaratibu wa kuwahamisha wananchi waliopo pembezoni ya mto huo. Mpango wa kuwaondoa umeshakamilika na kazi itaanza wakati wowote kuanzia sasa," alisema Mbena na kuongeza:

"Kwa mfano katika maeneo ya daraja la Selander na barabara ya Kawawa, ekari 142 zitatengwa na kujenga maegesho ya magari, viwanja vya michezo na bustani za miti na maua baada ya wananchi kuhamishwa. Katika mpango huu tunasubiri fungu kutoka Wizara ya Fedha, hata kituo cha mabasi cha mwendokasi kitahamishwa na lengo ni kuimarisha miundombinu."

Alisema tayari wamefanya tathmini na kuwatambua wanaoishi maeneo hatarishi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya B & F Global inayojishughulisha na ushauri wa uendelevu katika sekta ya miundombinu na mazingira, Bruno Kinyaga, alisema ili taifa lisonge mbele ni lazima kuwe na miundombinu imara ambayo itasaidia kuleta mapinduzi ya viwanda.

Ofisa kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Rashid Mtamila, alisema wataendelea kushauriana namna ya kupambana na majanga ili kuondoa athari za miundombinu za kimazingira.

Mtamila alitoa wito kwa wananchi kushirikiana na serikali katika kukabiliana na majanga.




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, baada ya kuweka jiwe la msingi la ufunguzi wa barabara za mtandao wenye urefu wa kilomita 6.1 za Karume, Boma Kinyeto, Double Road Junction (Semali Singida-Dodoma), wilayani Singida, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Singida jana. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa Singida, Dk. Rehema Nchimbi. **PICHA: OMR**

# Wanakijiji wampongeza JPM

Na Mwandishi Wetu, MOROGORO

WAKULIMA na wafugaji wa Wilaya ya Morogoro Kata ya Duthumi, wamempongeza Rais John Magufuli kwa agizo lake la kutaka wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi ndogo ndogo nchini wasibugudhiwe na badala yake waachiwe waendelee na shughuli zao za kilimo na ufugaji.

Maelfu ya wananchi hao kutoka kijiji cha Mbwande, waliandamana kumpongeza Rais Magufuli kwa uamuzi huo wakisema hatua hiyo itawafanya kupata maendeleo ya haraka.

Hivi karibuni, Rais Magufuli aliagiza mawaziri wa Kilimo, Ardhi na Tamisemi, kuwaacha wananchi wanaoishi katika baadhi ya maeneo ya hifadhi na mabonde kuendelee na shughuli zao za kilimo, ufugaji na nyinginezo.

Mkazi wa kijiji cha Mbwande, Juma Mbassa, alisema wanamshukuru Rais Magufuli kwa maelekezo yake na kuwapa fursa wanyonge kuendelea na shughuli zao za kilimo na ufugaji kwa maslahi ya vizazi vyao.

"Tunachukua fursa hii adhimu kumpongeza Rais wetu mpendwa kwa kuonyesha kuwapenda na kuwajali wakulima na wafugaji kwa sababu miaka yote tumekuwa tukiondolewa kwa nguvu na kusababisha hasara ya mali na vitu vingi kwa familia zetu, tunamshukuru sana," alisema.

Mkazi mwingine, Lucas Daandi, alisema kauli mbiu ya Rais Magufuli ya "Hapa Kazi Tu" kipindi cha kampeni anaitekeleza kwa vitendo kwa kutoa fursa kwa wanyonge kufanya kazi kwa bidii ili kujikwamua kwenye lindi la umaskini. Aliongeza kuwa wanamwomba Rais aweke mkazo ili viongozi wa ngazi ya mkoa na wilaya watekeleze agizo hilo na maelekezo ya Rais Magufuli kwa vitendo na kwamba wanakijiji hao wametoa ng'ombe watano kama zawadi kwa Rais Magufuli kwa agizo lake hilo.

## Bil.10/- zatengwa utafiti michikichi

Na Mwandishi Wetu, KIGOMA

SERIKALI imeeleza dhamira yake ya kukabiliana na uagizaji wa mafuta ya kula nje ya nchi kwa kuanzisha mashamba ya michikichi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mafuta na uimarishaji wa sekta ya kilimo cha mazao hayo kwa wananchi.

Tayari Wizara ya Kilimo imetenga zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kuendeleza zao hilo katika mkoa wa Kigoma na mingine nchini yenye uwezo wa kuzalisha michikichi katika mwaka ujao wa fedha.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, aliyasema hayo juzi 2019, wakati akieleza wizara yake ilivyojipanga kuimarisha kilimo cha michikichi wakati wa ziara ya kikazi ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mkoani Kigoma.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu tusingeweza kusubiri hadi mwezi wa saba kwa ajili ya kupitisha bajeti. Badala yake tumetumia mbinu zingine kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida (OC) kuanza kutekeleza azima ya serikali ya kuendeleza zao la michikichi na kumaliza tatizo la mafuta," alisema.

Mgumba alisema kuwa wizara imepeleka watumishi wawili mkoani Kigoma waliobobea katika utafiti wa michikichi katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI-Kihinga), huku wengine 10 wakiwa mbioni kuwasili tayari kwa kuanza kazi hiyo.

Pia alisema TARI-Kihinga si kituo kidogo tena badala yake kitakuwa kituo kikuu cha utafiti wa zao hilo nchini, huku vituo vingine vyote vya utafiti wa michikichi vikiwa chini ya Kihinga.

Mgumba alizipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Magereza kwa ushirikiano zinaouonyesha katika uimarishaji na uendelezaji wa kilimo cha michikichi.

"Kama unavyofahamu mchakato wa kuandaa miche ya michikichi unachukua zaidi ya mwaka mmoja na nusu kuanzia kuchavisha mpaka kuwa mche kwa ajili ya kupeleka kwa wakulima, hivyo ushirikiano huo tunaoupata ni utimilifu wa uratibu wa kazi hii," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

## MASHAMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo Kisongo Arusha jirani na Braebun School Kina upana wa 43,urefu 93 . Bei Milioni 40 kimepimwa. Maji, barabara na umeme vipo. Mawasiliano:-0755 907 520.

**VIWANJA VINAUZWA,** Kimoja kipo Ukonga Kitunda Sqm 5670 (Eka 1 na robo) Kingine kipo Tabata Liwiti Sqm 4565 (Eka 1). Bei Shs 220m @ 0719 619444 / 0782 574669.

**ENEO LINAUZWA,** Nauza eneo liko mpiji magoe yanapogeukia magari ya kutoka mbezi ni unatembea mita mita mia miambili hadi kwenye eneo ukubwa ni mita 20@40 bei nafuu kabisa simu no 0621607825

## NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

*Uza Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311*

---

Yetu Microfinance Bank PLC

**Wekeza nasi katika akaunti maalum upate faida kubwa.**

**Muda wa uwekezaji:** Miaka miwili

Kwa mwekezaji mwenye kiasi cha zaidi ya million 50, tafadhali piga simu 0762623062

**Unaweza kuwekeza kuanzia shilingi million moja kwa faida ya hadi 13%**

215048502

---

## CHETI KIMEPOTEA



**MALIWA MASUNGA MUHOJA** wa Kibara, Bunda. Anatangaza kupotelewa na Cheti cha Ualimu chenye **Index Number E0522-0264** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2013 katika Chuo cha Ualimu Kinampanda. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilicho karibu. Taarifa ya Polisi: **BND/RB/6141/2016**

215067002

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**Gedeon Rwezahura** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo; cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0148/0016** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 1994 katika shule ya Sekondari St. Mary's Seminary Rubya, Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0146/0511** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 1997 katika shule ya Sekondari St. Mary's Seminary Nyegezi, degree ya kwanza kilichotolewa na chuo cha Mt. Augustino – Mwanza mwaka 2015. Yeyote atakaevion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **MUL/RB/365/2019**

115067102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;33/2019**

**Ombi la THERESIA L.NGODOKI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu LETICIA LADISLAUS NGODOKI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 01/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 11/02/2019.

115068202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 32/2019**

**Mdai:............................ NEEMA EDSON**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa:........................... SYLVESTER MLOKA**

**Kwa: SYLVESTER MLOKA – BIGWA MOROGORO**

**Ombi la Mdai: ..........................NEEMA EDSON**

**Madai ya PESA TASLIM TSH. 2,000,000**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 25 mwezi 02 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

**Angalia**
kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 18 mwezi 02 mwaka 2019.

115067802

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BLASTO GODWIN MAKUNDI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 406 DCH** Aina yake TATA. Yenye chassis namba **MAT382042E7R13224** na injini namba **497TC93HVY828473.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MOR/TR/RB/173/2019.**

115068001

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No........40/2019**

**Ombi la FEDAH ATHANASIO CHAGALA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CHAGALA EDWARD ATANASIO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/02/2019.

115067902

---


**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ramos kulimwa umeme ni majanga Real - Solari

**MADRID, Hispania**

SANTIAGO Solari ameielezea kadi nyekundu ya Sergio Ramos kama ni mjumuiko wa majanga baada ya nahodha huyo wa Real Madrid kutolewa nje kwenye mchezo wa kichapo kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, dhidi ya Girona.

Real Madrid walifungwa bao la pili katika dakika za majeruhi Jumapili wakati wakichapwa 2-1 na Girona waliopo kwenye hatari ya kushuka daraja katika dimba la Santiago Bernabeu.

Beki huyo wa kimataifa wa Hispania alisababisha penalti kwa kuunawa mpira, ambapo alipewa kadi ya njano, na kujikuta akipewa nyekundu, kwani tayari alikuwa na kadi ya njano.

Imekuwa ni wiki ya majanga kwa Ramos, ambapo alipata kadi nyekundu wakati Madrid ikishinda 2-1 dhidi ya Ajax kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16 bora.

Hivyo ataukosa mchezo wa pili dhidi ya Ajax na atakuwapo dimbani kama Real Madrid watafuzu kwenye hatua ya robo fainali.

Ramos sasa amepewa kadi nyekundu mara 20 kwenye La Liga, na kuwa mchezaji anayeongoza katika historia ya mashindano hayo, lakini Solari hakumshutumu nahodha wake.

"Ni majanga," alisema Solari akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kuhusu kadi hiyo nyekundu ya Ramos.

Licha ya Madrid kutokuwa na mchezo wowote katikati ya wiki hii, Solari aliamua kuwapumzisha wachezaji wake nyota, Vinicius Junior, Gareth Bale, Sergio Reguilon na Dani Carvajal dhidi ya Girona.




# Mourinho agusia kufundisha Ufaransa

**MONTPELLIER, Ufaransa**

JOSE Mourinho amebainisha anaweza kufanya kazi kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, wakati alipohudhuria mchezo wa nyumbani wa Lille dhidi ya Montpellier.

Mourinho, ambaye amekuwa akifanya kazi kama mchambuzi kwenye televisheni baada ya kufukuzwa pale Manchester United Desemba mwaka jana, alipigwa picha akipeana mkono na mshambuliaji wa zamani wa Ufaransa, Nicolas Anelka kwenye mchezo huo wa Jumapili.

Mapema mwezi huu Mourinho alipigwa picha akiwa nchini Urusi kwenye michezo ya kwenye barafu, na baadaye akahudhuria mechi kwenye Uwanja wa Pierre Mauroy.

"Angalia nani amealikwa kwenye jukwaa la Uwanja wa Pierre Mauroy kuangalia mpira," klabu ya Lille iliposti kwenye ukurasa wake wa Twitter pamoja na picha ya Mourinho.

"Hapana, hapana, sio ndoto ni kweli huyu ni Jose Mourinho," iliandikwa kwenye Twitter hiyo .

Kocha huyo raia wa Ureno ameshinda mataji ya ligi katika ardhi ya nyumbani kwake Urusi, Italia, Hispania na England na sasa amebainisha anaweza kufanya kazi Ufaransa.

"Naweza kujifikiria mwenyewe kama kocha kwenye Ligue 1," Mourinho alisema ambaye alikanusha uvumi kwake anaweza kuwa kocha wa Benfica, akiiambia beIN SPORTS.

"Mimi ni mtu ambaye nimefanya kazi katika nchini nne tofauti, napenda kujua na kujifunza tamaduni nyingine. Kufanya kazi kwenye ligi nyingine itakuwa ni uzoefu wa kuvutia.

"Kwa sasa nimetulia, najaribu kuishi maisha bora na familia yangu pamoja na marafiki na nafanya hivyo ili nipate nafasi sahihi."



# Solskjaer aona wakati ujao wa Sanchez Utd

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesisitiza kwamba mshambuliaji anayepigania kurudi katika kiwango chake, Alexis Sanchez atarudi katika kiwango chake bora.

Solskjaer amebainisha kuwa mchezaji huyo anaweza kurudi kwenye kiwango baada ya mwaka mmoja wa kuwa na kiwango kibovu tangu alipojiunga na timu hiyo akitokea Arsenal.

Sanchez amefunga mabao matatu tu kwenye Ligi Kuu England katika mechi 13 alizowachezea na alikuwa kwenye kiwango kibovu zaidi katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain na alitolewa nje.

"Nafikiri ni mchezaji mzuri. Ana kipaji, lakini bila shaka kuna mambo mengi ambayo unaweza kukaa chini na kuzungumzia kuhusu kiwango chake," alisema Solskjaer akinukuliwa na Sky Sports wakati United ilipokuwa inajiandaa kuivaa Chelsea kwenye mchezo wa raundi ya tano wa FA jana Jumatatu.

"Ulimuona dhidi ya Fulham, wakati anapopata nafasi, ana kasi, lakini anapoteza mpira kwa haraka," aliongeza kusema kocha huyo raia wa Norway.




# MBAPPE

## AWEKA REKODI PSG IKIUA

**PARIS, Ufaransa**

MCHEZAJI Kylian Mbappe amechagua kuendelea kuitumikia zaidi Paris Saint-Germain licha ya kutengeneza rekodi yake mpya wakati wakiifunga Saint-Etienne.

Mbappe alifunga bao pekee kwenye ushindi huo, akiunganisha pasi ya Dani Alves katika dakika ya 73.

Hilo lilikuwa bao la 19 la Mbappe kwenye mechi 18 za Ligue 1 msimu huu na kumfanya kuwa mchezaji wa kwanza kufikia idadi hiyo ya mabao kwa mechi hizo kwa kipindi cha miaka 45.

"Tulicheza dhidi ya timu nzuri, hasa nyumbani," alisema akiiambia Televisheni ya Canal+.

"Timu chache huwa zinakuja hapa na kupata ushindi. Tunafuraha kwa kuondoka na pointi tatu.

"Tunatakiwa kuendelea kuwa na malengo mazuri. Takwimu zangu ni nzuri, lakini timu ni bora zaidi.

"Kwa uhakika PSG ni bora zaidi kushinda mabao yangu, maana ni timu ambayo inapambana kwa ajili ya kupata ushindi uwanjani na mimi kama mchezaji jukumu langu ni kufunga mabao."

# MESSI

## ananirahisishia kazi Barca - Dembele

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi ni mchezaji bora zaidi kwa wachezaji wenzake kwa sababu anafikiria zaidi mafanikio ya timu, kwa mujibu wa mchezaji mwezake wa Barcelona, Ousmane Dembele.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, Messi na nyota wa Ufaransa, Dembele wamekuwa na msimu wenye mafanikio wakati wakiingia kipindi cha pili cha msimu hapo kwenye dimba la Camp Nou, ambapo kwa pamoja wamefunga jumla ya mabao 43 kwenye mashindano yote msimu huu.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund ameanza kuonekana akiziba vizuri pengo la Neymar, ambaye aliondoka kwenda Paris Saint-Germain mwaka 2017 na amebainisha kwamba anajisikia fahari kucheza pamoja na Messi.

Dembele, ana furaha zaidi kwa sababu nahodha wake huyo anakuwa tayari kubeba majukumu ya timu yote.

"Inavutia, anaufanya mchezo wa soka kuwa rahisi zaidi," amesema Dembele akiiambia tovuti ya Barca.

"Nikimpa mpira anafanya vitu vya kuvutia. Yeye akiwa uwanjani inakuwa rahisi kwa mshambuliaji, kwa sababu timu pinzani inamuangalia zaidi yeye."

Messi na Dembele wote leo Jumanne watacheza pamoja kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16-Bora ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lyon.

# Aguero ataka Man City iweke historia

**MANCHESTER, England**

SERGIO Aguero anahisi Manchester City ina uwezo wa kushinda kila kitu na amewataka wachezaji wenzake kuweka historia ya kushinda mataji manne msimu huu.

Kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola kilirudi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England baada ya kuifunga Chelsea mabao 6-0, na pia wametinga robo fainali ya Kombe la FA baada ya kuifunga Newport County 4-1 kwenye raundi ya tano Jumamosi.

Na sasa City watacheza na Schalke ya Ujerumani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16-Bora na baadaye watakwenda kwenye Uwanja wa Wembley kucheza na Chelsea kwenye fainali ya Kombe la Ligi (EFL), na Aguero amesisitiza kwamba wana uwezo wa kushinda kila kitu.

"Kama ukiingia kwenye hatua hii ni nafasi kwetu kushinda mataji manne, na maana yake kwamba uwezo huo tunao," alisema nyota huyo wa kimataifa wa Argentina akiliambia Gazeti la The Mirror.

"Natarajia inaweza kutokea. Nina matarajio hayo na mara zote nafikiria hivyo. "Najua kwamba hakuna timu iliyoweza kufanya hivyo hapo kabla na ninapenda sisi tufanye hivyo na kuweka historia. Na kwa upande wangu nataka kuwa kwenye historia ya kufunga mabao.

"Naiona timu hii ya Man City ikiwa na uwezo wa kushinda kila kitu na hiyo ndio changamoto yetu kubwa kwa sasa."

Mabao matatu aliyofunga Aguero kwenye ushindi dhidi ya Chelsea yalimuwezesha kufikia rekodi ya Alan Shearer ya kufunga 'hat-trick' 11 kwenye Ligi Kuu ya England na akifikisha jumla ya mabao 17 katika mechi 23 alizocheza msimu huu.

Katika umri wake wa miaka 30, swali kubwa ni kwamba Aguero atamalizia kipindi chake cha uchezaji akiwa City au ataamua kurudi nyumbani kwake, lakini mfungaji huyo amesema hana mpango huo wa kuondoka hapo.

"City ni timu ya mabingwa pamoja na kocha," alisema. "Wapi kwingine nitataka kwenda?

"Nina furaha hapa City na kwa sasa sifikirii kabisa suala la kuondoka. Ni klabu kubwa na mara zote inapendwa na wachezaji wengi na hapa ndipo ninapotaka kumalizia kipindi changu cha uchezaji."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ICARDI ACHAFUA HEWA INTER, MKEWE AFUNGUKA

**MILAN, Italia**

KOCHA Luciano Spalletti amekerwa na kitendo cha Mauro Icardi kutojumuika na wachezaji wenzake katika chumba cha kubadilishia nguo kushangilia ushindi wa mabao 2-1, Inter Milan iliyoupata juzi Jumapili dhidi ya Sampdoria.

Icardi, ambaye 'aliporwa' unahodha na kupewa Samir Handanovic wiki hii, huku tetesi za mustakabali wake wa baadaye zikiwa hazieleweki, aliitazama mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa San Siro akiwa jukwaani kutokana na kuwa majeruhi wa goti, majeraha ambayo yalianza kumuweka nje wakati wakishinda bao 1-0 dhidi ya Rapid Vienna Alhamisi iliyopita.

Mkurugenzi Mkuu wa Inter, Giuseppe Marotta, alithibitisha kuwa straika huyo wa kimataifa wa Argentina bado atapewa ofa ya mkataba mpya licha ya kuonekana kutokuwapo kwa uhusiano mzuri kati ya mchezaji na klabu.

Kikosi cha Spalletti kilihaha kuweza kuziona nyavu kabla ya kupata ushindi kupitia kwa Radja Nainggolan baada Manolo Gabbiadini kusawazisha bao la kwanza la Danilo D'Ambrosio la dakika ya 73.

Wakati kocha wa Inter alikuwa ni mwenye furaha kumuona Icardi uwanjani, ambaye hakusafiri na timu Austria Alhamisi, alikatishwa tamaa kwa straika huyo kutokwenda katika chumba cha kubadilishia baada ya mechi.

"Ukweli nilipendezwa kwa uwapo wake uwanjani na ningeweza kupendezwa zaidi kama angekuja chumba cha kubadilishia nguo na kushangilia ushindi pamoja nasi baada ya mechi, kwa sababu ulikuwa ushindi muhimu na ni sehemu ya kundi hili, hivyo ninachukulia alikuwa na furaha kwa ushindi kama ilivyokuwa kwetu," Spalletti alisema.

"Tunahitaji kurejea katika hali yetu ya kawaida. Katika timu, katika chumba cha kubadilishia wote tunahitaji kufanya kazi katika mwelekeo mmoja.

"Kuna hatua zaidi za kuchukua, ambazo ni kwake kuja chumba cha kubadilishia nguo, kufurahia kuwa sehemu ya kundi hili zuri, kupendezwa kuvaa jezi nzuri ya Inter."

Spalletti alitofautiana na nguli wa klabu, Francesco Totti wakiwa Roma, lakini alifunguka kuwa suala lake na Icardi halijawahi kutokea katika wasifu wake kisoka.

"Ukweli nilipenda kupigiwa makofi na mashabiki baada ya kusawazisha, kama walivyotaka tutokee nyuma na kuwa imara katika wakati huo mgumu," alisema.

"Chakuchanganya ni kwamba tunachoshwa na mjadala huu kuhusu Inter. Nimekuwa na hali fulani katika kazi yangu kwa makini sana, lakini kamwe si kama hii.

"Ushindi ni ishara ya ukomavu, hivyo tunaweza kuanza kuumaliza mlima wa mambo ambayo daima husemwa kuhusu Inter."

Hata hivyo, mke wa Icardi, Wanda Nara, ambaye ni wakala wake, amesema mshambuliaji huyo hana lengo la kuondoka Inter mwishoni mwa msimu licha ya kupoteza unahodha.

Icardi, 25, amekuwa akihusishwa na Real Madrid, Manchester United na Barcelona licha ya kuwa na mkataba na Inter hadi 2021.

Nara akizungumzia kuhusu mkataba wake Jumapili, alisema: "Baadhi wanasema unahodha hauna maana, lakini kwa Mauro ni kama kuchukua mguu wake kuliko mkono.

"Anavaa jezi na sifa ya kitambaa hicho na kama kulikuwa na maamuzi ambayo yangepatikana katika siku za nyuma kuhusu pesa au upendo wa jezi, yeye huchagua jezi daima.

"Sikutoa onyo hata kidogo. Mimi ninawasiliana na Inter, daima ninalishughulikia kwa haraka, lakini nimetafuta tu kuhusu uamuzi wa kukomesha uamuzi wa unaodha wake kwenye Twitter."

## KWA UFUPI

### ZIDANE ATOA MASHARTI CHELSEA

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane, atakubali tu kuinoa Chelsea - na kutwaa mikoba ya Maurizio Sarri - kama atapewa pauni milioni 200 za usajili na klabu hiyo kuhakikisha inambakisha kiungo Mbelgiji Eden Hazard, 28, kwa kumpa mkataba mpya. ***(Sun)***

### MARTIAL, LINGARD KUIVAA LIVER

STRAIKA Mfaransa Anthony Martial, 23, na mshambuliaji wa kimataifa wa England, Jesse Lingard, 26, watarejea kikosini Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Liverpool Jumapili ijayo, licha ya kuwekwa nje "wiki mbili kwa tatu" na kocha wa muda Ole Gunnar Solskjaer. ***(Mirror)***

### POCHETTINO KUIGHARIMU UNITED

Manchester United ipo tayari kuilipa Tottenham pauni milioni 34 kama ada ya fidia ili kumpata kocha Mauricio Pochettino endapo itamsajili kama kocha wa kudumu majira ya joto. ***(Standard)***

### COURTOIS AMWANIKA BALE

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Wales, Gareth Bale, 29, si maarufu miongoni mwa wachezaji wenzake katika dimba la Bernabeu, na anajulikana kama 'The Golfer', kwa mujibu wa kipa Thibaut Courtois. ***(Mail)***

### CHRISTENSEN AKANA KUONDOKA

BEKI wa Chelsea, Mdenmark, Andreas Christensen, 22, amekana taarifa kuwa anataka kuondoka Stamford Bridge, baada ya kuona anapata nafasi finyu ya kucheza kikosi cha kwanza chini ya Maurizio Sarri. ***(Bold via Football London)***

### NEYMAR BADO SANA PSG

MSHAMBULIAJI Mbrazil Neymar, 27, hana mpango wa kuondoka Paris St-Germain kwa mujibu wa baba yake - ambaye aliongeza kuwa "soka linaweza kubadilika muda wowote". ***(Le Perisien - In French)***

### ARSENAL KUMFUATA POPE

Arsenal inajiandaa kwenda kumsajili kipa wa Burnley, Muingereza Nick Pope, 26, ambaye hajaweza kupata nafasi ya kuanza hapo Turf Moor kutokana na majeraha. ***(Sun)***

### OZIL AJIPUMZISHA UTURUKI

KIUNGO wa Arsenal, Mjerumani Mezut Ozil, 30, ameondoka London na kwenda kupumzika Uturuki kwa siku chache baada ya kuachwa katika kikosi cha timu hiyo kilichokwenda kucheza mechi ya Europa League katikati ya wiki. ***(Mirror)***


### MOURINHO KUTUA LIGUE 1

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Chelsea na Real Madrid, Jose Mourinho, anaweza kufungua milango ya kufundisha soka klabu mojawapo ya Ufaransa inayoshiriki Ligue 1. ***(Bein Sports)***

### SPURS UWANJA MPYA APRILI

UFUNGUZI wa uwanja mpya wa Tottenham, umechelewa na sasa pengine unaweza kuwa hadi Aprili mwaka huu kutokana na ratiba ya Kombe la FA. ***(Sun)***

### VALENCIA ATAKIWA WEST HAM



West Ham inapanga kutoa ofa kwa beki wa pembeni wa Manchester United raia wa Ecuador, Antonio Valencia, 33, kama beki wa kulia Muargentina Pablo Zabaleta, 34, ataamua kutundika daluga mwishoni mwa msimu. ***(Mail)***

### ARSENAL, UNITED VITANI

Manchester United na Arsenal zinavutiwa na mshambuliaji wa Birmingham City, Muingereza Che Adams, 22. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# KABWILI AWATULIZA MASHABIKI YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya timu yake kupoteza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya watani zao, Simba, golikipa chipukizi wa Yanga, Ramadhani Kabwili, amesema anaamini ataisaidia timu yake kumaliza katika nafasi ya juu kwenye ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kabwili alisema bado ana nafasi ya kuifanyia "mambo makubwa" Yanga na ni klabu ambayo alikuwa anaipenda tangu akiwa mdogo.

Kabwili alisema kupoteza mechi ni sehemu ya mchezo na amewataka mashabiki na wanachama wa Yanga kutokata tamaa kwa sababu wao wanaongoza ligi wakiwa wameshakusanya pointi nyingi ukilinganisha na Simba ambao wana mechi za viporo.

Kipa huyo alisema pia bado mbio za ubingwa ziko wazi na mechi zilizobakia ni nyingi kwa timu yoyote kutamba kuwa imemaliza kazi. "Nashukuru niko Yanga, ni klabu ambayo nilikuwa na ndoto ya kuichezea tangu nikiwa mdogo, kwa sasa tunaangalia mechi zilizoko mbele, tutaendelea kupambana mpaka siku ya mwisho ya ligi ndipo tutajua nani atacheka na nani atanuna," alisema kipa huyo aliyeanza kung'ara wakati anaitumikia timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 maarufu Serengeti Boys.

Kipa huyo ameanza kuwa chaguo la kwanza la Yanga baada ya kuondoka kwa Beno Kakolanya na benchi la ufundi kuondoa imani kwa mlinda mlango kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Clatous Kindoki.

Yanga iko Mwanza tayari kuwakabili wenyeji Mbao FC katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho Jumatano kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

Vinara hao wa Ligi Kuu watashuka uwanjani kesho wakiwa na kumbukumbu ya kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa watani zao, Simba walichokipata Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini, shukrani kwa mfungaji, Meddie Kagere.

LA 20...



Mbwana Samatta, akishangilia kwa ishara ya kunyoosha kidole juu baada ya kuifungia KRC Genk bao pekee juzi wakati wakikubali kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa wenyeji wao, Club Brugge katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza A Ubelgiji uliopigwa Uwanja wa Jan Breydel mjini Brugge. Hilo ni bao la 20 kwa Samatta msimu huu. **PICHA: BIN ZUBEIRY**

# Kocha Selem View afurahia sare Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Msaidizi wa Selem View inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Khamis Buruti, amesema anaamini timu yake itafanya vizuri katika mzunguko wa lala salama wa ligi hiyo tofauti na ilivyokuwa kwenye mzunguko wa kwanza.

Selem View ililazimishwa sare ya bao 1-1 na Zimamoto katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Mao ze Dong.

Buruti aliliambia gazeti hili jana kuwa timu yake imejipanga vema na imeimarika kwa ajili ya kusaka matokeo chanya kwenye mzunguko huu wa lala salama.

"Timu yangu imejipanga kuhakikisha wachezaji wanafanya vizuri uwanjani na kupachika mabao ili waweze kujiweka katika nafasi nzuri itakayowaondoa katika mstari wa hatari wa kushuka daraja, kwa kifupi tumeimarika tofauti na tulivyokuwa wakati wa mzunguko wa kwanza," alisema Buruti.

Aliongeza kuwa wamejitahidi kwa kufanya usajili mzuri wa wachezaji katika kipindi cha dirisha dogo, wachezaji ambao wanahakika watakisaidia kikosi chao kutimiza malengo ya kubaki Ligi Kuu Zanzibar.

"Tumeanza vizuri katika mchezo wa kwanza wa mzunguko wa pili kwa kutoka sare ya 1-1, si matokeo mazuri kutokana nafasi tuliyopo, lakini pia si mabaya kwa matokea ambayo tulikuwa tunayapata hapo awali, naamini timu ikijituma tutajinasua kushuka daraja," alisema Buruti wakati huu wakiwa nafasi ya 14 na pointi 14.

## Lyon wajiandaa kuikimbia Arusha

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa African Lyon umesema kuwa endapo timu hiyo itabakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, haitatumia tena Uwanja wa Sheikh Amri Abeid ulioko jijini Arusha kama uwanja wake wa nyumbani.

African Lyon inatarajia kuwakaribisha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba katika mechi ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo itakayochezwa leo kwenye uwanja huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi Mtendaji wa African Lyon, Rahim Kangezi alisema uamuzi wa kuondoka Arusha unatokana na kushindwa kufikia malengo waliyoyatarajia wakati wanahamia jijini humo.

Kangezi alisema kwa sasa wanapambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika mechi zao za mzunguko wa pili zinazoendelea ili wasishuke daraja.

**"Tumejipanga kuhakikisha tunabaki Ligi Kuu, tunajua huko chini ni kugumu ndio maana hatutaki kurudi, tutaendelea kujiimarisha kuhakikisha hatupotezi mechi, tunaanza na Simba na wote watakaofuata," alisema kiongozi huyo.**

Aliongeza kuwa changamoto za udhamini zimechaingia kupunguza ushindani kwenye Ligi Kuu na kueleza kwamba timu zimekuwa katika wakati mgumu wa kulea wachezaji katika mazingira bora yanayotakiwa.

Mpaka sasa African Lyon yenye pointi 21 ndiyo inayoburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa imecheza mechi 26 wakati inayoifuata ni Biashara United ya Musoma yenye pointi 23, lakini wamecheza mechi 25 na Yanga ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa wamejikusanyia pointi 58.

Mabingwa wa Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame, Azam FC wenye pointi 49 wako katika nafasi ya pili wakati Simba ambayo inashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika inafuata ikiwa na pointi 39 baada ya kucheza mechi 16.

# Timu za Pemba zateseka Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU za Ligi Kuu zinazotoka kisiwani Pemba, zimeendelea kujichimbia mkiani na kujiweka katika hatari ya kushuka daraja msimu huu katika msimamo wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Timu hizo ambazo ni Chipukizi, New star, Hard Rock pamoja na Opec zimeshindwa kuondoka na pointI baada ya hapo jana ( juzi), kuambulia vichapo katika michezo yao ya kwanza ya ligi hiyo katika mzunguko huu wa lala salama.

Akizungumza na Nipashe mmoja wa viongozi wa timu ya New Star, Said Fakih, ambayo yenyewe ilipokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa maafande wa KVZ, alisema haikuwa bahati yao kutoka na ushindi licha ya timu hiyo kujiandaa vizuri ili kuhakikisha haishuki daraja.

Alisema wachezaji walicheza vizuri na walijituma uwanjani ila tu wameshindwa kuzitumia nafasi wanazozipata na hii ndio changamoto kubwa inayoikabili timu hiyo hali ya kuwa kocha anaendelea kulifanyia kazi.

Aidha, alisema timu hiyo haina nia ya kuchukua ubingwa wala umakamu bingwa, bali wanachoangalia wao ni kuweza kujilinda ili isishuke daraja jambo ambalo ni ngumu kutokana na ushindani uliopo.


"Kufungwa katika mchezo ni kawaida na hii inatokana na kuzidiwa mbinu na timu pinzani kwa hiyo kocha kila anapoangalia mechi anajua mapungufu yapo wapi, hivyo tutajitahidi ili kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri angalau kujinasua na kushuka daraja."alisema

Baada ya matokeo hayo timu ya New Star imeendelea kusota nafasi ya 14 ikiwa na alama 14, Timu ya Hard Rock nayo imebaki nafasi 17 ikiwa na alama 12 huku timu ya Opec ikiwa nayo nafasi ya 18 ikiwa na alama 11 katika msimamo huo wa Ligi Kuu Zanzibar.

# Michezo

Jumanne Februari 19, 2019

Nipashe

Icardi achafua hewa Inter, mkewe afunguka

HABARI UK 30

WAYA...



Casemiro (kulia jezi nyeupe), akiitendea haki krosi ya Toni Kroos na kuifungia Real Madrid kwa kichwa bao la kuongoza wakati wakilala 2-1 nyumbani dhidi ya Girona juzi, anayejitahidi kuokoa bila mafanikio ni beki Pedro Alcala. **HABARI UK. 28**

# KAGERE AANZA KUAGA SIMBA

●●●Kuikosa African Lyon Arusha leo, TP Mazembe, Waturuki wamtaka, Okwi aachwa Dar huku...

**Na Somoe Ng'itu**

MBIO za kuwania taji la Ligi Kuu Tanzania Bara zinatarajia kuendelea leo katika viwanja vinne tofauti hapa nchini wakati African Lyon ikiwakaribisha mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba, watakaoshuka Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha kuanzia saa 10:00 jioni bila ya washambuliaji wao wawili wanaongoza katika klabu hiyo kwa utupiaji mabao.

Simba yenye kumbukumbu ya kumfunga mtani wake katika mechi iliyopita Uwanja wa Taifa, itawakosa mastraika wake, Emmanuel Okwi na Meddie Kagere pamoja na beki Juuko Murshid ambao wote wana kadi tatu za njano.

Kati ya mabao 32, Simba iliyofunga hadi sasa katika mechi 16 ilizocheza, mabao 16 yamefungwa na wachezaji hao wawili huku Kagere akicheka na nyavu mara tisa na Okwi mara saba na kuiwezesha timu yao kuvuna pointi 39 hadi sasa inaposhuka dimbani kucheza na African Lyon iliyohamia Arusha ikiburuza mkia na pointi zake 21.

Aidha, Kagere jana alihojiwa na Redio Ten ya Rwanda na kufunguka kuwa baada ya msimu huu ataachana na Simba na kutimkia TP Mazembe ama klabu moja ya Uturuki ambayo hakuwa tayari kuitaja, lakini akieleza timu hizo kuvutiwa na huduma yake.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu aliiambia Nipashe jana kuwa wachezaji wote walioko Arusha wako salama na wanachosubiri ni muda wa mechi ufike.

"Tuko vizuri, naamini tutatimiza malengo yetu yaliyotuleta huku, nyota tutakaowakosa wa kikosi cha kwanza ambao walicheza mechi dhidi ya Yanga ni Okwi, Juuko na Kagere, ila Kagere yeye tuko naye Arusha kwa ajili ya kuendelea kujifua," alisema kwa kifupi meneja huyo.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, aliliambia gazeti hili jana kuwa kikosi chake kimefanya maandalizi mazuri kwa ajili ya mchezo huo ambao ni muhimu kupata pointi tatu ili kuendelea kujiweka katika nafasi nzuri ya kuchukua ubingwa.

Aussems alisema wachezaji wote wa timu hiyo wako tayari kwa mchezo huo ambao wanahitaji kuondoka na pointi zote tatu kabla ya kurejea Dar es Salaam kukutana na Azam FC.

"Nimewaambia wachezaji wangu, tuna kazi ngumu ya kufanya na tuna michezo nane ambayo ni viporo mikononi, michezo yote ni muhimu kwetu lazima tupambane, ninaziheshimu timu zote, ninajua ugumu wa wachezaji wangu ni umaliziaji, ninalifanyia kazi hili jambo na inawezekana kuleta mabadiliko kwenye michezo yangu inayofuata, ninachohitaji ni pointi tu," alisema Aussems.

Mechi nyingine za ligi hiyo zinazotarajiwa kuchezwa leo ni kati ya Mwadui FC dhidi ya Biashara United wakati Ruvu Shooting wataikaribisha Kagera Sugar na kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga wenyeji Coastal Union wataialika Azam FC.

Ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itaendelea tena kesho kwa Mbao FC kuwakaribisha vinara Yanga kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza na Ndanda FC kuwakabili Singida United kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona uliopo mkoani Mtwara.

## Yanga yatishwa kuangukiwa Mbao kesho

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kocha Mkuu wa Mbao FC, Ali Bushiri, akisema kuwa kikosi chake hakina hofu yoyote kuelekea mechi dhidi ya Yanga itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza, vinara hao watawakosa nyota wake wawili, Feisal Salum "Fei Toto" na Gadiel Michael, imeelezwa.

Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh aliliambia gazeti hili kuwa nyota hao hawatacheza mechi hiyo kwa sababu wanatumikia adhabu ya kuonyeshwa kadi tatu za njano.

Saleh alisema kwa sasa akili yao iko tayari kuwavaa Mbao FC na wamewaandaa wachezaji wao kusahau matokeo yaliyopita ambayo walifungwa na Simba.

"Tunawaza mechi ya Mbao, kanuni zinatubana na kwa maana hiyo tutawakosa Fei Toto na Gadiel, lakini tuna wachezaji wengine watakaocheza katika nafasi hizo, na tunatarajia matokeo mazuri, wote ni wapambanaji," alisema mratibu huyo.

Bushiri alisema wanaifahamu Yanga na nyota wake wamejiandaa kuendeleza rekodi nzuri dhidi ya vinara hao wa Ligi Kuu Bara.

"Tutakuwa nyumbani, naamini tuna kila sababu za kupata ushindi, wao wana uchovu na wamesafiri, hii ni sababu nyingine inayotufanya tuamini kuwa nafasi ya kuondoka na ushindi Jumatano ni kubwa," alisema Bushiri, kocha wa zamani wa magolikipa wa Taifa Stars.

Yanga yenye pointi 58 ikiwa imecheza mechi 24, ndio vinara wa ligi hiyo wakati Mbao FC wako katika nafasi ya sita kwenye msimamo wakiwa na pointi 36 baada ya kushuka dimbani mara 26.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >